**5 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Nne – Tarehe 5 Aprili, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, sasa aulize swali lake.

Na. 38

### Ujenzi wa Barabara ya Bukiko - Bwisya - Ukerewe

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, kwa nini ujenzi wa Barabara ya Bukiko hadi Bwisya kupitia Katende inayosimamiwa na *TARURA* haukamiliki kwa zaidi ya miaka miwili sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo ndio siku ya kwanza nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza kama Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nichukue dakika moja kutoa maneno ya utangulizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na siha njema mpaka wakati huu. Kipekeee naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniteua katika nafasi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namuahidi Mheshimiwa Rais nitafanya kazi kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa ili kumsaidia majukumu yake na kutimiza maono yake kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kukushukuru wewe kama mlezi wetu sisi Wabunge, kwa nasaha zako, kwa mafunzo yako ambayo yamenijenga mimi kiuongozi, lakini pia katika maisha yangu binafsi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenionesha. Kwa heshima kubwa na unyenyekevu niwaombe ushirikiano zaidi sasa ili kwa pamoja tuweze kushirikiana kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutimiza maono yake kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii adhimu pia kuwashukuru akinamama wote na wapigakura wangu wa Mkoa wa Kigoma kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa unaonipa utulivu katika kazi zangu. Baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini ilifanya matengenezo ya kufungua upya Barabara ya Bukiko hadi Bwisya kupitia Katende kilometa 7.54 kwa gharama ya shilingi milioni 141.2. Fedha hizo zilitekeleza kazi za ufunguzi wa barabara na kuunda tuta la barabara kilometa 7.54, ujenzi wa madaraja madogo matatu na ujenzi wa mistari minne ya madaraja madogo. Kazi zote zilikamilika kwa mujibu wa mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imeweka katika mipango yake ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, kufanya matengenezo ya kawaida na kujenga madaraja madogo mawili kwa gharama ya shilingi milioni 30.16 ili barabara iweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kutambua changamoto za kijiografia ambazo zimekuwa zinaathiri utendaji na kupata wakandarasi bora kwenye maeneo ya pembezoni kama Ukerewe, mwaka jana Serikali iliniahidi kutupatia vifaa vya ujenzi kama magreda na kadhalika kwa ajili ya kuondoa changamoto hiyo. Nataka kujua na Wakerewe wanataka kujua hatua ipi imefikiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa pesa za mafuta kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji kwa *TARURA* zinapelekwa mkoani jambo ambalo limekuwa linaathiri wahandisi wilayani kufuatilia hasa inapotokea dharura. Ni upi sasa mkakati wa Serikali kufanya marekebisho ya utaratibu huu? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilitoa ahadi ya kupeleka magreda na vifaa mbalimbali vya ujenzi wa miundombinu ya barabara na ahadi hii mpaka sasa bado haijatekelezwa. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa vifaa hivi katika jimbo lake na inafanya taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kununua vifaa hivyo ili viweze kupelekwa. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itatekeleza ahadi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali inatambua changamoto aliyoiainisha Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na upatikanaji wa fedha kwa wakati kwa ajili ya T*ARURA* kuweza kutoa huduma zake kwa dharura. Kwa muktadha wa suala hili analozungumza Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kuhakikisha inasimamia upatikanaji wa fedha za *TARURA* kutoka Serikali Kuu lakini kutoka katika Serikali ya Mkoa zinapatikana kwa wakati ili kuweza kutimiza mahitaji ya ujenzi wa barabara kwa dharura. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Agnes Hokororo.

Na. 39

**Ujenzi wa Barabara na Mitaro Mji wa Geita**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kujenga barabara na mitaro Geita Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024, Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 77.94 na ujenzi wa mitaro yenye jumla ya kilometa 6.395. Aidha, Geita ni miongoni mwa miji 45 inayotekeleza Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania *(TACTIC)* ambapo mradi utajenga kilometa 17 za barabara kwa kiwango cha lami na kilometa 25 za mitaro kwa gharama ya shilingi bilioni 22.23.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni kuongeza milioni 500 kuwa bilioni moja katika Barabara za *TARURA*, je, ni lini fedha hizo zitatoka?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa barabara nyingi zimekatika kutokana na athari za mvua ikiwemo Chiwale, Masasi Mkoani Mtwara. Je, Serikali ina mpango gani kupitia *TARURA* wa kuhakikisha barabara hizo zinapitika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kweli kuongeza bajeti kutoka shilingi milioni 500 mpaka shilingi bilioni 1.5 na Serikali ina nia ya kutekeleza ahadi hiyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, Serikali itaweza kutimiza ahadi hii na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitalifuatilia suala hili. Tukitoka hapa tunaweza tukakutana tukazungumza ili kujua mustakabali wa masuala ya wananchi wa Geita Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeendelea kutenga bajeti ya kutosha na hivi sasa bajeti ya *TARURA* imetoka shilingi bilioni 272 na imeongezwa mpaka shilingi bilioni 710. Ni ongezeko kubwa, lakini tunatambua kwamba bado kuna mahitaji zaidi. Nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kwa kadri pesa zinavyopatikana Serikali inatambua umuhimu wa barabara hizi za *TARURA* na hasa kwa sababu zinagusa ustawi wa wananchi lakini pia zinagusa ustawi wa uchumi. Kwa hiyo, kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana Serikali ina nia ya kuhakikisha barabara hizi zinajengwa na zinafanyiwa ukarabati. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Ujenzi wa Shule za Sekondari Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari katika Kata za Ngima, Mhongozi na Muungano - Halmashauri ya Mbinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ina Kata tatu za Muungano, Ngima na Mhongozi ambazo hazina shule za sekondari. Aidha, Kupitia Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)*, halmashauri itaendelea kujenga Shule ya Kata ya Muungano *(SEQUIP)*, awamu ya tatu ambapo ilitengewa shilingi milioni 560 katika bajeti ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/2025, Kata ya Mhongozi imetengewa shilingi milioni 560 kwa ajili ya kujenga shule katika kata hiyo kupitia mpango wa kuboresha elimu ya sekondari awamu ya nne. Aidha, Kata ya Ngima itatengewa fedha katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 ili kukamilisha

ujenzi wa shule za kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; hii Kata ya Ngima wananchi kwa kushirikiana na mimi Mbunge tumejenga tayari madarasa manne. Je, Serikali iko tayari kutenga fedha japo kidogo kukamilisha madarasa haya ili yaweze kutumika mwakani Januari?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi wa Kata ya Matiri pamoja na Kata ya Nguzo nao wamejenga Shule ya Sekondari Nguzo pamoja na Benaya Sekondari hazina miundombinu ya kutosha. Je, Serikali iko tayari kupeleka fedha kukamilisha miundombinu ya shule hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia ya kuendelea kuboresha miundombinu ya shule na hivyo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha Serikali itaweza kujenga madarasa hayo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, Serikali inatambua jitihada ambazo zimefanywa na wananchi wa *Mbinga DC* za kujenga Shule ya Sekondari ya Benaya na Nguzo na shule hizo tayari zimeshasajiliwa na zina wanafunzi mpaka kidato cha pili. Kwa kuzingatia miundombinu ambayo bado haijakamilika katika shule hizo, Serikali kupitia bajeti ya halmashauri ya 2024/2025 imepanga kutumia shilingi milioni 62.5 kwa ajili ya shule hizo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya ukamilishwaji wa miundombinu ya shule hizo ili kuongeza fedha kulingana na upatikanaji wake kwa ajili ya

kuhakikisha kuwa ujenzi wa shule hizo unakamilishwa na kuunga mkono jitihada za wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 41

**Ujenzi wa Soko la Kisasa - Singida Mjini**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga soko la kisasa Singida Mjini kwani Soko Kuu la Ipembe ni la muda mrefu na miundombinu yake ni chakavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa miundombinu ya Soko Kuu la Singida Mjini lililopo Mtaa wa Ipembe ni ya muda mrefu na ni chakavu. Halmashauri ya Manispaa ya Singida iliandaa andiko la kuomba fedha za ujenzi wa Soko la Vitunguu la Misuna na Soko Kuu la Ipembe ambalo limependekezwa kujengwa upya.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia Soko la Vitunguu la Misuna lilipata ufadhili kwa awamu ya kwanza na shughuli za upembuzi na usanifu wa mradi zinaendelea. Kwa upande wa Soko Kuu la Ipembe, Mkandarasi anatazamiwa kuanza utekelezaji wa mradi ifikapo Disemba, 2024. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, swali la nyongeza

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize swali dogo moja la nyongeza. Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wakati wa ujenzi wa Soko hili jipya la Ipembe kwamba shughuli za wafanyabiashara hazitaathirika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika taratibu za ujenzi wa miradi hii na hususani miradi ambayo tayari wananchi wanafanyia shughuli zao za kiuchumi katika maeneo hayo, utaratibu utazingatiwa kwa kushirikisha wananchi wenyewe lakini pia Viongozi wa Halmashauri. Mheshimiwa Mbunge tutashirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuona ni namna gani tunawawezesha wananchi wale kuendelea na shughuli zao bila kuathirika lakini pia hilo soko linajengwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuliboresha Soko la *Stereo* Temeke liendane na ukuaji wa Mji wa Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumekwishafanya tathmini ya masoko makubwa ya kimkakati katika halmashauri zetu zote ikiwemo Halmashauri ya Temeke katika Soko lile la *Stereo*. Tayari Serikali imeshaweka mpango kwanza kupitia mapato ya ndani ili ianze kutengwa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wakati Serikali Kuu inatafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi hizo. Kwa

hiyo, naomba nitumie fursa hii kumwelekeza kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kuweka kipaumbele katika bajeti zake ili tuanze kuboresha Soko la *Stereo*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itajenga soko zuri katika Wilaya ya Nachingwea kwa sababu lililopo limechakaa sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kujenga masoko mazuri ili kuboresha huduma kwa wananchi likiwemo soko hili katika Halmashauri ya Nachingwea. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge amekuwa akishirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nachingwea na niwahakikishie tu kwamba tumeshamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nachingwea kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kujenga soko lile ili tuweze kuona tunapata fedha kupitia mapato ya ndani na Serikali Kuu kwa ajili ya kuboresha soko hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itajenga Soko la Manzese lilipo Kata ya Misufini, Manispaa ya Songea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Soko hilo la Manzese lililoko Manispaa ya Songea linamilikiwa na Halmashauri na tulishaelekeza Halmashauri kupitia Wakurugenzi na Menejimenti ya Halmashauri kufanya tathmini na kuweka vipaumbele vya masoko. Kwa hiyo, naomba nilichukue suala hili

la Mheshimiwa Mbunge na baada ya kikao hiki tutawasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea ili tuweze kujua *status* ya utekelezaji ikoje na tuweze kuona namna gani tunapata fedha kwa ajili ya kuboresha soko hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga soko jipya Wilayani Lushoto maana lililopo ni la tangu mkoloni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, soko ambalo linahitajika katika Halmashauri ya Lushoto ni moja ya vipaumbele vya Serikali, kazi kubwa ambayo inafanywa ni halmashauri zenyewe kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kulingana na *design* ya masoko yenyewe.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Manispaa, Halmashauri na Majiji kote nchini kuhakikisha kwanza wanafanya tathmini ya uhitaji wa masoko hayo, lakini pia kuandaa makadirio ya gharama na kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu wakati huo na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo kwa awamu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa shughuli ya kiuchumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ni pamoja na uvuvi wa samaki na dagaa lakini hatuna soko la kisasa. Je, ni lini Serikali itajenga soko la kisasa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika maeneo ya uvuvi tunahitaji kuwa na masoko ya kisasa ya samaki na hicho ni kipaumbele cha Serikali. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu tulishafanya ziara pale Halmashauri ya Rorya na miongoni mwa eneo ambalo tulipita ni pamoja na maeneo ya masoko. Nimhakikishie tu kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili twende kujenga Soko la Kisasa la Samaki katika eneo hilo la Rorya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa kujenga Soko la Kisasa katika eneo la Madira ambalo michoro yake tumeshawasilisha Wizarani? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Halmashauri ya Meru kwa kupitia Mheshimiwa Mbunge Pallangyo kwa kuandaa michoro na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama maelekezo ya Serikali yalivyopelekwa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa tutafanya tathmini kuona gharama hizo zinazohitajika na kuona vyanzo vya fedha kupitia Serikali Kuu, lakini pia kupitia mapato ya ndani ili tuanze kujenga soko hilo kwa awamu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Masasi haina soko kabisa, ni lini Serikali itajenga soko katika Kijiji cha Mbuyuni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Lulindi kwamba Serikali ilikwishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanatenga maeneo mahsusi kwa ajili ya ujenzi wa masoko. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri hii ya Masasi Vijijini kwa kutenga eneo hilo, namwelekeza Mkurugenzi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI aanze kutenga fedha kwa mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo wakati Serikali pia ikitafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Kuongezeka kwa Kina cha Maji Bahari ya Hindi**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, kuna ukweli kwamba kina cha maji ya Bahari ya Hindi hapa Tanzania kimeongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na nini athari zake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Selemani Jafo, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli kina cha maji ya Bahari ya Hindi hapa Tanzania kimeongezeka kutokana na kuendelea kuongezeka kwa joto la dunia linalosababisha kuendelea kuyeyuka kwa barafu katika maeno mbalimbali duniani. Kwa mujibu wa utafiti na vipimo vilivyopo maji ya Bahari ya Hindi katika Pwani ya Dar es Salaam yanaongezeka kwa wastani wa kiasi cha milimita sita kwa mwaka tangu mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, athari za kuongezeka kwa kiwango cha maji ya bahari ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa mmomonyoko na upotevu za fukwe;

(ii) Uharibifu wa miundombinu kama vile gati za bahari, barabara, nyumba ofisi na masoko;

(iii) Upotevu wa bioanuwai muhimu ikiwemo mikoko na nyasi za bahari;

(iv) Upotevu wa ardhi ya kilimo, makazi na visima vya maji baridi kuingiwa na chumvi na mafuriko ya mara kwa mara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna ongezeko la kina cha maji kule baharini, je, Serikali ina mpango gani wa kuyalinda maeneo haya ili yasije yakazama kwenye maji huko siku za mbeleni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa hili ni tatizo la kidunia, je, Serikali inashirikianaje na wadau mbalimbali wa kimataifa ili kukabiliana na changamoto hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya mtaalam mbobezi, Mtaalam wa Kilimo na Sayansi ya Udongo – Profesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika kuona hili ndiyo maana mwaka 2021 tulifanya rejea ya Sera yetu ya Mazingira ya mwaka 1997, lakini mwaka 2022 tulikuja na mpango mkakati wa kuona jinsi gani tunashughulikia masuala mbalimbali ya kimazingira ikiwemo na suala hili la uharibu wa mazingira hasa upande wa fukwe. Kwa hiyo katika hili naomba niwahakikishie Wabunge kwamba tumejipanga vizuri na hivi karibuni tunakuja na Sera nyingine mpya ya *Blue Economy* ambayo itaangalia *corridor* zote za bahari na jinsi gani tunaweza kuzilinda. Kwa hiyo, Serikali iko mbioni kuhakikisha kwamba tunafanya mambo hayo kwa uhakika wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano tunafanya vipi? Kwanza tumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan katika *agenda* yake ya mazingira, tunakumbuka Mkutano wa *COP 26* alipokuwa Glasgow alivyotangaza duniani *agenda* ya mazingira na kufanya *resource mobilization* kutafuta wadau mbalimbali katika upande huu. Katika hili naomba niwahakikishie kwamba, Serikali ina mahusiano mazuri sasa hivi na *UNEP, FAO* na *UNDP*. Pia sasa hivi tuna mchakato mkubwa wa kujiunga na Shirika kubwa la *GGI* kule Korea kwa lengo kubwa la kuweza kupata fedha ili kusaidia shughuli za maendeleo katika nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona, maswali mafupi na Mheshimiwa Waziri majibu mafupi.

Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali ya Mkoa wa Manyara imeendelea kupambana kuokoa kina cha Ziwa Babati na tumeshaomba fedha zaidi ya

miaka mitatu na Mheshimiwa Waziri amekuwa akituahidi mara kwa mara…

**SPIKA:** Swali.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Je, nini kauli ya Serikali sasa juu ya kuliokoa Ziwa Babati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inakuja na mpango katika mwaka huu wa bajeti kwa Ziwa Babati na Ziwa Jipe na maeneo mengine kuhakikisha kwamba tuna-*address* changamoto ya magugu maji katika maeneo haya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, je, kuna mpango gani wa kukinusuru Kisiwa cha Mtambwe Mkuu kilichopo katika Jimbo la Mtambwe kuzama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kule Pemba eneo hili lina changamoto kubwa na ndiyo maana tulituma wataalam wetu sasa hivi kupitia maeneo mbalimbali. Katika hilo ni kwamba tutaainisha nini kifanyike, lakini kubwa tutashirikiana na wananchi wetu katika maeneo mbalimbali hasa kutoa elimu ya kwanza ya jinsi ya kuyalinda maeneo hayo hasa kupanda miti katika maeneo hayo. Hata hivyo tutaenda kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kuta za bahari katika maeneo kama hayo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa athari hizi pia zinasababisha theluji iliyopo kwenye Mlima Kilimanjaro kuyeyuka. Je, Serikali ina mpango gani kugawa miche kila siku iitwayo siku kwa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro ili waendelee kuotesha mgombani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mama yangu Shally Raymond, Mbunge machachari kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkoa wa Kilimanjaro tuna changamoto kubwa na hasa kulinda Mlima ule Kilimanjaro na hapa naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wenzetu wa *TFS* wameendelea kufanya kazi hii, naomba nimpongeze Profesa Dos Santos Silayo wa *TFS* kwa sababu yeye ameamua kuweka nguvu kubwa ya upatikanaji wa miche katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kugawa. Kwa hiyo, nawaomba akinamama wa Mkoa wa Kilimanjaro wawasiliane na *TFS* kwa maeneo hayo, naamini watapata miti kwa ajili ya kupanda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nadhani umemwita Mheshimiwa Shally Raymond, Shayrose ama kitu kama hicho, anaitwa Mheshimiwa Shally Raymond. *(Makofi)*

Mheshimiwa Simai, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea kutambua athari za ongezeko la maji ya bahari zinazoendelea kutokea kule Nungwi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Simai, kwa sababu mimi na yeye

tumefika katika eneo la Jimbo lake pale na kweli kuna changamoto kubwa sana, hata upande wa soko mpaka msikitini pale kuna changamoto kubwa. Sasa hivi Serikali inatafuta fedha mahsusi ili kuhakikisha tunasaidia eneo la Nungwi kwa sababu changamoto yake ni kubwa. Kwa hiyo, Serikali tunaendelea kuhangaikia fedha na wewe nimekuambia kwamba tuna vikao mbalimbali, Mheshimiwa Mbunge nimeongea naye, vikao mbalimbali vya kuangalia namna ya kusaidia *specific* eneo la Nungwi kutokana na uharibifu unaotokea pale. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Kuhamasisha Balozi kufungua Ofisi za Ubalozi Mdogo Zanzibar**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuzihamasisha Balozi na nchi mbalimbali duniani kufungua Ofisi za Ubalozi Mdogo Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashiriki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki hufanya uchambuzi wa kimkakati kwa ajili ya kuimarisha na kudumisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi nyingine na kuzishawishi kufungua Ofisi za Ubalozi nchini kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Uchambuzi huo unahusu ushirikiano katika masuala mbalimbali ikiwemo uchumi, biashara, utalii, utamaduni, elimu na utaalam katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Kitaifa wanapopata nafasi ya kukutana na Waheshimiwa Mabalozi huwashawishi wafungue Ofisi Ndogo za Kibalozi Zanzibar, kadhalika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hutumia fursa hiyo kukutana na Waheshimiwa Mabalozi wanapoomba miadi na kuwashawishi wafungue ofisi ndogo za kibalozi Zanzibar. Hadi sasa tayari zimekwishafunguliwa Ofisi za Balozi Ndogo tano Zanzibar ambazo ni China, Oman, India, Msumbiji na hivi karibuni Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE)*. Ni matumaini ya Wizara kuwa, jitihada zinazoendelea kufanywa zitawezesha Balozi nyingi kufungua ofisi zake ndogo Zanzibar. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imeshafanya kazi kubwa ya kuwa na *almost* Balozi ndogo tano kule Zanzibar. Je, Serikali ina mpango gani wa kudumisha na kuimarisha huduma za kidiplomasia katika zile Balozi ambazo ziko pale Zanzibar ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa *VISA* kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kuja na mpango maalum wa kisera na kimkakati ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum kama vile viwanja ili kuvutia nchi zaidi kuweza kuanzisha Balozi zake ndogo kule Zanzibar? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza sikulisikia vizuri kuhusu *VISA*.

**SPIKA:** Balozi ambazo tayari zina Balozi ndogo Zanzibar, Wizara ama Serikali mnahakikishaje zinaweza kutoa hiyo huduma kwa wakati kwa watu wanaoomba huko Zanzibar.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ofisi yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje Zanzibar ina ushirikiano mzuri sana na hizi ofisi ndogo za Ubalozi zilizopo Zanzibar na muda wote tumekuwa tukiwapa ushirikiano mzuri na hakujawahi kuwa na tatizo la kutoa *VISA* kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni wazo zuri kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kujenga Ofisi za Kibalozi Zanzibar na hili ni wazo zuri na tunalichukua, lakini hata hivyo hii haijawa changamoto kwani kipindi chote Balozi zinapotaka kufungua hizo ofisi zao ndogo Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikitoa ushirikiano mkubwa na hiyo imefanyika kwa Ubalozi wa China, imefanyika kwa Ubalozi wa Oman na hivi karibuni kwa Ubalozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Utaratibu wa Kupima Ufanisi wa Balozi kwa Kutumia Hadidu za Rejea Zinazofanana**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kupitia utaratibu wa kupima ufanisi wa Balozi zetu wa kuimarisha Diplomasia ya Uchumi kwa kutumia hadidu za rejea zinazofanana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapitia upya utaratibu wa kupima ufanisi wa Balozi zetu katika kuchangia na kuimarisha diplomasia ya uchumi kwa kutumia hadidu za rejea zinazofanana. Katika kufanikisha utekelezaji wake Wizara imeandaa mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ambao umeainisha maeneo saba ya kipaumbele. Maeneo hayo ni, kuongeza mauzo ya bidhaa nje, kuongeza uwekezaji kutoka nje, kukuza utalii, kuimarisha ushirikiano wa kimaendeleo, kuongeza fursa za ajira na elimu kwa Watanzania katika nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa, kuimarisha taswira ya nchi yetu kimataifa na kuimarisha uwezo wa Wizara kuratibu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Katika kila kipaumbele, kumewekwa viashiria vya mafanikio ya utekelezaji wa mkakati huo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka Serikalini na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Serikali inapitia utaratibu wa kupima ufanisi wa Balozi zetu kwa kuzingatia viashiria vilivyopo kwenye mkakati. Aidha, utaratibu wa upimaji wa ufanisi wa Balozi zetu utatumia hadidu za rejea zinazofanana ingawa uzito wa kila kigezo hautolingana kutokana na utofauti wa mahali na jukumu la kila Balozi. Kwa mfano, Balozi zinazowakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali zinakuwa na viashiria tofauti kidogo kulinganisha na Balozi zinazowakilisha nchi yetu kwenye mashirika ya kimataifa ambapo mkazo utawekwa zaidi kwenye kuimarisha ushirikiano wa kimaendeleo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo saba ya kipaumbele yaliyoainishwa katika diplomasia ya uchumi yanasimamiwa na Wizara nyingine za Kisekta, je, Wizara ya Mambo ya Nje imeweka utaratibu gani kuhakikisha Wizara hizi za Kisekta pia zinaweka kipaumbele katika maeneo haya saba ya kipaumbele katika diplomasia ya uchumi ikiwemo kutenga bajeti ili kuleta tija ilikusudiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na kuwa na hadidu za rejea *(KPI's)* ili Serikali iweze kupima balozi zetu kwa ufanisi zaidi, je, Serikali ipo tayari kuandaa ramani ya fursa za uchumi ili balozi zetu ziweze kujua ni fursa gani ambazo zinapambania katika kila nchi ambazo balozi zetu zipo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO):** Mheshimiwa Spika, tunatarajia mwishoni mwa mwezi huu tuuzindue huu mkakati ambao ni wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa ujumla wake. Ndani yake ndiyo kuna hayo maeneo saba ambayo pia yatatumika kwenye kupima balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuzindua pale Wizarani na kwenye Serikali na tukaanza utekelezaji wake wa miaka mitatu, tutahakikisha tunaweka mkakati mzuri wa kuzishirikisha wizara na sekta nyingine, ambao tayari *of course* tayari upo, na si wizara na sekta bali na taasisi na sekta binafsi ili tuweze kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mkakati huu unakuwa na ufanisi ambao tunautarajia. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tunakubaliana kwamba tutalichukua.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili, ramani ipo lakini haina *clear picture* ndiyo maana sasa tunataka tuingie kwenye kumpa vigezo kiongozi aliyeko kwenye ubalozi wetu vya kuhakikisha tunashirikiana kutengeneza ramani ambayo ina mwonekano mzuri zaidi na taarifa sahihi kwa umma ili kama anavyopendekeza Mheshimiwa Neema tuweze kuweka wazi kirahisi zaidi na kila mtu aweze kujua eneo analoweza kufanyia

biashara. Balozi iweze kuonesha na kuonekana inawajibika kwenye eneo gani ili kwa pamoja tuweze kufanikisha diplomasia ya uchumi. Kwa hiyo, ushauri huo pia tumeuchukua.

**SPIKA:** Kwenye jibu lako umesema ramani haina nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO):** Mheshimiwa Spika, ramani haielezi vizuri fursa za kiuchumi ziko eneo gani, nilitumia neno *clear picture.*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Huduma ya Mionzi kwa Wagonjwa wa Saratani Nchini**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, hospitali ngapi zinatoa huduma ya tiba ya mionzi kwa wagonjwa wa saratani hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, majibu.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ina jumla ya vituo vinne ambavyo vinatoa huduma ya matibabu ya saratani nchini kwa njia ya mionzi. Vituo hivyo ni Taasisi ya Saratani *Ocean Road*, Hospitali ya Kanda Bugando, Hospitali ya Binafsi Besta na Hospitali ya *Good Sammaritan St. Francis,* Ifakara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na taratibu za uwekezaji kwa kuongeza vituo vingine vinne kwa ajili ya matibabu ya saratani kwa njia ya mionzi ambavyo ni Hospitali ya Benjamin Mkapa, Aga Khan, *KCMC* na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya kwa Tanzania Bara na kimoja kwa Visiwani, kwa kujenga majengo na kuviwezesha vifaa vitakavyotumika kutibu wagonjwa wa saratani kwa njia ya mionzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza; je, Serikali haioni umuhimu wa kuleta huduma hii ya mionzi katika Hospitali ya Kanda ya Kusini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; wagonjwa wengi wa saratani wanaenda hospitali wakati hali imekuwa mbaya, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha iwafikie wanawake wengi ambao wako vijijini ili waweze kutibiwa magonjwa haya kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Tunza kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Ni kweli Serikali tunao mpango wa kujenga huduma za saratani kwa njia ya mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa bajeti na wewe umekuwa ukituhimiza sana na kutusukuma, tunataka tukamilishe kwanza Mbeya kwa sababu kanda ina mikoa mingi kama vile Katavi, Rukwa, Mbeya, Iringa na Njombe ambako kuna watu wengi, takribani zaidi ya milioni 15 na wanasafiri hadi kuja *Ocean Road* kwa ajili ya kupata huduma za saratani kwa njia ya mionzi. Kwa hiyo mwaka huu kipaumbele chetu ni angalau kwanza tumalize kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; pia, tukamilishe

*KCMC* na watu wa Kusini tutakuja kwenu kwenye Bajeti ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili la Mheshimiwa Tunza, suala la elimu nakubaliana naye kwa asilimia kubwa, kwa sababu bahati mbaya Tanzania tunakadiriwa tuna wagonjwa wapya wa saratani kila mwaka takribani 40,000, lakini wanaofika kwenda kupata huduma ni kama asilimia 28 hadi asilimia 30. Hao wanaokwenda hospitali kupata huduma ni asilimia zaidi ya 70 wanafika hospitali tayari saratani ikiwa katika hatua ya tatu au ya nne ambapo inakuwa ngumu kutibu au matibabu yanachukua muda mrefu. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia njia mbalimbali za kutoa elimu ya kupima saratani. Niwahimize sana Waheshimiwa Wabunge kwenye mikutano yenu ya hadhara kuwakumbusha wananchi kupima saratani kwa sababu saratani inatibika, ikigunduliwa mapema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kinga ni bora zaidi tiba ifuate baadaye; je, Serikali ina mpango gani wa ushirikiano na wadau husika katika kuimarisha udhibiti wa vile vinavyosadikiwa husababisha *cancer,* kama vile viuatilifu vyenye sumu ambavyo vimepigwa marufuku lakini bado vinaendelea kusambaa na kuleta shida ambazo zinasababisha gharama kubwa katika...

**SPIKA:** Mheshimiwa tafadhali maliza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** ...matibabu ya *cancer* na kuongeza bajeti kwa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kinga ni bora kuliko tiba, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha tunashughulikia visababishi vya saratani ikiwemo kemikali zenye madhara kwa kutumia Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Tuna

vigezo na masharti ya jinsi ya kutunza, kusafirisha na matumizi ya *chemical,* lakini nataka tukiri hatujafanya vizuri katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano saratani inayoongoza ni saratani ya mlango wa kizazi. Serikali imeanza kutoa chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwathibitishia Watanzania hususani wazazi kwamba chanjo hii ni salama, haihusiani na kuja kuzuia msichana kupata ujauzito au masuala ya uzazi wa mpango. Chanjo hii ni salama na inawakinga wasichana kupata saratani ya mlango wa kizazi. Ukienda *Ocean Road* na ukienda Bugando utaona...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa gharama za usafishaji wa figo nchini imekuwa kubwa sana. Je, Serikali ina mkakati gani sasa kupitia Bima ya Afya kwa Wote kupunguza gharama hii kwa Watanzania?

**SPIKA:** Hilo litakuja kama swali la msingi. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wanaweka Madaktari kwenye hospitali zetu za wilaya ili kuchunguza saratani mapema kabla haijafikia *stage* ya mwisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali tumeshaelekeza kila kituo angalau kila mwezi kuwe na siku moja kwa ajili ya wananchi kupima saratani *(free and open day)* kwa ajili ya watu kupima saratani. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwataka Waganga Wafawidhi wa Vituo vyote vya Serikali vya kutoa huduma za afya kutenga angalau siku moja kila mwezi iwe ni siku maalum ya watu

kupima saratani. Madaktari wa Wilaya na Mikoa wasimamie maelekezo haya ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Katika vituo vyetu vya afya na hospitali zetu suala la watoto wenye umri chini ya miaka mitano pamoja na wajawazito kuombwa fedha kwa ajili ya matibabu limekuwa ni la lazima; je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba hilo tatizo linakwisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, bado sera ya Serikali kuhusu matibabu bila malipo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wazee wasio na uwezo na wajawazito haijabadilika iko pale pale. Nataka kukiri ipo changamoto ya utekelezaji wa sera hii. Tunaamini kupitia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote tutaweza kutatua changamoto hii kwa kiasi kikubwa kwa sababu sasa watu hawa watapewa kadi ya bima ya afya na hivyo itawawezesha kupata huduma za matibabu bila malipo kama inavyoelekezwa na Sera ya Afya ya mwaka 2007.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, wagonjwa wa saratani wanaendelea kukumbana na kadhia kubwa ya gharama za matibabu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama kubwa zinazotumika kwenye ugonjwa wa saratani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Kunti Majala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli gharama za saratani ni kubwa, lakini tunajitahidi kupata wadau ambao wanaweza kutupatia dawa kwa gharama nafuu. Sasa hivi tunakamilisha mazungumzo. Kuna wadau kama wawili, watatu wako tayari kutupatia dawa za saratani ambazo ni *brand,* lakini kwa bei ya kushuka. Tunakamilisha mazungumzo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kwa wagonjwa wasio na uwezo kati ya jambo kubwa ambalo Bunge lako hili limefanya ni kupitisha Sheria ya Bima Afya kwa Wote ambayo siyo tu wasio na uwezo watapata Bima ya Afya, lakini pia itagharamia magonjwa sugu ikiwemo magonjwa ya saratani pamoja na watu wanaosafisha damu au *dialysis* kwa sababu gharama ni kubwa sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wilaya ya Hai ina wataalam watatu tu wa mionzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wataalam wa mionzi ili waweze kubaini hatua za awali za saratani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Saashisha kwa swali lake zuri. Ni kweli kati ya eneo ambalo tuna uhaba mkubwa wa wataalam ni pamoja na wataalam wa mionzi. Serikali kupitia mpango wa Dkt. Samia *Supper Specialisation Programme* tunafadhili madaktari kusomea Udaktari Bingwa wa Mionzi. Sasa hivi sina takwimu, lakini kwenye bajeti yetu tutaonesha ni wangapi sasa hivi wako shule na wangapi watamaliza. Tunaamini ndani ya miaka mitatu au minne tutakuwa tumesogeza au tumepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto hii ya uhaba wa wataalam wa mionzi ambao pia si tu watashughulikia masuala ya saratani lakini na magonjwa mengine ya mifupa na viungo vingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wapo Watanzania wenzetu hasa wakiwepo wa Mkoa wa Iringa hawana bima ya afya na hawana uwezo kabisa. Wanapokwenda Dar es Salaam kwenda kusubiria haya matibabu ya mionzi hawana sehemu ya kuishi na hawajui watakula nini. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuwasaidia Watanzania kama hawa ili na wao waweze kutibiwa kabisa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa swali lake zuri. Pia, linaonesha ni Mbunge anayejali watu, kuwathamini, ana huruma na utu. Sisi Wizara kwa kweli kazi yetu kubwa ni kuhakikisha wagonjwa wanapata matibabu, lakini ni kweli kwa sababu wagonjwa hawa inabidi wasubiri na wana changamoto ya malazi na vyakula, naomba nilichukue tukalifanyie kazi hapa sina jibu mahususi.

Mheshimiwa Spika, wapo wafadhili mbalimbali ambao wanajitokeza kuwapelekea chakula na kutoa misaada. Nitoe rai kwa Watanzania kujitokeza kuwasaidia wagonjwa wa saratani ambao wanatibiwa katika Taasisi yetu ya Saratani ya *Ocean Road*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa James Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga.

Na. 46

**Ujenzi wa Uzio Kuzuia Mamba Sehemu za Kuchota Maji Buchosa**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA K.n.y. MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kujenga uzio katika sehemu za kuchota maji ili kuzuia vifo vinavyosababishwa na mamba Buchosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imejenga uzio au vizimba vya mfano kwa ajili ya kuzuia mamba katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yana changamoto ya mamba. Kwa upande wa Jimbo la Buchosa, Wizara imejenga vizimba viwili vyenye thamani ya shilingi 60,470,000 katika Vijiji vya Kanyala na Izindabo vilivyopo Kata za Bulyaheke na Lugata kwenye Tarafa ya Buchosa.

Mheshimiwa Spika, halmashauri za wilaya zinahimizwa kujenga vizimba katika maeneo yenye changamoto ya mamba. Wizara inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuzihimiza halmashauri zao kutenga bajeti itakayowezesha ujenzi wa vizimba katika maeneo yao. Aidha, Wizara itatoa wataalam kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa vizimba hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanyama hawa wamekuwa wengi sana katika Ziwa Victoria, je, Serikali ina mpango gani wa kuwavuna au kuwapunguza ili angalau wananchi wasipate adha hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa jambo hili linahitaji elimu kubwa kwa wananchi, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ili kuhakikisha kwamba wanyama hawa wakali hawasumbui wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hili la kuwavua Wizara ina mikakati ya aina mbili.

Mkakati wa kwanza ni kufanya uvuvi kwa kutumia mfumo wa uvunaji wa kitalii. Pili, pale tunapopata taarifa kwamba eneo fulani limekuwa na mamba wengi tumekuwa tukifanya *operation* za kuwavua mamba hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na elimu, timu zetu ziko uwandani zinaendelea kutoa elimu kwa wananchi ya jinsi ya kuweza kutumia vizuri maeneo ya pembezoni mwa maziwa na mito ambayo yana mamba wengi, hususan kuwaelekeza jinsi ya kuacha kutumia maeneo hayo nyakati za usiku ambazo si rahisi kuweza kukwepa mashambulizi haya ya mamba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mikakati mingi ya kushughulika na mamba inaonekana kufeli, je, Serikali kwa nini isichukue njia ya kuhamisha mamba hawa ambao wamekuwa wakileta madhara makubwa maeneo mengi katika nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutauwasilisha kwa wataalam wetu ili uweze kufanyiwa kazi tuone jinsi ambavyo jambo hili linaweza kushughulikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti tembo katika Kata ya Engikaret Wilayani Longido ambao wamekuwa wasumbufu sana na wanasababisha madhara kwa wanadamu?

**SPIKA:** Sasa hili la tembo nadhani lije kama swali la msingi, tembo ama ndovu, lakini lije kama swali la msingi kwa sababu maeneo Wabunge wanazungumzia na hili la leo hapa linazungumza kuhusu mamba.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nimeahirisha.

**SPIKA:** Aaa, ameahirisha. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Halmashauri ya Ushetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza kusimama mahali hapa kwa nafasi hii, naomba kwanza kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na zawadi ya uhai. Pia, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyonayo kwangu. Namhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, jukumu hili nitalifanya kwa weledi kwa maslahi mapana ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi pia, umekuwa mlezi wetu, nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, lakini nimekuwa Mwenyekiti wa Bunge, nakushukuru sana kwa malezi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambao nimefanya nao kwa kipindi chote kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa ushirikiano wenu wakati wote nilipokuwa Mwenyekiti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa, nawaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Ushetu ambacho ni kituo daraja C kinajengwa kwa kutumia nguvu na michango ya wananchi. Ujenzi wake umesimama ukiwa umefikia kwenye hatua ya msingi. Tathmini kwa ajili ya kumaliza ujenzi ili kuunga mkono jitihada na nguvu za wananchi ilishafanyika na kiasi cha shilingi 300,265,723 kinahitajika. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ahsante *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimekuwa nikiahidiwa toka mwaka 2021 kwamba fedha itatengwa, mwaka 2022/2023, niliahidiwa tena fedha itatengwa. Pia, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika katika Kituo cha Polisi na kuongea na wananchi na akawaahidi kwamba fedha zitapatikana, lakini leo napewa jibu kwamba…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba Serikali ni endelevu, huyu ni Naibu Waziri mpya, sasa ukisema Naibu Waziri alikuja siyo huyu aliyekuja. Kwa hiyo, wewe muulize hapo ili aanzie mahali na yeye pa kukujibu leo. Ahsante sana.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba sasa mkakati mkubwa wa Serikali kwa sababu tena 2025/2026 imekuwa kama ni mbali zaidi. Ni nini sasa mkakati wa karibu wa Serikali wa kukamilisha Kituo hiki cha Polisi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tuna Kituo cha Polisi Kata ya Bulungwa, tuna Kituo cha Polisi Kata ya Uloa na Kata hii ya Nyamilangano havina magari wala usafiri. Eneo la Ushetu linaingiliana na watu wa nchi jirani, je, nini mkakati wa Serikali kupeleka magari ya kuhudumia wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina nia ya dhati kuhakikisha kwamba Kituo hiki cha Polisi kinakamilika. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tutatenga fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ili kituo hiki kiweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa magari, hivi sasa Serikali imeshanunua magari kwa ajili ya ofisi za polisi katika wilaya zote hapa nchini na fedha itakapopatikana tutanunua pia magari kwa ajili ya vituo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Bado lingine.

**SPIKA:** Bado lingine?

**WABUNGE FULANI:** Limeshajibiwa.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Tanzania Kuruhusu Uraia Pacha**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, kwa nini Tanzania hairuhusu uraia pacha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Uraia wa Tanzania unasimamiwa na Sheria ya Uraia ya Tanzania, Sura ya 357, rejeo la mwaka 2002. Sheria hii inabainisha aina tatu za Uraia wa Tanzania ambazo ni Uraia wa Kuzaliwa, Uraia wa Kurithi na Uraia wa Tajnisi. Kwa mujibu wa Sheria hii, Serikali hairuhusu Uraia pacha kwa watu wazima isipokuwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kuandaa utaratibu wa kuwapatia hadhi maalum raia wa mataifa mengine wenye asili ya Tanzania ili kuwawezesha kuchangia maendeleo ya nchi yao ya asili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali la kwanza; je, kuna hasara gani Serikali kuruhusu uraia pacha kama zilivyo nchi zingine ambazo zinafaidika na raia walio nchi za nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Nchi jirani ya Kenya kupitia uraia pacha inaingiza fedha za kigeni dola bilioni 4.2. Tanzania kupitia mambo ya uraia tunaingiza dola milioni 520. Je, hatuoni kwamba tungeruhusu uraia pacha tungeongeza pato la nchi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha utaratibu wa kuwapa hadhi maalum raia wa mataifa mengine wenye asili ya Kitanzania. Kwa hiyo, hatuoni hasara, lakini hadhi hii itakapokamilika basi wananchi hao watachangia katika uchumi na pato la Taifa kama ambavyo nimejibu kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kwenye swali la pili, hadhi hii itakapokamilika wananchi hao watachangia kwenye maendeleo ya nchi yao kama nilivyosema. Kuchangia maendeleo ya nchi hii ni pamoja na kuchangia uchumi wa Taifa, kwa hiyo, Serikali inalifahamu jambo hili ni jambo muhimu. Tunashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, niliona umesimama.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. BALOZI. MBAROUK NASSOR. MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kueleza tu kwamba kutokuwa na uraia pacha hakujawa sababu kwamba ni kikwazo cha *remittance* au mafao kutoka kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Ushahidi ni kwamba *remittance* zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali tayari imeshaamua kutoa hadhi maalum na hapo baadaye miaka ya mbeleni huko, Serikali itaona kama kutakuwa na umuhimu wa kuwa na huo uraia pacha, kwa sasa hadhi maalum haijawa kikwazo kwa *remittance* na haijawa kikwazo kwa Watanzania wanaoishi nje kuwekeza nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Athuman Maige *remittance* kwa Kiswahili ni nini? Ngoja atusaidie ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge ziwe zinakaa kwa lugha…

Mheshimiwa Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, *remittance* ni toleo.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Nasikia toleo, nasikia miamala, tutafute neno hilo kwa Kiswahili ili Kiswahili chetu kikue, hatuwasikii hawa wa lugha nyingine wakichanganya lugha wakati wakizungumza.

Haya, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Kutolipwa kwa Madeni ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)***

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa kutolipwa kwa madeni ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kunaathiri ufanisi wa Mfuko huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abass, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* umeathiriwa na vitendo vya mtu mmoja au kikundi kuchelewa kurudisha mkopo kwa wakati hivyo kusababisha Mfuko kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, Wizara inaendelea kuratibu na kuimarisha huduma za Mfuko huo ili uendelee kuwafikia wanawake wengi zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Wizara ina mipango gani sasa wa kuyafuatilia marejesho hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni ipi mikakati ya kuuimarisha Mfuko huu ili uendelee kuwanufaisha wanawake wengi zaidi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, Wizara tumeteua Maafisa Maendeleo ya Jamii wakishirikiana na maafisa wa halmashauri zote Tanzania nzima kufuatilia marejesho ya mikopo hii ili kuwezesha wananchi wengine kufaidika zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali imeandaa mkakati wa kuanzisha mikopo kupitia taasisi za Serikali kwa lengo la uendelevu na zenye uhakika ili tuweze kuwafikia wanawake wengi zaidi. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM A. MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kuwakopesha wanawake ambao hawajanufaika na mkopo huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, Wizara ina mkakati wa kuongeza elimu na kuongeza mtaji kwa umma kwa kuhakikisha uwepo wa mikopo ili kuendeleza wanawake na wale ambao hawajapata mikopo hiyo, waweze kuipata kwa wakati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Uzalishaji wa Zao la Ngano – Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi wa Makete soko na bei ya uhakika ya zao la ngano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2023/2024 Wilaya ya Makete ilipata upendeleo wa kupewa mbegu za ngano tani 1,000 kupitia mpango wa ruzuku inayoratibiwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)*. Kutokana na upatikanaji wa mbegu, wakulima wameongeza uzalishaji hivyo kuwepo na changamoto ya soko la zao la ngano.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hiyo, Wizara ya Kilimo imeielekeza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*CPB*) kwenda Makete na kufanya tathmini ya ngano iliyopo ili kubaini kiasi cha ngano chenye ubora na kisha kuongea na wakulima kupitia vyama vyao kwa ajili ya kuinunua ngano hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE: FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali, hususan Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kusimamia kitabu cha bajeti kilichopita ambacho alituahidi kwamba watazuia watu kununua ngano nje, wanunue ngano ya ndani. Wiki iliyopita tumepokea mnunuzi wa ndani ambaye ni Bakhresa, amekuja kununua ngano tani 400 kwa kilo shilingi 1,000. Uzuri ni kwamba anakusanya yeye mwenyewe kwa gharama zake kwa maana ya kutoka kwa wakulima ili aweze kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu ni mawili. Swali la kwanza; kwenye jibu amesema Serikali imeleta tani 1,000, lakini sisi Makete tumepokea tani 476 tu; je, ni lini Serikali italeta tani 534 zilizosalia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tunajua Serikali ina mpango mkakati wa kujenga viwanda viwili kwa ajili ya mazao mchanganyiko hususan zao la ngano. Sisi wananchi wa Makete tuko tayari kutoa eneo ili muweze kujenga kiwanda. Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusu kujenga Kiwanda cha Ngano Makete ili zao hili liwe na tija kwa wakulima wa Makete ambao wameanza kuzalisha kwa wingi na Serikali iipe kipaumbele Makete kwa ajili ya uzalishaji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Serikali ni kupeleka tani 1,000 za ngano za ruzuku. Tumeshapaleka tani 476 bado 524. Kwa sababu msimu wa ngano bado unaendelea, sisi Wizara kupitia *ASA* tutaendelea kuzitoa mbegu hizo kwa kadri ya mahitaji ya wananchi katika Jimbo la Makete.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda ni kweli Wizara ina mpango wa kujenga viwanda viwili vya kuchakata ngano. Tunafanya tathmini katika maeneo yote yanayozalisha yakiwemo maeneo ya Makete. Tukishamaliza hiyo tathmini yetu maana yake tutajenga maeneo hayo. Ikiwemo kulipa kipaumbele Jimbo la

Makete ambako sasa hivi uzalishaji wa ngano ni mkubwa zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, simwoni nani anajibu swali la maji kwa hiyo nashindwa nikuruhusu au ni wewe mwenyewe unajibu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, yupo Naibu Waziri.

**SPIKA:** Au yupo Waziri wa Maji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, yupo Mheshimiwa Kundo.

**SPIKA:** Mbona hajahamia hapo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, amejisahau. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa inafuata Wizara ya Maji, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Tatizo la Maji Mkoa wa Dodoma**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, lini tatizo la maji katika Mkoa wa Dodoma litatafutiwa ufumbuzi wa kudumu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji, Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa Naibu Waziri wa Maji ambapo nimetumika kama Naibu Waziri wa Mawasiliano kwa miaka mitatu. Napenda kutumia fursa hii kushukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipatia kwa kipindi cha miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge kwa sababu katika kipindi cha miaka mitatu nimefika katika majimbo 203 kati ya majimbo 265. Nakushukuru wewe mwenyewe kwa kuendelea kutuongoza na kuendelea kusimamia miongozo ambayo inaenda kulinda maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua na kunipa imani nyingine ili niweze kutumika katika Wizara hii ambayo matamanio yake ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji, kwa vijijini 85% na kwa mijini 95%. Vilevile, tunatambua kwamba changamoto bado ipo, lakini Mheshimiwa Waziri tayari tumeshakubaliana huko tunaenda kuhakikisha kwamba maji yanatoka. Pale ambapo tutaona bomba halitoi maji tutalibadilisha, tukiona koki haitoi maji tutabadilisha koki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto kubwa ya huduma ya maji inayokabili Mkoa wa Dodoma. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ina mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kuboresha huduma ya maji katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mfupi Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi 79 ambapo miradi 15 ipo maeneo ya mijini na miradi 64 ni maeneo ya vijijini. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda wa kati, Serikali inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa bwawa la Farkwa

ambapo mkandarasi wa ujenzi wa bwawa hilo anatarajiwa kupatikana mwezi Septemba na ujenzi kuanza katika Mheshimiwa Spika 2024/2025. Aidha, kwa upande wa mpango wa muda mrefu, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kumwajiri mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria na kuja katika Mkoa wa Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu na kuna maeneo mengi ya Wilaya za Dodoma hakuna maji, natamani sana Serikali ituambie ni lini huo mchakato wa upembuzi utakamilika kwa sababu hili swali nimeliuliza zaidi ya mara moja. Kwa hiyo, nahitaji watu wa Dodoma wapate maji *especially* ninyi Wabunge na wananchi wote wa Dodoma. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri na kwa kuonyesha kwamba maji ni msingi wa uhai wa binadamu na injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tunatambua kwamba bwawa hili limekuwa na ucheleweshaji, lakini ni kwa sababu ya mabadiliko ya *scope* ya kazi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, bwawa hili lilifanyiwa usanifu au *study* mwaka 2015 wakati mahitaji ya Dodoma yalikuwa tofauti na sasa. Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali imeamua kuleta *consultant* ili kuhakikisha kwamba tunaangalia mahitaji ya sasa. Tayari Mheshimiwa Waziri alisaini mkataba mwaka 2022 ili kumpata *consultant* huyo na alishapatikana na anatarajiwa kukamilisha

kazi hiyo mwezi Septemba, 2024 na ujenzi utaanza mara moja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele kisha tutaendelea na ratiba yetu.

Wageni wanaoingizwa kule juu wasimame kidogo kwa sababu nimesimama, kwa hiyo, inabidi msimame msubirie nimalize. Tutaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii na matangazo mengine yatafuata.

Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 18 wa kwangu, ambao ni viongozi wa Kanisa la Waadventista Wasabato, Jimbo la Kati mwa Tanzania *(CTF),* karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Cosato David Chumi, ambaye ni mwanafunzi kutoka Chuo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim cha Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Kilwa Kaskazini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ambao ni marafiki na jirani zake hapa Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Kelvin Amos kutoka Kanisa la *Free Church Dodoma,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Edward Olelekaita, ambao ni wapiga kura wake kutoka Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Vwawa, Mbozi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 122 wa Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 100 na walimu nane kutoka *St. Florence Academy* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao hapa Bungeni, lakini ninayo matangazo mengine; tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge wote, ofisi imepokea sadaka ya mchele iliyotolewa na Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Mbarali, Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Siku akija hapa tutampigia haya makofi, lakini tunamshukuru sana kwa sababu, amekuwa na utaratibu huu tangu awe Mbunge mwenzetu na sasa pamoja na kwamba yuko nje ya Bunge, lakini bado anaendelea kutukumbuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed tunakushukuru sana kwa sadaka hii ambayo umeitoa kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kwa Watumishi wa Bunge. Tunakushukuru sana na Mwenyezi Mungu akujaalie baraka nyingi zaidi. *(Makofi)*

Aah! Niendelee na sala? Haya, ahsanteni sana. Kwa hiyo, utaratibu ni kwamba, kwa sababu mchele umeshafika, mtataarifiwa wapi mkauchukue ili kila Mheshimiwa Mbunge akachukue wa kwake na mtumishi akachukue wa kwake.

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo pia, kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi Bungeni humu. Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge Wote wa Chama Cha Mapinduzi anawatangazia kwamba, wakutane kwenye Ukumbi wa Msekwa, Saa 7.00 mchana, mara baada ya kusitisha Shughuli

za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wa CCM, Ukumbi wa Msekwa, Saa 7.00 mchana, mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau. Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Leo nitajikita kwenye sehemu moja tu ya masuala ya afya hapa nchini kwetu kwa sababu, nimeona tunalizungumzia sana hili suala hasa kwenye upande wa bima. Tunalipigia kelele sana Waheshimiwa Wabunge, lakini nimeona nisilipeleke kwenye Wizara ya Afya nilipeleke kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu, ni jambo ambalo ni la muhimu.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kutoa ushauri kwa upande wa bima kwa sababu, wananchi wetu maskini, hasa wa vijijini, wanahangaika sana na masuala ya bima. Niipongeze Wizara na dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kulihangaikia sana hili pamoja na Waheshimiwa Wabunge, lakini bado limekuwa na kizungumkuti kwenye yale maamuzi ya mwisho. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge bado hatuelewi kwamba hii bima itakuwa bei gani.

Mheshimiwa Spika, wengine tunajua shilingi 300,000 na kitu, kwa yale matibabu ya kawaida shilingi 60,000, lakini nataka kusema kama sisi wenyewe Watanzania hatutajionea huruma hili suala la bima litazidi kuumiza wananchi wetu wa vijijini kwa sababu, ukiangalia katika mipango ni kutaka kuchangisha wananchi. Utasikia mwananchi anatakiwa atoe bima shilingi 300,000, utasikia wananchi wanatakiwa watoe bima shilingi 60,000. Ukienda vyuoni labda wanatakiwa watoe shilingi 51,000 kwa wanachuo.

Mheshimiwa Spika, namna ya kupata hizi pesa inakuwa ni ngumu kwa sababu kama *CHF* ilianza shilingi 10,000 wananchi wa vijijini walishindwa kuchanga. *CHF* ilikawa shilingi 30,000, wananchi wa vijijini walishindwa kuchanga. Je, hicho kitakachokuja cha Bima ya Wote kitakuwa kiasi gani? Ukimwekea mwananchi leo, tena ameshindwa kuchanga shilingi 30,000, labda kwa mfano uje umwekee shilingi 60,000, ataimudu? Hicho ni kitu ambacho hakiwezekani kwa hiyo, tutakuwa tunapiga propaganda ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukiangalia wanufaika wa bima katika Watanzania 100 ni watu nane tu ambao wanalipa bima. Sasa ukiichukulia hii, hatuna chanzo maalum cha kupata pesa ambayo inaweza ikasaidia wananchi wa vijijini na watu maskini pamoja na wananchi wa mijini, hata mijini wapo maskini wengi tu tena zaidi ya hata hao wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndio maana nimeona ni lazima hili suala tulizungumzie bila uwoga. Najua kuna mawazo mengine tutatoa hapa kwenye mtandao watatukana, lakini acha watukane maana kuna watu wengine duniani hawapo, mbinguni nako hawajafika, wanaelea tu katikati. Sasa huwezi kuogopa kutoa mchango kwa sababu, mtu ata-*comment* vibaya. Atakaye-*comment* vibaya acha a-*comment* vibaya, lakini kwenye hii bima ya afya, ushauri ninaotoa, tupende tusipende ni lazima tuingize chanzo cha muhimu ambacho tutakipata kwa urahisi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii kwenye nchi yetu watumiaji wa simu, *line* za simu ziko milioni 72. Kwenye milioni 72 hata ukiweka shilingi 2,000 kwenye kila *line* moja ikatwe kwa mwezi, ambayo kwa mwaka kwenye ile *line* inakuwa ni shilingi 24,000, tutapata shilingi 1,720,000,000,000. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo tu, ukate shilingi 2,000 ambayo kwa mwaka mzima utakata shilingi 24,000, tutapata shilingi 1,720,000,000,000. Kwa hiyo, hapo kwanza tayari tutakuwa na chanzo cha uhakika. Tukiangalia kwa wale watumiaji wa simu wakubwa kama sisi Waheshimiwa Wabunge, wafanyabiashara, wafanyakazi, wao wataalam wa simu wanafahamu, wataelewa, wanaweza wakaongeza hata shilingi 10,000 kwa mwezi au hata shilingi 15,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukichukua hivi vyanzo vyote unaweza ukapata shilingi 2,000,000,000,000. Kwa hiyo, tayari unakuwa na chanzo cha kudumu cha kila mwaka kwa ajili ya hii bima ya afya. Kwa hiyo, wananchi wetu wa vijijini wasiwekewe *limit* ya matibabu kwamba, aah! Wewe utatoa hela hii shilingi 60,000, lakini tiba yako tu ni kuangaliwa hapo na dawa hazipatikani, haiwezekani! Yeye kama anaingia kwenye ile ya kusafisha damu, nilimsikia hapa Mheshimiwa Waziri wa Afya wakati anajibu kwenye maswali, hiyo bima iwe inafaa.

Mheshimiwa Spika, akiingia kwenye *T-Scan* iwe inafaa, akiingia kwenye *MRI*, iwe inafaa, kwa hiyo, matibabu yake yawe hayana kikomo. Tutafute tena na vyanzo vingine hata kwenye mazao; ukisema kwenye kila kilo tuchukue shilingi moja au shilingi mbili kwa sababu, yeye mkulima naye yuko huko. Kama mtu hana *line* ya simu ina maana huyo ni maskini wa kutupwa, huyo hafai kuchukuliwa hata shilingi 200, atatibiwa kutokana na mifumo hii. Kwa hiyo lazima tutafute vyanzo vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kupata vyanzo vya kutosha vya bima, sasa hiki kinachokuja najua wengi mtashangaa, lakini ndiyo ukweli. Hizi hospitali, zahanati za vijiji, sijui vituo vya afya, hivi lazima vifikie hatua vibinafsishwe, huo ndiyo ukweli, tuige habari ya *South Korea*, tusiwe wavivu. Nendeni

mkaangalie *South Korea* wanafanya nini? *Abu Dhabi* wanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, *South Korea* hakuna hospitali ya kijijini ambayo ni ya Serikali, hakuna kituo cha afya ambacho ni cha Serikali. Zahanati zote zimeingizwa kwenye mfumo mmoja, vituo vya afya vyote vipo kwenye mfumo mmoja, hospitali za wilaya zote, hospitali zote tuseme, kitu chochote kinachohusu huduma ya afya. Kuna jengo moja kubwa wamejenga pale, wako watu wa mambo ya *internet*, wako madaktari bingwa pale kwa hiyo, zahanati yoyote mtu akitibiwa ile ripoti yake inakwenda kule. Mtu mwenye zahanati siku akitaka kulipwa na bima, lazima wale wanakagua ile zahanati. Nilimtibu lini Mheshimiwa Njelu hapa?

Mheshimiwa Spika, Aah! Labda Mheshimiwa Njelu alikuja nimempiga *X-Ray,* lakini baadaye nikaona ugonjwa huo hauhusiani na *X-Ray,* nimempa *quinine* atibiwe malaria. Kwa hiyo, wanakata ile *X-Ray* kwamba, wewe mwenye zahanati ulikuwa tapeli, umetibu malaria, wanakulipa hela ya malaria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pakiwa na mfumo kama huo utakuta kwamba, watu waongo kwenye hizi zahanati na hospitali watakuwa hawapo na watu watachukua hizi zahanati wataziendesha. Ukiangalia leo hii zahanati moja inatakiwa watumishi 13, madaktari wawepo wasiopungua watatu, manesi wasiopungua wanne, pawepo na watu wa maabara. Zahanati zetu za Tanzania mpaka sasa hivi tunashindana na ukuta, huo ndiyo ukweli wala tusidanganyane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakwenda unakuta daktari mmoja na nesi mmoja na anafunga kama duka la kwake. Ikifika saa 8.00 anaweza akafunga akaondoka, ikifika jioni huduma hakuna, wakati tuna manesi wamesoma, tuna madaktari wamesoma. Wakijiunga sisi kazi yetu Serikali siyo kwenda kujenga tu, kila siku tunapeleka vifaa, unapeleka leo darubini, keshokutwa imepasuka. Ukitembea zahanati zote, ukitembea vituo vya afya vyote unakuta mashine ya *blood picture* imenunuliwa mwaka jana, mwaka huu imeshakufa, imefunikwa kwa sababu hakuna mzalendo ambaye analinda vile vitu, lakini tuwape taasisi za dini,

tuwape wale madaktari ambao wamekosa ajira na manesi, wachukue, wazikodishe kwa Serikali, watumie bima.

Mheshimiwa Spika, leo hii tubakize tu hospitali za rufaa, kama hii ya Muhimbili na sehemu zingine. Leo hii ukisema ufunge bima ya afya kwa hospitali binafsi ina maana hospitali zote za binafsi zimekufa kwa sababu, kazi yao ni utapeli wa kula hela za wananchi. Sasa ina maana katika 100 wako watu nane wenye bima, lakini katika hao watu nane wenye bima ndiyo wanaoendesha hospitali zote za binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijaribu ifunge tu, waseme sasa hivi bima hii itumike kwenye hospitali za Serikali peke yake kama wataona hizi hospitali za binafsi zitakuwepo. Zote zitakufa *automatic,* lakini nawashangaa wataalam kufikiria wamekuwa wavivu au wanafikiria tu sehemu yenye *deal* ya kupiga pesa? Lazima kwenye afya tusilete mambo ya mipango mingi. Hata dada yangu hapa wa afya lazima nimsifu, wakati ule alipoamua kupanga bei za matibabu.

Mheshimiwa Spika, ukienda Muhimbili, mama mjamzito wa kujifungua kwa *operation* nafikiri ni shilingi 500,000, ukienda katika hospitali binafsi ni shilingi 3,000,000 na ni lazima pale alazwe. Akilazwa, akija kutoka ni shilingi 7,000,000 mpaka shilingi 8,000,000. Daktari huyo huyo anayetibu hospitali binafsi saa nyingine ndiye anayetibu hospitali ya Serikali. Sasa na kule ameshaambiwa kabisa na bosi wake ee bwana ee, ukienda kule hospitali yako ya Serikali hebu tuletee huku wateja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mtu akienda kwenye hospitali ya Serikali, anakuta daktari ni yuleyule, lakini anamwambia hapa vifaa hatuna. Yeye mwenyewe tena anaiporomosha ile hospitali anayofanya kazi, anasema hapa hatuna vifaa, njoo hospitali fulani nitakutibu. Yote hiyo ni kutafuta, anajua nikienda kule huyu akija atapigwa shilingi 3,000,000 ya *operation*, pamoja na kodi na mimi nitapata *percent* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa tunashindana na ukuta kama hatuna mikakati mizuri, kama imeshindikana, basi tujue tu,

hospitali za Serikali ziboreshwe vizuri, bima itumike kwenye hospitali za Serikali isitumike kwenye hospitali za watu binafsi, muone kama hospitali za binafsi keshokutwa zitakuwepo zile. Mtakuta zote hazipo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa bado nataka kuendelea…

**SPIKA:** Dakika moja, malizia.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kutoa ushauri kwa Bunge lako, tuangalie jamani, wananchi wanatupa tabu, watu wanasema tu Waheshimiwa Wabunge wana mishahara mikubwa, lakini ukifikiria hela zote zinaishia kwa wananchi. Nachukua mfano, kwa wewe dada yangu hapo, Mheshimiwa Spika, nikiangalia hela unazotumia kwenye jimbo, huwa nakuonea huruma na siku ukija kutoka kwenye Ubunge, wewe lazima tu utavaa kandambili moja nyekundu moja ya kijani, utakuwa umeshachanganyikiwa. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kwanza inabidi huo unabii niukatae. Kwanza inabidi niukatae maana kuna Wachungaji humu ndani wasije wakasema sasa Mheshimiwa, lakini hoja yako nadhani imeeleweka. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, anafuata Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema ambayo ametupa na leo tuko hapa. Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali nzima akiwepo Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote walioko Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanajaribu kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naenda kwenye mchango wangu. Tumesikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu

ambayo imeelezea mambo mengi sana ambayo Serikali ya Awamu ya Sita inajaribu kufanya. Kwa kweli yako mambo mengi mazuri sana, lakini leo nataka kuchangia kuhusu barabara.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tulisema kwamba, tutajenga kilometa karibu 8,506 hivi za lami na ule mpango wa barabara za *EPC+F* ambao kwa kweli, ilikuwa ni barabara karibu saba na kilometa 2,035. Ziko barabara ambazo ni muhimu zinaunganisha mikoa na zinafungua nchi yetu kiuchumi. Tulifanya mkutano mkubwa sana na wananchi walikuja kushuhudia, tumesaini mikataba tarehe 16 Juni, 2023 na sasa wanachotaka wananchi ni barabara hizi zijengwe, lakini je, lini zitajengwa?

Mheshimiwa Spika, hizi barabara zinapita kwenye mikoa mingi sana ambayo ni muhimu kwa uzalishaji wa nchi yetu. Tunachoomba, Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali itafute pesa haraka hizi barabara zijengwe. Barabara ya kutoka Kongwa – Kiteto – Simanjiro – Arusha ni barabara inayounganisha karibu mikoa mitatu. Barabara kutoka Tanga – Kiteto – Chemba mpaka Singida ni barabara inayounganisha mikoa minne. Kwa hivyo, ni barabara ambazo ni muhimu sana. Hizi barabara zote za *EPC* tuishukuru Serikali kwa kuja na mpango huu. Sisi matarajio yetu ni kwamba, mpango huu wa *EPC* utatujengea barabara hizi kwa haraka sana. Wananchi wa Kiteto leo wanataka kusikia majibu au anapokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu, atuambie hizi barabara zinaanza kujengwa lini?

Mheshimiwa Spika, pili, Sekta ya Kilimo, sekta ya uzalishaji hususani awamu wa pili ya A*SDP II* tumeona kwamba Serikali ina mpango wa kuleta mbegu, lakini zifike kwa wakulima kwa wakati. Ina mpango wa kuleta mbolea, tunaomba zifike kwa wakati, lakini ambacho hakiko *clear* sana ni mpango wa Serikali kutafuta matrekta ya bei nafuu ambayo ni ya muda mrefu. Mkopo uwe ni wa muda mrefu na uwe ni rafiki kwa wakulima, tukifanya hivi tutawaondoa wakulima kwenye kulima kwa jembe la mkono na tija itaongezeka kwenye kilimo. Wananchi wangu wa Kiteto kwa kweli wanalisubiri sana hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matrekta haya sasa yawe mazuri siyo kama yale matrekta ya *URSUS* ambayo yametuletea hasara kubwa sana. Kwa hivyo, tutaomba baadaye Waziri Mkuu atuambie wana mpango gani wa kuleta matrekta kwa ajili ya kukopesha wananchi? Matrekta yawe ya muda mrefu na yawe mazuri ili wananchi wapate kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Umwagiliaji; nchi yetu tunategemea mvua lakini tuna ardhi nzuri sana, tungewekeza kwenye umwagiliaji zaidi maana yake wananchi wetu watakwenda kulima kila wakati na tuna *plan* hapa na tumesema mpaka 2030 sijui tuwe tumefikia 50% ya umwagiliaji. Sasa tunatamani sana hii miradi ambayo tuliipitisha mwaka jana ya umwagiliaji ianze kazi sasa ili wananchi waweze kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu *BBT; BBT* kwa kilimo na mifugo ni mpango mzuri sana na kwa kuwa tumeanza na *experiment*, tutatarajia itoe matunda mazuri sana. Kwa sababu ni *experiment* nashauri tutengeneze *BBT* nyingine tofauti kidogo ambayo itajaribu kuwakwamua wale wananchi ambao ni vijana na akinamama ambao tayari wako mashambani. Wapo vijana wako Kiteto, kwa miaka mitano, kumi hadi ishirini wamekuwa wanafanya kazi za kilimo, wapo akinamama wanachotaka ni kuwezeshwa. Kwa hivyo, ili tuendane na hii *BBT* tunayoendelea nayo ambayo naamini ni kitu kizuri sana, tutengeneze nyingine sasa ili tuwe na *comparison*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka mkulima kijana anayetajwa Kiteto kwamba anapata *support* hii awe ni kijana ambaye anafahamika na Wanakiteto kwamba ni mkulima na mama ambaye anaonekana yupo shambani kila wakati. Hii *system* ya kutafuta kwa njia za *interviews* na *internet* na tunataka kufanya kilimo eti kiwe *sexy,* ndiyo watu wakananii wakati tayari kuna watu wanafuga na tayari kuna watu wanalima, naomba sasa tuwe *practical*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati; kwa kweli mipango ya Serikali ni mingi sana na tunataka vijiji vyote vipate umeme, lakini bado kuna maeneo mengi umeme haujafika na tulitarajia sana

kama tulivyosema ifike kama ni Juni au Desemba mwaka huu tufunge mjadala wa umeme angalau kufika kwenye vijiji. Kwenye hili tulizungumza hapa Bungeni tukasema tuna miji midogo ambayo kisheria ni miji midogo, lakini kiuhalisia ni sura za vijiji. Wakatuambia hapa kwamba kuna Tume Maalum inazunguka nchi nzima kujaribu kuangalia ile miji midogo midogo ambayo kiuhalisia ni vijiji ili na wao waanze kupata huduma ya umeme kwa shilingi 27,000 ya vijijini. Sasa hii iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka majibu, Kiteto, Matui, Kibaya kuna vijiji ambavyo ni vijiji kiuhalisia na ukizingatia tena mwaka huu tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wapo Wenyeviti ambao ni wa miji lakini kiuhalisia bado miji ile haina faida za miji midogo. Kwa hivyo, kama tutaona kwamba, bado *plan* ya kufanya ile miji midogo ipate huduma zinazostahili, basi tuite vijiji kwa sasa ili na wao waendelee kuitwa Wenyeviti wa Vijiji ili wasipitwe na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na tumetoa mapendekezo mengi sana. Tunaomba Serikali ifuatilie maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo hayo kwa Mafungu yote.

Mheshimiwa Spika, pili kuna miradi ya mkakati kama bomba la mafuta inapita Kiteto karibu kwa kilometa 117. Kila wakati tulifikiri miradi hii ingeleta fursa za ajira, za kibiashara kwa wananchi ambao wanapitiwa na miradi hii, lakini mifumo ya kuwaambia wasajili kwenye mitandao haitaweza kutupa wananchi wa Kiteto fursa hizi. Ni vyema Serikali ikajaribu kuweka mkakati kwamba, ni lazima wananchi wanaopitiwa na hii miradi mikubwa wanufaike nayo. Ningetamani sana kesho kujua madereva wangapi wa Kiteto wameajiriwa. Akinamama wangapi wanauza chakula na wangapi wameajiriwa kwenye nafasi ambazo hiyo elimu iko Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari ya kuanza kusema tu-*compete* na sisi tu-*apply* kwenye mitandao, mwananchi wa Kiteto ataweza ku-*compete* namna gani? Kwa hivyo ni lazima kuwepo na *an affirmative action* ya kuonesha kabisa kuwa, kuna watu

wanaotokana na vijiji ambao wananufaika na fursa hizi, ambao kimsingi ni wale wasioweza ku-*compete* kwa njia za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika moja malizia.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, alaa! Basi nimalizie kwa kusema hivi, Fungu 65 tunajua Ofisi hii inayoshughulika na Ajira kama tunavyofahamu haitoi ajira, lakini kazi yake ni kutoa miongozo ili tupime tija na ubunifu na tunajua Serikali inajaribu kufanya mambo fulani Fulani, lakini tunachotaka sasa ni kujua kwamba, Serikali ina mkakati gani wa kufanya miongozo na sera hii itekelezeke kwa haraka ili tuweze kupima tija na ubunifu katika eneo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya na kwa sababu ya *interest* ya muda, niwaombee Timu ya Wananchi ya Yanga leo ushindi mkubwa sana na kwamba Watanzania wengi wana imani na timu ya Yanga. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, nilikuwa natafakari hapa si mlisema kuna uzalendo? Mbona unaiombea timu moja na nimeambiwa zinacheza timu mbili? *(Kicheko)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naogopa muda lakini naweza sasa kusema, nawatakia Timu ya Yanga na Simba ushindi mkubwa sana na walete ushindi huu nyumbani. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Said Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga na Mheshimiwa Angeline Sylvester Mabula ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi

wa rehema aliyetujalia kupata afya njema na kuwepo hapa. Pili, nami niipongeze Timu yetu ya *Tembo Warriors* ambayo ni timu machachari, timu ambayo imetuletea heshima kwa sababu iliweza kuingia mpaka *World Cup* na inakwenda katika mpira wa Afrika ambao utafanyika Misri. Wewe kama mdau na Mheshimiwa Waziri Mkuu ningependa sana twende tukawaone vijana wetu wale, tukawatie nguvu ili ushindi uweze kupatikana. Penye mpira siyo Yanga peke yake, hivyo hata watu wenye ulemavu wanaweza. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwa haraka kutokana na muda na nitazungumzia suala la vijana. Katika Takwimu za Tanzania asilimia 50 ni vijana, hii ni nguvu kazi ambayo inabidi tupambane nayo na tuweze kuisaidia ili tuweze kupeleka uchumi mbele. Kama vijana hawa hawatakuwa na ajira ya kutosha au hawatawezeshwa, ina maana tunatengeneza kundi la vijana maskini katika nchi yetu. Katika bajeti ya mwaka jana tuliidhinisha Fungu namba 65 bilioni moja kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Mpaka leo tunazungumza hapa ni mwezi wa tatu, Wizara haijapewa hizo pesa, lakini ni mwaka wa tano huu sasa pesa za vijana kwa ajili ya maendeleo yao haziingii katika Wizara pamoja na kuwa tumeidhinisha humu ndani, lakini Wizara haipati chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, bilioni moja hazikuingia lakini kuna pesa za *SDL (Skills Development Levy)* kila mfanyakazi anakatwa asilimia nne na katika asilimia nne tumekusanya bilioni 291 na katika bilioni 291 asilimia moja ya tatu zinakwenda kwa ajili ya Mfuko wa Vijana. Leo ninavyozungumza hazijaenda na hela hizi hazina mjadala kwa vile zilishakatwa na zimeshakusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji bilioni 97 ambazo zitakwenda Wizara ya Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu ili kusaidia vijana kujiwezesha. Fungu hilo hilo tena kuna fedha za kukopeshana vijana ambazo ni kutokana na Sheria ya Mwaka 1963 ilikuwa tumepanga kabisa kuwa tuwe na Fungu maalum kuwasaidia vijana kwa ajili ya kukopeshana. Leo ninavyozungumza mpaka sasa hivi hakuna fedha ambazo zimekwenda kule na tayari tuna

vijana 681,000 ambao inabidi wapatiwe fungu lao ili waweze kujiendesha. Kama hatujaweza kuwapatia hilo fungu ina maana hatuko tayari kuwasaidia vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumza hivyo? Nazungumza hivyo kwa sababu Wajumbe wa Kamati tulikwenda katika maeneo mbalimbali, tulikwenda Butimba na vyuo mbalimbali vya *VETA*, tumekuta vijana wanafanya kazi, vijana wabunifu. Tumekwenda Butimba tumemkuta kijana mbunifu anajua ku-*detect* mahali gani kuna madini, iwe dhahabu au vito. Tatizo unamsomesha yule mtoto lakini akitoka pale hana hata nyenzo ya kutoka nayo. Tulivyokwenda tumewakuta vijana wengi wana ubunifu mkubwa, lakini akimaliza kozi yake hata kile kifaa kuondoka nacho hawezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tujifunze kwa wenzetu kama vile China, India na Uturuki kwa nini wamefanikiwa? Walifanikiwa kwa ajili ya kusimama na vijana, lakini kama tutaona hizi fedha za vijana hazina umuhimu, basi kwa kweli tutatengeneza panya *road* wengi katika Tanzania hii. Tunatengeneza vijana ambao wanamaliza vyuo vikuu lakini hawatakuwa na ajira wala hawatakuwa na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais, aliliona sana suala la Barabara za Liwale. Liwale kwa kweli katika wilaya ambayo iko katika hali ngumu ukilinganisha na zingine ni Liwale, kwa vile hii kwanza ni barabara ya kimkakati ya mkoa lakini barabara hii haipitiki. Mheshimiwa Rais, alitoa helikopta na kumwambia Waziri aende kule na Waziri alienda Liwale kujionea hali ilivyo pamoja na maeneo mengine yote. Tumwombe Mwenyezi Mungu ajalie katika kipindi hiki tuweze kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tutayarekebishaje hayo maeneo? Kuna nguzo kumi za uchumi, hizi nguzo ni lazima zisimamiwe na kama hatujazisimamia, basi ina maana hata watu wanaoomba barabara, maji, wanaotaka vituo vya afya, vitu hivi vitakuwa havina msingi.

Mheshimiwa Spika, sasa nitaizungumzia bandari *(TPA); TPA* ni taasisi kubwa na imeingia ubia wa uwekezaji na *DP World,* lakini kama *TPA* haijapewa nafasi kubwa ya kujiendesha, hivyo, itakuwa ina kazi kubwa ya kujiboresha na kuleta uchumi wa ziada. Tunategemea *TPA* ikiwezeshwa na kupewa fungu la kutosha, Serikali itapata mapato makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi Mamlaka ya Bandari *(TPA)* ina bandari ndogo ndogo 86. Katika Bahari ya Hindi peke yake ina bandari 22 ikiwemo Lindi, Kilwa, Pangani, Mkuranga, Kisiju na Mafia, zote hizo ziko chini ya Pwani ya Bahari ya Hindi. Vilevile, kuna Bandari za Ziwa Tanganyika ziko 22, Bandari za Ziwa Nyasa ziko 12 na za *Lake Victoria* ziko 29, lakini je, bandari hizi zitajiendeshaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari itafanyaje kazi kama Serikali haijaiwezesha kiuchumi kwa sababu makusanyo yote yanakwenda Mfuko Mkuu na yakienda katika Mfuko Mkuu inabidi ipewe fedha kidogo kwa ajili ya kujiendesha. Sasa huyu ni ng'ombe, ng'ombe ili aweze kutoa maziwa ni lazima apate chakula. Kama Serikali haijaiwezesha Mamlaka ya Bandari ikasimama kwa kutopata fedha za kutosha, ina maana tunaipeleka bandari kwenye kuanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa tahadhari humu ndani na kwa wote wanaonisikiliza humu ndani, Waziri wa Fedha ni msikivu, tusimame kwa pamoja, Wabunge tuisimamie Bandari ya Tanzania isije ikaanguka kwa kupewa majukumu makubwa lakini haina uwezo na wanatamani wapate uwezo. Uwezo ninaouzungumzia ni wa kuifanya bandari ile iweze kuleta pato zaidi kwa ajili ya Serikali Kuu na iweze kutoa gawio kwa Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nitalizungumzia ni viwanda na biashara. Viwanda vidogo vidogo ndiyo viliwasaidia vijana kuweza kuendelea kiuchumi na siyo vijana hata na wanawake na wenye ulemavu wana uwezo mkubwa. Tulikutana na ubunifu mkubwa wa vijana katika upande huu wa viwanda, lakini hawana uwezo. Sasa kama vijana hawa katika *small scale*

*industry* hawajaendelezwa, tusitegemee mabadiliko makubwa ya kiuchumi ambayo ndiyo yanaweza kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano hai, leo kuna ubanguaji wa korosho unaofanywa na vijana, lakini kama hawana mashine za kubangulia korosho hawa vijana watafanyaje? Tunataka kuondoa umaskini kwa vijana wa mikoa ambayo inalima korosho, lakini kama hawana vifaa, mashine za kufanyia kazi ina maana tunatengeneza umaskini mkubwa. Si hivyo tu, maeneo mbalimbali yanahitaji mabadiliko makubwa ya kiuchumi. Sasa tusimame kwa pamoja tujiulize ni maeneo gani ambayo Tanzania inabidi tusimame nayo na tuyape kipaumbele. Bila kuyapatia kipaumbele ina maana tutajikuta bado tunatafuta hela za kujenga barabara, lakini je, tunataka kujenga barabara hela ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, leo ukiangalia barabara zote zimekufa. Naizungumzia Lindi kwenda Mtwara ni kisiwa Daraja kubwa la Mbwemkuru limeshaanguka tayari, hivyo watu wa Lindi wanashindwa kuja Dar es Salaam, inabidi wapite Ruvuma. Sasa bila kutafuta vyanzo vya mapato makubwa ina maana nchi hii itakuwa haiendelei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu Bandari ya Lindi ambayo imekufa kwa muda mrefu. Hiyo bandari ilikuwa ni bora kabisa kwa kuwa Lindi tunapakana na Comoro, mzigo wa Comoro unatoka Dar es Salaam, kwa nini tusisimame na Comoro wakakaa? Tuna Balozi mzuri ambaye yuko Comoro, anasema kama atapewa bandari za Lindi na Mtwara, zikatumika kwa ajili ya mizigo ya Comoro, nchi hii itaweza kuinuka kiuchumi na tutahakikisha Mji wa Lindi ambao umedorora kiuchumi hata kwa ajira utaweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naitakia kheri nchi yangu, naiomba kwa uchungu Serikali itoe pesa ipeleke Bandari na *TANAPA*, hawa watu wawezeshwe ili nchi iweze kujikwamua kiuchumi. Kila anayesimama anaomba Barabara, kama hakuna mtaji mbadala au hakuna *source of income* kwa kupitia taasisi mbalimbali, itakuwa tunapiga kelele ambazo hazina umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumtakie kheri Mheshimiwa Rais, anapambana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika moja…

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, lakini na wale watendaji ambao wanajiona hawataki kufanya kazi na Mheshimiwa Rais, watupishe. Mheshimiwa Rais, anataka kufanya kazi na watu ambao wana utayari wa kufanya kazi na yeye…

**SPIKA:** Mheshimiwa Lulida…

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Mheshimiwa Lulida, dakika moja malizia.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba wote mnaochangia humu ndani muangalie watu wenye ulemavu, ulemavu ni utarajiwa. Sasa tukiangalia katika kila mkoa kuna walemavu, je, watu wenye ulemavu ambao wako katika maeneo yako unawasaidiaje? Wenye ulemavu ambao wanakaa wanahitaji msaada mkubwa sana, wanakuja mpaka milangoni. Je, wewe kama Mbunge, mwakilishi wa jimbo au wilaya unawasaidiaje watu hawa kwa sababu watu wenye ulemavu sasa hivi wameonesha uwezo mkubwa, wanafanya kazi kubwa na ni wazalishaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Angeline Mabula na Mheshimiwa Priscus Tarimo, ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwenye

bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana ametusomea bajeti yake ambayo imejaa matumaini makubwa, inaleta neema na inaonesha kabisa kwamba tunakwenda kwenye nchi iliyo bora zaidi ya hapa ilipo. Pia nisisahau kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jenista, Waziri mpambanaji, Waziri mwanamke ambaye kwa kweli hajatuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza ripoti hii, bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonesha mafanikio mengi katika sekta mbalimbali. Naomba kusema kwamba, bila Mheshimiwa Rais kusimama imara, tusingefika hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kule Shinyanga, kiwango cha pesa ambacho kimekuja hakielezeki, haijawahi kutokea tangu uhuru umepatikana. Katika sekta ya afya, shilingi bilioni 32.6 zimekuja, haijawahi kutokea. Katika sekta ya elimu, shilingi bilioni 37.2 zimekuja, haijawahi kutokea. Katika sekta ya maji ndiyo usiseme, shilingi bilioni 52.2. Akinamama wa maeneo ya vijijini kule ambao walikuwa wanapata shida, wanateseka kwenda kufuata huduma kwenye maeneo ya mbali, sasa hivi huduma nyingi zimesogezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na nampongeza kwa sababu aliingia madarakani kipindi ambacho kilikuwa ni kigumu. Dunia na nchi nyingi zilikuwa zipo kwenye kitu kinaitwa *exogeneous shock*. *Exogenous shock* ni matatizo au majanga ambayo yanalipata Taifa wakati wewe mwenyewe huna uwezo wa kuzuia na wala huna maamuzi kwa majanga hayo. Matatizo kama *COVID*, Vita ya Ukraine ni matatizo ambayo yalisababisha athari kubwa kwenye nchi nyingi duniani, bila Mheshimiwa Rais wetu kipenzi kusimama kwa uwezo wake aliomjaalia Mungu, tusingefika hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba nizungumzie suala moja ambalo jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alilizungumzia kwenye hotuba yake. Mheshimiwa Rais tunamsifia kwenye maeneo mengi sana, kwenye sekta za elimu, afya na

kadhalika, lakini naomba kwa nafasi ya kipekee na kwa kipekee sana nimpomngeze sana Mheshimiwa Rais kwenye mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Kwa nini nasema hivyo? Kiwango cha madawa ya kulevya ambacho kimekamatwa tangu yeye aingie madarakani mpaka leo, haijawahi kutokea kwenye Serikali yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kwamba mapambano ya biashara hii ni mapambano makubwa na yanatisha sana, lakini katika kipindi cha Januari mpaka Desemba, mwaka mmoja tu wa 2023, kiwango cha madawa ya kulevya kilichokamatwa ni kilo 1,365,340. Kiwango hiki ni kikubwa sana ukilinganisha na kiwango cha madawa ya kulevya kilichokamatwa kwa miaka 11. Mwaka 2011 – 2022 kiwango cha madawa ya kulevya kilo zilizokamatwa zilikuwa ni kilo 660,465. Sasa yote haya ni juhudi za kipekee ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madawa haya yangeingia sokoni, athari kubwa sana zingetokea kwa vijana wetu, wote tunafahamu kwamba, vijana ni nguvu kazi, hakuna kitu kinauma kama una mtoto, umemzaa vizuri, unamsomesha, katika familia nyingi watu wengi huwa wanajua kwamba ukiwa na mtoto basi na wewe unategemea aje kukulea, lakini matokeo yake watoto wengi wamekwenda kuumia kwenye madawa ya kulevya. Vijana wetu, nguvu kazi, wasomi, wamekwenda kutumbukia kwenye matumizi ya madawa ya kulevya. Hawa wanaoingiza madawa ya kulevya ni akina nani? Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliamua kuchukua juhudi za makusudi akaamua kuimarisha upande wa Mahakama, hivi sasa kesi za madawa ya kulevya hazicheleweshwi kama miaka ya zamani. Pia ameimarisha sana Maabara Kuu ya Taifa. Miaka ya zamani wote tunajua, ilikuwa mtu anakamatwa na madawa ya kulevya, baadaye baada ya siku mbili anaambiwa huu ulikuwa ni unga wa ngano, ilikuwa ni aibu sana. Baada ya Mheshimiwa Rais kuingia madarakani kwa kweli tunaona juhudi ambazo zimefanyika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, maamuzi yake kwenye kuchagua watu, nasema na namuunga mkono Mheshimiwa Rais, acha aendelee, hata akikuweka leo, kesho ukitoka sawa, kwa sababu wewe kama umeonesha kuna baadhi ya vitu havijakaa sawasawa, toka tu kesho aje mwingine, ni sawa naunga mkono hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kuitengeneza na kuiunda hii Tume na Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya. Wapo watu walikuwepo, wamefanya kazi yao wamemaliza kutokea hapo mpaka walipofikia, kazi hii inataka uzalendo wa kiwango cha juu sana. Kazi hii inataka uwe mzalendo tu na siyo mzalendo wa mdomoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pesa ilimuua hata Yesu kwa Wakristo, wote tunajua kuwa biashara hii kubwa ni biashara yenye pesa nyingi sana, pale ambapo watu wanakaa, wafanyabiashara wakubwa, wenye akili zao timamu, wenye pesa zao nyingi wanakaa, wafanyabiashara 10, wanasema tunajiunga tupate bilioni 100 kwa kuagiza madawa ya kulevya kama mtu anavyoagiza nguo, tujue kwamba ni biashara ambayo ni kubwa sana. Biashara hii kwa utaratibu huo ni biashara ambayo ina rushwa kubwa sana. Nimpongeze Mtendaji Mkuu, Kamishna wa Mamlaka hii ya Madawa ya Kulevya Ndugu Aretus Lyimo kwa kazi kubwa na ya kizalendo ambayo amekuwa akifanya yeye na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu juzi juzi hapa kuna kiwango kikubwa sana cha madawa ya kulevya kilikamatwa, ingawa jana kuna mdogo wangu mmoja nimemsahau ni nani alikuwa anachangia, akasema kwamba Serikali hii inakamata sana lakini haiweki nguvu kwenye matibabu. Nimemsahau ni nani. Naomba tu nimkumbushe na nimweleze, tena alifika mbali zaidi akasema kwamba, miaka ya zamani tulikuwa tunashuhudia baadhi ya waraibu walikuwa wanafikia mpaka kiwango cha kulipiwa kodi za nyumba za miezi sita. Naomba tu nimshauri Mheshimiwa Jenista hata kama nchi yetu itakuwa na uwezo wa kiwango gani isije ikafikia kiwango cha

kutaka kutoa pesa kwa ajili ya kulipia kodi waraibu na najua kwamba haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapambano haya ni makubwa sana, tunapokaa na kuona kwamba nchi iko salama, Rais wetu anapambana, ndiyo mambo yanakwenda. Vijana wa miaka ya zamani wote walikuwa wanakaa kule Kinondoni, unamwona kijana anapiga debe, Posta, Kariakoo udenda unamtoka, mwingine analala chini na kadhalika. Tukiona mambo hayo yamepungua sasa hivi Tanzania, tumshukuru Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazazi wengi, mjomba wangu anakaa pale Kinondoni Mtaa wa Ufipa, huwa nikienda kule Kinondoni nakaa naulizia, hivi fulani yupo? Hapana, fulani alikuwa anasoma, lakini bahati mbaya ameingia kwenye matumizi ya madawa ya kulevya, sasa hivi ameharibika. Unashangaa na inauma kwamba vijana ambao walikuwa wapo *bright,* ni tegemeo, lakini leo hii ameenda kuishia kwenye njia ambazo hazieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii kupitia Rais wetu kipenzi Mama Samia amepambana sana, licha ya kwamba baadhi ya nchi nyingine mitazamo inatofautiana kwenye kuwahudumia hawa waraibu. Inatofautiana kwa sababu wapo watu wengine ambao wanasema hawa ni matatizo ya kujitakia na hawafanyi chochote, lakini Mheshimiwa Rais wetu anatoa pesa nyingi sana. Kilo moja ya kuwahudumia hawa watumiaji wa madawa ya kulevya ni Dola 750. Dola 750 watahudumiwa waraibu kadhaa, lakini vituo vilivyopo mpaka sasa hivi, kuna vituo 16 ambavyo vinatoa huduma ya kuwapa madawa hawa waraibu. Vile vile *sober houses,* mpaka sasa hivi nchi yetu ina *sober houses* 52 ambazo zina waraibu zaidi ya 4,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi ambazo zinachukuliwa na Mheshimiwa Rais wetu...

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Taarifa mimi sipendi *aah! (Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tarimba Abbas.

**TAARIFA**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Mayenga kwa mchango mzuri sana na hasa anapolinganisha juhudi za Mheshimiwa Rais katika kuangalia waraibu.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Jenista alikuja na Kamati ya Mheshimiwa Mhagama pale Kinondoni katika kituo ambacho Mheshimiwa Rais anakilea na kuhakikisha kwamba waraibu wanapata huduma, hivyo anachokizungumza ni jambo la kweli sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa za hivi ndiyo ziwe zinakuja, ahsante sana, taarifa naipokea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia kwa sababu kengele imegonga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nizungumzie kuhusu suala la dola. Kwa kifupi naomba nipongeze *BOT* kwa kuongeza riba kutoka asilimia 5.5 mpaka kufikia asilimia sita. Hii itasaidia kupunguza *inflation,* lakini naomba kusisitiza kwamba, wafanyabiashara wengi wanalalamika kuhusu tatizo la dola.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa niseme kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara yuko wapi? Azungumze na wafanyabiashara. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Angeline Sylvester Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa ambayo amenijalia leo na kuniwezesha kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anafanya kazi yake vizuri na hasa katika ile miradi ya kimkakati. Bajeti hii imebeba mambo mengi sitaweza kuyasema yote, lakini nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais katika ile miradi ya kimkakati ambayo hakuna hata mradi mmoja ambao umesimama na yote inakwenda vizuri. Nampongeza sana kwa sababu utekelezaji kwa 100% kwa miradi ile ndiyo utakaofungua uchumi kwa Watanzania, lakini utasaidia pia katika suala zima la maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza sana Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake bila kumsahau Seneta Jenista Mhagama, ni Waziri ambaye amekuwa akifanya kazi zake vizuri pamoja na wale waandamizi walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite katika masuala machache, nianze katika Mradi wa Kufua Umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mradi ule unakwenda vizuri na mpaka sasa tunapoongea tayari mtambo namba 9 umeshafanya kazi na umeshaingiza umeme katika gridi ya Taifa kwa megawati 235. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuunganisha katika suala hilo ni kwamba, tuwe na *multiply effect* katika suala zima la matumizi ya bwawa lile. Kwa sehemu ya juu kuna maeneo ambayo tunaweza tukawa na kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kizuri na kuweza kulinda yale maji yaliyokuwa pale yasipotee bure pia kuweza kufanya kazi ya kilimo ambacho kingeweza kutumika. Nawaomba wenzetu wa Wizara ya Kilimo katika yale maeneo ya juu ambayo siyo hatarishi, basi waweze kuwa na kilimo cha umwagiliaji ili wananchi waweze kulima kwa mwaka mzima na kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la uboreshaji viwanja vya ndege. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais anaendelea kuboresha viwanja vya ndege kikiwepo Kiwanja cha Msalato. Hata hivyo, nizungumzie Kiwanja cha Mwanza ambacho ni juzi tu wamesaini mkataba wa kuboresha Jengo la Abiria, naomba sana mkataba ule utimizwe ili tuweze kufanya kazi vizuri. Uwanja ule ukiboreshwa, tutafungua wigo na maeneo mengine ya utalii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kutoka Mwanza kwenda Serengeti ni kilomita zisizopungua 200 lakini kutoka *KIA* kwenda Serengeti ni kilomita 380. Maana yake ni kwamba, tukifungua uwanja ule, tayari tutakuwa tumeongeza idadi ya watalii ambao wanaongezeka nchini kila mwaka, kwa hiyo, naomba sana hilo lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, tunapoboresha viwanja vya ndege, tuangalie hapa ni Makao Makuu, lakini Wabunge tunapata changamoto kubwa kutoka hapa kwenda Mwanza, Arusha, Mbeya, naomba sana tunapoboresha viwanja, basi tuone namna ya kuboresha usafiri kwa Watanzania ambao wengi wanakuja Makao Makuu hapa, tuwapunguzie adha ya kuzunguka Dar es Salaam ndiyo waje Dodoma. Tuanzishe usafiri wa kutoka Dodoma kwenda Mwanza, Dodoma kwenda *KIA*, Arusha, Mbeya na maeneo mengine ambayo yameboreshwa ili kurahisisha pia namna ya utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la uvuvi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amewakumbuka wavuvi wa Kanda ya Ziwa na hasa kwa Maziwa Makuu mpaka kwenda *Lake* Nyasa na mengine kule. Ameweza kutoa vitendea kazi vya kutosha kabisa na kuwawezesha kwa kuwapa mikopo. Changamoto iliyopo katika suala zima la watu walioko kwenye sekta ya uvuvi, ni changamoto wanayoipata hususani Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania inamiliki ziwa zaidi ya asilimia 51, lakini kwa sasa wale wavuvi hasa wanaotoka Kanda ile, wanasafirisha mazao yao kupitia nchi za jirani kutokana na ushuru ambao umeongezwa kutoka shilingi 10 kwa kilo mpaka shilingi

100, suala ambalo Waziri husika anafahamu. Changamoto hii imefanya pia mapato ya Taifa yapotee, lakini masoko yaliyojengwa kwa ajili ya kuhudumia hayafanyi kazi sasa kwa sababu wanatorosha mazao wanaenda kuuzia nchi jirani ambako ushuru wake uko chini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri husika atakapokuwa anazungumza kwenye bajeti yake aliangalie hili kwa sababu limekuwa ni changamoto. Haiwezekani mtu anakuja kutoka Congo, Zambia na nchi za jirani anafuata samaki hapa, wanakwenda moja kwa moja visiwani, wananunua huko na hawapiti kwenye masoko. Kuna pesa nyingi inapotea hapo. Niombe sana usimamizi huo uboreshwe kwa sababu tunapoteza mapato mengi kwa njia ya watu kutorosha na kutofuata taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia suala la *loyalty* ni changamoto kubwa, Tanzania bei yetu ni kubwa ukilinganisha na Kenya pamoja na Uganda. Naomba pia hili liangaliwe kwa sababu ushuru huo unapotea kwa wavuvi kupeleka upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, lingine, naomba nizungumzie mwenendo wa mapato na makusanyo. Niipongeze sana Serikali katika makusanyo, kwa sehemu kubwa ukiangalia mapato yanayotokana na Serikali za Mitaa wamekusanya kwa asilimia 95, mapato yanayotokana na *TRA* yamekusanywa kwa asilimia 97, mapato yanayotokana na mawakala na taasisi mbalimbali wamekusanya kwa asilimia 78. Sasa kama mapato ni makubwa kiasi hiki, naomba sana katika zile sekta ambazo ni sekta wezeshi kwa mfano, ukiangalia TAMISEMI hasa upande wa *TARURA,* bajeti zake zinavyokwenda, haziendi sambamba na uhitaji katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, mapato yetu tulivyokusanya yamevuka malengo, lakini ukija kuangalia kwenye matumizi pesa inakwenda kidogo kiasi kwamba namna ya kuunganisha miundombinu yetu ya barabara hasa katika vijiji ambako ndipo kuna wazalishaji, bado ni changamoto. Naomba sana kwa sababu ukusanyaji mapato upo vizuri, basi tuangalie namna bora ya kuziwezesha

sekta ambazo ni za usafirishaji ambazo pia zinasaidia katika suala la kupunguza adha upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la utawala. Katika suala la utawala tumefanya sensa mwaka 2022 na ukiangalia maeneo mengi ongezeko la watu ni kubwa. Kwa *average* ya ongezeko kwa mwaka baada ya sensa ni 2.3% ambayo inaongezeka kwa watu, lakini ukiangalia Wilaya kama Nyamagana na Ilemela zina watu zaidi ya 500,000. Katika maeneo ya utawala zina Tarafa moja moja. *DC* hana tofauti na Afisa Tarafa, ukiangalia baadhi ya kata zina watu 45,000 ni sawasawa na wilaya katika mikoa fulani, nisingependa kuitaja.

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie namna ya kusogeza huduma kwa wananchi hawa ili waweze kupata huduma vizuri. Hivyo, ni lazima kuongeza maeneo ya utawala pamoja na changamoto ambayo Serikali inayo katika kuongeza, lakini tuangalie hivi Wilaya moja yenye watu zaidi ya 500,000 kuwe na Tarafa moja, kata ina watu zaidi ya 45,000 au zaidi ya 30,000 halafu haina tarafa ya kuunganisha. Maombi yapo katika Ofisi za Serikali, basi tuone namna bora ya kuongeza maeneo hayo ili kusogeza huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala zima la mawasiliano na teknolojia. Hivi karibuni tu Waziri alizungumzia suala zima la kufanya *registration* kwa watu, kuweza kuangalia matapeli ambao wamekuwa wakizungusha sana watu. Tulisema katika suala zima la teknolojia, tunapotumia mitandao ni ajira pia kwa wenzetu katika uchumi wa kidijitali, lakini mtandao huu umekuwa ukitumika vibaya. Kuna matapeli wengi pamoja na kufanya usajili upya kwa Watanzania wote, lakini ongezeko la matapeli limekuwa ni kubwa mno, wanatumia namba za watu, wanatumia majina ya watu kutapeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara inayohusika, hili suala limekuwa kubwa nami ni mmojawapo naomba ku-*declare interest,* nimekuwa ni muhanga mkubwa sana katika suala hili. Wapo na wengine ambao wanapata shida hii. Niombe sana katika hili, Serikali iangalie pamoja na kufanya *registration* upya,

lakini tuone namna bora kama Taifa tunasema tunakwenda kwenye uchumi wa kidijitali, lakini uchumi huo unakuwa siyo mzuri kwa watu wengine kutokana na suala la utapeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaongelea suala la usalama wa nchi, sasa usalama wa nchi unakuwaje kama kuna watu wanaweza waka-*temper* na mawasiliano ya watu na wakafanya mambo ambayo siyo mazuri. Kwa hiyo, niombe sana hilo nalo liangaliwe kwa sababu ni suala ambalo linakwenda kukinzana zaidi na lengo la Serikali ambalo ni zuri, lakini matokeo yake linakuwa siyo sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Sekta ya Madini; sekta hii uwekezaji wake ni mkubwa na niipongeze Wizara husika imekuwa ikifanya kazi nzuri sana na hasa kwa kuwajali wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapa mitaji, elimu na mambo mengine. Sasa ningeomba na kuishauri Wizara, tunapozungumzia suala la kutwaa maeneo na kuwapa wenye leseni tuangalie pia suala la kumwezesha mwenye ardhi yake, siyo lazima aondolewe pale, anaweza pia akawa ni sehemu ya umiliki wa leseni ile ambayo mwekezaji amekuja kuwekeza. Hata kama atapata asilimia mbili, lakini atakuwa na uhakika wa kuendelea na maisha mazuri kwa kutumia ardhi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusijikite katika kuwaondoa wananchi na kuwapa kipaumbele wawekezaji, bali tuone namna bora ya kumshirikisha huyu mwenye ardhi yake, akawa sehemu ya mmiliki wa ile migodi na yeye aka-*enjoy*. Hata kama atapata asilimia ndogo, lakini bado ataendelea ku-*enjoy* katika maisha yake. Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa sana katika suala la miundombinu ikiwemo pamoja na uchimbaji. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara inayohusika, tusiangalie tu kuwaondoa hawa watu, pia tuangalie namna bora ya kuwawezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa namna ambavyo *Royal Tour* ambayo Mheshimiwa Rais wetu alikuwa ndiyo *sterling* ambapo ameweza kuifungua nchi na kuweza pia kuongeza mapato na watalii kwa kiasi kikubwa. Niombe sana katika masuala mazima ya utalii tuangalie pande

zote katika nchi yetu, kila mahali kuna vivutio vya kutosha sana, ukiangalia Kusini, ukiangalia Kanda ya Ziwa na maeneo mengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

**MHE. DKT. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia suala zima la kuongeza maeneo ya utalii ili kuweza kuunga mkono lile suala zima la *Royal Tour* ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya na limeonekana lina tija kubwa. Niiombe Wizara inayohusika iangalie pia kanda nyingine ambazo pia, kuna vivutio vya kutosha ili angalau tuweze kupanua wigo na watalii hao waweze kufika katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza sana kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye kwa kweli anachapa kazi na kila mara tunamwona yupo katika maeneo mbalimbali ambapo ameweza kugundua mambo mengi ambayo hayakufanyika vizuri na kuyarekebisha. Kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wanafanya kazi ofisini kwake. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Mawaziri wake ni vijana wachapa kazi, kwa kweli wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru au nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anasimamia Serikali yake na namna ambavyo kwa kweli anahangaika usiku na mchana

kuhakikisha maendeleo yanapatikana katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa ku-*site* kurasa mbalimbali ambazo zina mambo ambayo ni muhimu tuyaangazie. Nikianza na ukurasa wa 50 wa hotuba ya Waziri Mkuu, umeongelea viwanja vya ndege mbalimbali ambavyo vinajengwa na viko kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Kiwanja cha Moshi ambacho kimepata fedha kama shilingi bilioni 12 kwenye bajeti kwa ajili ya kukirekebisha. Niishukuru sana Serikali kwa hatua hiyo. Nilete ombi mahususi ambalo Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ameshaleta barua kwa utaratibu wa kiserikali. Ili kiwanja kile kiwe na tija sawasawa, inahitajika kuwaondoa watu kaya kama sita pale ili kiwe na urefu unaotakiwa. Katika hizo kaya, kaya tatu zina hati, kwa maana wako rasmi eneo lile na wana-*qualify* kupata fidia, lakini kuna kaya tatu ambazo hawakuwa rasmi kwa hiyo, hawa-*qualify* kupata fidia.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyofanyika kwenye Uwanja wa *KIA,* naomba Serikali ione namna tu ya kuwafuta machozi hata wale ambao hawana hati ili zile kaya sita zinazotakiwa kupisha upanuzi ule basi ziweze kupata chochote ili upanuzi wetu ulete tija na tuweze kupata ndege kubwa katika uwanja wa Moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kurasa za 14, 28 na 21; katika ukurasa wa 14 ameongelea Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi, lakini ukurasa wa 28 ameongelea upatikanaji wa sukari au uzalishaji wa sukari na ukurasa wa 21 ameongelea uwekezaji. Naomba nilete mawazo au ushauri mahsusi; Serikali ni vizuri iondokane kabisa na uendeshaji wa shughuli zote za kibiashara, kwa sababu haiwezi. Urasimu ulioko kwenye Serikali hauruhusu kufanya shughuli ambazo zina sura ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, hiki Kiwanda cha Mkulazi nafikiri hatua zianze za namna ya kutafuta mwekezaji ambaye atakiendesha kwa ubia na Serikali, yaani hili nilitolee mfano kwa kiwanda

ambacho kiko kwenye Wizara hii hii, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, cha *Kilimanjaro International Leather Industry Limited.* Serikali imeshawekeza zaidi ya bilioni 120, lakini uendeshaji wake hau-*match* kabisa na uwekezaji uliowekezwa.

Mheshimiwa Spika, bilioni hizo kwa miaka ambayo zimeshawekezwa, kiwanda ambacho kilitakiwa kiajiri watu 3,000 mpaka 10,000, leo kimeajiri watu 250. Kina mashine za kisasa kabisa za duniani, hata ukienda Italia, ukienda Spain, viwanda vinavyotengeneza ngozi vina mashine kama hizi, lakini Serikali tunaendesha kwa kuchukua *pair* 10, 20, zinakuja kuoneshwa hapa Bungeni, tunasubiri maonesho, hakutakuwa na tija milele kwenye kiwanda kwa uendeshaji wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tutafute wawekezaji iwe kwenye kile Kiwanda cha Ngozi cha Moshi, kiwanda hiki cha sukari ili tija ipatikane, ajira zipatikane, kodi ipatikane na Serikali ipate mapato, vinginevyo tutasubiri wakati vinakufa tutoe kwa dharura kama tulivyoitoa hii *DART*. Kwa hiyo ushauri wangu, tufanye mapema hii ili vikikamilika tukabidhi kwa kuuza *share* au kwa namna nyingine yoyote ya kutafuta ubia wa uendeshaji ili vilete tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mapambano dhidi ya dawa za kulevya niipongeze sana Serikali kwa ujumla na niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu. Kama alivyotoa takwimu msemaji aliyepita kwamba kwa historia tumekamata dawa nyingi zaidi. Mimi nijielekeze kwenye tiba ile hasa ya kutumia *methadone*. Kwa mfano, Moshi Mjini wale waraibu wanahitajika kwenda Arusha kila siku ili wapate ile huduma ya *methadone*. Nishukuru, nilimletea Naibu Waziri na wameshaanza kulifanyia kazi. Hospitali ya Mawenzi imeonekana hakuna nafasi, lakini pale Moshi Mjini tunayo maeneo mengi ambayo huduma hii inaweza ikapatikana ili tupunguze huu uraibu. Kupunguza uraibu kwa kutumia hizi dawa ni kupunguza soko la wanaoleta hii bidhaa tayari. Kwa hiyo, tukiweza kuleta hizi huduma karibu na wananchi na pale Moshi kama tunavyohitaji, watatusaidia sana. Hili nimeona limeongelewa vizuri kwenye ukurasa wa 90.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ukurasa wa 44 wa hotuba ya Waziri Mkuu, eneo la ardhi. Hata mzungumzaji aliyetoka ameongelea maeneo ya utawala; hili lote linaungana na hili suala la ardhi. Sisi Moshi Mjini tulishaleta maombi, tulishapitisha michakato yote ya kuipanua Halmashauri ile kutoka kilometa za mraba 58 kwenda kwenye 142. Tumeshamaliza ngazi zote, lakini ilisimamishwa baada ya watu kuonesha kwamba kuna hatua nyingine za kufuata.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu matatizo ambayo yapo, kwa sasa hatuna eneo la kuweka kiwanda. kwa sasa Moshi Mjini hatuna eneo la makaburi na yaliyopo yamejaa. Eneo la dampo tumenunua Moshi Vijijini, kilometa takriban 20 kutoka pale mjini, lakini adha kubwa sio tu kwamba, liko mbali bali pia barabara ile hatuwezi kuirekebisha na fedha za *TARURA* kwa sababu kwenye mtandao wa *TARURA* wa Moshi Mjini, barabara ya kwenda kwenye eneo la dampo haipo kwenye mtandao wetu. Kwa hiyo barabara ile inabidi tutafute wafadhili na hivyo inaendelea kuwa mbovu na hatuwezi kuihudumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana maombi ya muda mrefu ya Moshi kuwa Jiji na kupanuka mipaka yake kutoka kilometa za mraba 58 kwenda 142 yachukuliwe kwa uharaka wake kutokana na umuhimu wa utoaji wa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile mikopo ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu kila mtu ameiongelea. Ilikuwa ni kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ilikuwa ni kauli thabiti ya kuokoa upotevu wa hela ya Serikali, lakini muda umeshakwenda sana, sasa ni mwaka fedha zile hazijaanza kurejeshwa. Wasiwasi wangu, watu hawapati ile mikopo, hiyo ni adha ya kwanza, lakini ya pili, kule kwenye halmashauri ziko salama, hazijabadilishiwa matumizi zikaenda katika maeneo mengine? Naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu iharakishe suala hili kwa sababu ni mwaka sasa na mikopo hii haitolewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye eneo la huduma za usafirishaji. Moshi Mjini tulianza mchakato wa kutengeneza Stendi

ya Ngangamfumuni, stendi ya Mkoa. Serikali ilipeleka bilioni saba, lakini kuna matatizo yaliyotokea, kuna matatizo yaliyokuwa ndani ya halmashauri na kuna matatizo ya nje. Tulisharekebisha karibu matatizo yote yaliyokuwepo pale na Kamati mbalimbali, nyingine za Bunge na nyingine zinazotoka Serikalini zimekuja na zimeona hatua tuliyopiga. Maombi yangu, tuukwamue sasa mchakato ule kwa sababu tayari zimeshawekwa zaidi ya bilioni saba kutoka Serikali Kuu na milioni 800 kutokana na mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuchelewesha ukamilishaji ule fedha ile inaendelea kupotea pale na kile ni chanzo cha mapato cha halmashauri, lakini tunashindwa kupata fedha kutoka kwenye mradi ule. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe alifika pale akatoa na maagizo; naomba arudi atusaidie kuwa na timu ya kukwamua mchakato ule ili stendi ile ianze kazi. Tumeshafanya kazi kubwa kwa maana ya halmashauri. Tumeondoa ule ujenzi wa hoteli pale, tumeona hauna tija kwa sasa. Tunaomba watusaidie tukamilishe ili mabasi yapite na chanzo cha mapato kianze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie eneo la mfumuko wa bei pamoja na tatizo la dola ambalo lipo na wengi wanafahamu, hii iko kwenye ukurasa wa 19 wa hotuba. Sasa hivi kuna shida ya dola kwenye nchi yetu na ni shida kubwa sana ambayo ina tu-*cost,* lakini kibaya zaidi tunapoteza pia mapato. Uhalisia wa watu wanaobadilisha hela sasahivi wamerudi kwenye *black market* ambako wanabadilisha kati ya shilingi 2,800 mpaka wakati mwingine shilingi 3,000. Sasa kwa sababu sisi tumeng'ang'ania ile *rate* ya benki, lakini benki wanashindwa kupata hizo dola kwa sababu watu wanajua kuna *black market*.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue hatua madhubuti za haraka za kunusuru hali hii ya upotevu wa dola ambao ndio utakaosababisha mfumuko wa bei, kwa sababu tunadhani vitu vimeagizwa kwa gharama ya 2,600/= lakini watu wameagiza kwa 2,800/=, hivyo vikija sokoni bei yake itakuwa kubwa na mfumuko wa bei utakuwa juu. Serikali ni vizuri ichukulie suala hili kwa dharura, ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba niseme naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Conchester Rwamlaza ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa ningependa kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ametekeleza falsafa za *4R,* kwa maana ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi Upya.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu safari hii Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetenga fedha zote kwa ajili ya kuendesha uchaguzi wetu. Jambo ambalo ni la kihistoria na litasababisha kwenda kulinda maslahi mapana ya Taifa letu katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusaini zile sheria ambazo Bunge lako Tukufu tulizipitisha, zinazosimamia masuala ya uchaguzi pamoja na vyama vya siasa. Hapa hapa nimpongeze sana *mentor* wangu, dada yetu mkubwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi kubwa aliyofanya kuratibu zoezi hili kuanzia majadiliano ndani ya vyama vya siasa hadi mchakato mzima wa kupitishwa sheria hizi na mpaka sasa zimesainiwa. Aidha, katika eneo hili la uchaguzi ningependa kuishauri Serikali mambo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ili kulinda nyaraka zetu za uchaguzi ni vyema Serikali iweke mkakati thabiti wa kuhakikisha kwamba Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ndiye atakayechapa nyaraka zote zitakazohusu uchaguzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ili Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali aweze kutekeleza jukumu la kuchapa nyaraka za uchaguzi ipo mashine ambayo Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali anahitaji. Hivyo ningependa kuishauri Serikali iweke jitihada za makusudi kabisa kuhakikisha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali anapata mashine hiyo ili aweze kutekeleza majukumu haya, hata pale ambapo Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itaamua kuchapa nyaraka zote za uchaguzi huko, basi wataweza kufanya hivyo. Hii ni kwa sababu mwaka huu tunakwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa na ni muhimu kujihakikishia ulinzi na usalama wa nyaraka zetu za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho katika eneo hili la uchaguzi ni kwamba, kwa kuwa sasa hivi Sheria ya Vyama vya Siasa imeshasainiwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na sheria hii inaelekeza vyama vya siasa vianzishe madawati ya jinsia, basi nitumie fursa hii kuiomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikahakikishe kwamba vyama vya siasa sasa vinakwenda kuanzisha madawati haya ya kijinsia pamoja na kuweka muda kwamba mpaka ifikapo muda fulani madawati haya yawe yanafanya kazi. Hii ni muhimu sana kwa kuzingatia tunakwenda kwenye michakato ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni eneo zima la *TASAF*. Napenda kuipongeza sana Serikali chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kufanyika ya kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini *(TASAF)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo inafanyika napenda kuishauri Serikali kwamba, iweke jitihada za makusudi kabisa za kufanya tathmini ya kuhakikisha kwamba kaya ambazo zimesajiliwa kunufaika na mpango wa *TASAF* iwe ni kaya ambazo zinastahili kunufaika, lakini vivyo hivyo zile kaya ambazo bado hazijasajiliwa basi mpango wa haraka ufanyike ili ziweze kusajiliwa. Nasema hivi kwa sababu pale kwenye Wilaya yetu ya Bukoba Mjini, tuna takribani kaya 5,000 ambazo

zinapaswa ziwekwe kwenye mpango wa *TASAF,* lakini mpaka hivi sasa ni kaya 3,081 ambazo zimesajiliwa na tayari zinanufaika na mpango huu wa *TASAF*. Hivyo tuna kaya 1,919 ambazo bado hazijaingizwa kwenye utaratibu huu wa kunufaika na *TASAF* na 62% kati ya hizo ni kaya ambazo hazikusajiliwa katika awamu zote zilizopita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili tuendane na kasi na maono ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuinua kaya hizi maskini, niiombe sana Serikali, utakapofika wakati wa kufanya mchakato huu wa kupitia na kuhuisha na kusajili hizi kaya maskini basi pale Bukoba Mjini hizi kaya zetu 1,919 ziweze kuangaliwa kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naendelea kuipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu ikiongozwa na yeye mwenyewe Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, dada yangu, *mentor* wangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na Naibu Mawaziri na ofisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya ya kuratibu masuala ya Serikali, lakini ya kuratibu masuala yote ambayo yanahusiana na haya maeneo tuliyochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natarajia kutokana na jitihada kubwa iliyowekwa na bajeti zilizopitishwa watahakikisha kwamba ile bajeti ambayo imetengwa kwa ajili ya elimu kwa umma kwenye masuala ya uchaguzi, basi itatumika pia kuhakikisha inatolewa hamasa kwa wanawake ili waweze kujitokeza kwa wingi kugombea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, halikadhalika na Uchaguzi Mkuu mwakani. Pia iweze kutoa shime kwa vijana na wanawake waweze kujitokeza kwa wingi kupiga kura ili watumie haki yao ya Kikatiba ya kuchagua viongozi wao, viongozi bora na bila ya kusahau Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa fursa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchester Rwamlaza na Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika mchango wangu nitajikita kwenye mambo machache, jambo la kwanza litakuwa ni kwenye sekta ya nishati, lakini nitajikita pia kwenye suala la barabara kwa maana ya *TARURA* na *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, nikianza kwenye suala la barabara, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha wazi nia thabiti ya Serikali ya kuchagiza upatikanaji wa miundombinu imara ya barabara nchini, lakini nizungumze jambo moja tu. Mwaka 2022 Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya kikao na watu wa *TARURA* nchini. Kati ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yalikuwa ni watu wa *TARURA* kubadilisha mchakato wa manunuzi, hususan kwenye mikoa na kwenye wilaya ambazo zina upatikanaji wa mvua nyingi, hasa kwenye maeneo kama Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Makete, Ludewa, Wanging'ombe na majimbo mengine yote ambayo yana changamoto ya mvua.

Mheshimiwa Spika, licha ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini hadi sasa kumekuwa na changamoto kwa sababu tenda nyingi zimekuwa zikitangazwa majira ambayo ni ya mvua, mathalani Makete. Nazungumza muda huu si tu kwa sababu ya mvua ambayo inaendelea kunyesha, lakini barabara zimetangazwa majira ambayo si sahihi, kiasi kwamba fedha ambazo zinatolewa na Serikali zinakosa kuleta tija kwenye ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Makete ambayo ni miongoni mwa wilaya zenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo, wilaya hii ninavyozungumza leo tuna Barabara kama za kutoka Lupila kuelekea Kipengele, kutoka Matamba kuelekea Chimala na kutoka Ikuwo kuelekea Nkenja, barabara hizi zimefungwa si tu kwa sababu ya mvua ni kwa sababu pia zimekosa ujenzi imara, lakini pia kutokana na bajeti kidogo.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kuwe na uwiano, unakuta jimbo X na jimbo X kijiografia yanaendana, lakini utofauti wa kibajeti kwenye *TARURA* umekuwa ni mkubwa sana. Unakuta jimbo hili bajeti ni ndogo lakini ukiangalia *population structure* yake iko juu. Niiombe Serikali angalau kuwepo na uwiano kwenye haya majimbo ambayo yanapatikana kwenye maeneo kadha wa kadha nchini ikiwemo Makete na Majimbo ya Mkoa wa Njombe, kwani tumekuwa na changamoto ya utofauti wa kibajeti, kitu ambacho hata wananchi wanaona kwamba, barabara za jimbo fulani zinaboreshwa zaidi kuliko barabara za jimbo fulani. Hili jambo limekuwa likituletea msuguano wa kisiasa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye maelekezo yake kwa sababu yeye ndiye Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, tungeomba uwiano wa kibajeti kwenye majimbo haya ambayo kwa kweli ni ya kiuzalishaji na yanaisaidia sana Serikali kwenye sekta ya mazao.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la upatikanaji wa umeme nchini kwa maana ya nishati, kati ya jambo ambalo Watanzania wanaotusikiliza huwa wanapata wakati mgumu pale ambapo umeme unakuwa haupatikani na sababu zinakuwa ni *valid*, sababu zinakuwa ni *valid* kabisa. Niiombe Serikali kitu kimoja, upatikanaji wa nishati ya umeme na usambazaji wa nishati ya umeme nchini umekuwa ni mkubwa, kwa maana ya kwamba tumesambaza sana umeme kwenye vijiji, kwenye vitongoji na tumeita wawekezaji kadha wa kadha nchini kuja kuwekeza, kwa maana kwamba, matumizi ya umeme nchini yamekuwa ni makubwa sana. Naona sasa kuna haja ya Serikali kuongeza vyanzo vya uzalishaji wa umeme nchini na upatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuukamilisha Mradi wa Mwalimu Nyerere na tayari mitambo imeanza kuwashwa, kiasi kwamba imepunguza kukatikakatika kwa umeme nchini. Naiomba Serikali, tuna Mradi kama wa Bwawa la Lumakalya ambalo linapatikana Wilaya ya Makete, ni mradi namba mbili kwa ukubwa nchini baada ya Mradi wa

Bwawa la Mwalimu Nyerere. Wananchi wale wako tayari kupisha mradi na tayari tathmini imefanyika, naiomba Serikali ipeleke fedha kwa wakati ili wananchi wale wapishe na mradi uweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumza kitu kwenye nishati ya umeme na upatikanaji wake nchini. *TANESCO* kama shirika la uzalishaji umeme wakati linaanzishwa *population* ya nchi haikuwa kama tuliyonayo leo ya watu milioni 61, watu walikuwa ni wachache na umeme ulikuwa hautumiki kwa wingi kwa kiwango hiki. Sasa, kwa sababu katika Shirika la *TANESCO* kuna masuala matatu, kuna suala la *generation,* kwa maana ya uzalishaji na ufuaji wa umeme; kuna suala la *transmission,* kwa maana ya usambazaji wa umeme; na kuna suala la *distribution* kwa maana ya kupeleka umeme kwenye makazi, naishauri Serikali, sasa ni muda muafaka wa kuipunguzia mzigo *TANESCO,* kwa maana gani? Kwa maana kwamba, naomba tuwe na idara au taasisi inayohusika na uzalishaji au kufua tu umeme nchini; tuwe na taasisi nchini inayohusika na usambazaji peke yake, kwa maana ya hizi gridi za Taifa; na tuwe na taasisi ambazo zinahusika na usambazaji wa umeme kwenye makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumza hivyo? Nazungumza hivyo kwa sababu katika *population* ya watu milioni 61, *manpower* ya *TANESCO* ni ndogo, mara nyingi ukienda Ofisi za *TANESCO* zinapatikana Makao Makuu ya Wilaya, changamoto ya umeme imetokea kata *X*, hadi mtu kutoka Makao Makuu ya Wilaya kwenda kutatua tatizo imekuwa ikichukua muda mrefu huko vijijini. Pili, mathalani tumeanzisha taasisi kama *REA*, taasisi kama *REA* imesaidia kwenye usambazaji wa umeme vijijini, lakini wananchi wanapata changamoto moja, *REA* anasafirisha umeme anaufikisha kwenye kijiji, baada ya hapo anaondoka anamwachia mtu anaitwa *TANESCO*. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa Serikali kuipunguzia mzigo *TANESCO* kwa kuwa na watu wa *transmission*, wa *generation* na wa *distribution,* kwa maana ya kwamba watu wanaosambaza umeme katika maeneo tofauti.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya pili?

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, malizia dakika moja.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia hapo kwenye umeme ili kuhakikisha kwamba nishati hii inapatikana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni jambo moja, mimi ni mdau wa michezo, naipongeza Serikali kesho wanaenda kusaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa uwanja pale Arusha, lakini naomba, maandalizi ya viwanja yaendane na maandalizi ya Timu ya Taifa kuelekea *AFCON* 2027 kwa sababu tusije kuandaa viwanja, lakini tukashindwa kuandaa Timu ya Taifa. Mwisho wa siku tukapata aibu kwenye nchi yetu, kitu ambacho siyo kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, naitakia kila la heri *Simba Sports Club,* leo wanacheza, niitakie kila la heri *Dar Young Africans*, *solidarity forever*! Tuzitakie timu zetu ushindi huko ziliko na tuendele kuziombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ng'azi Ulenge na Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache kuhusu hoja iliyo mezani ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mipango tunaiweka katika fedha lakini tunalenga katika kuleta maendeleo ya watu, maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii. Napenda kwanza kuongelea kuhusu barabara na nitakwenda mojamoja katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba inayojulikana hasa hasa kama Bukoba Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tupate uhuru tumekuwa tukilia ndani ya Bunge hili. Napenda kuiuliza Serikali, ni kwa nini vilio

vyetu tunavyolia hapa wameviweka pembeni? Halmashauri ya Bukoba inapakana na Manispaa ya Bukoba, inapakana na Muleba Kusini, inapaka na Karagwe, inapakana na Misenyi, yaani sisi tuko katikati, lakini kwa muda mrefu hatuna barabara yoyote ambayo inatutoa ili tuweze kwenda katika majimbo hayo. Sasa ni miaka karibu 60 ya uhuru hatujawahi kufikiriwa kupata barabara ya lami na sisi tunachangia katika Uchumi. Tumelia kuhusu Madaraja ya Kalebe, tumelia kuhusu Vivuko vya Nyabasa na Kansinda, tumesema sana ndani ya Bunge hili kwamba jamani sisi tumekosa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika kwenye kampeni kule Bukoba Vijijini, alisafiri mpaka kule Bubare, barabara aliyopitia mwaka 2020 ndiyo hiyo hiyo ambayo atapitia mwaka 2025 kwenda kupiga kampeni, hakuna mabadiliko yoyote. Kwa hiyo, ajifunge kibwebwe kwamba atakapokwenda kupiga kampeni katika Jimbo la Bukoba Vijijini, ajue barabara ni hizo hizo walizopitia mwaka 2020, ndiyo hizo hizo watapita kwenda kupiga kampeni mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niongee kuhusu elimu, mimi sina ubishi kwamba miundombinu ya elimu haijatengenezwa katika nchi yetu. Shule zimejengwa na ni nzuri. zinameremeta kama maua huko, mimi nitaongea kuhusu *dropouts* ambazo zinatokea katika shule ambazo tumejenga. Ukienda katika Ripoti ya *CAG* ya Mwaka wa Fedha 2019/2020, 2020/2021 na 2021/2022, ameongelea sana kuhusu *dropouts* za wanafunzi. Watoto hawamalizi darasa la saba, watoto hawamalizi *secondary school* hasa *form four*. Hizi *dropouts* ziko katika mikoa ya pembezoni, ukienda Kigoma, Songwe na maeneo mengine ya pembezoni ziko *dropouts*, nina wasiwasi, inawezekana Serikali hawasomi taarifa ya *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wangekuwa wamesoma wakaona jambo hili linalotunyemelea, lingekuwa limeanza kuchukuliwa hatua. Nchi haiwezi kuwekeza kwa kiwango kikubwa na kwa pesa kubwa katika elimu halafu unakuwa na watoto ambao hawamalizi shule. Tunachotegemea huko mbele baada ya miaka 10 ni *disaster*, sisi tumeenda na hata juzi tumezunguka, tumeona

shule za sekondari za wasichana nzuri tu zimejengwa, pesa zimetolewa hilo halina ubishi, lakini tujiulize, je, hawa watoto wanaokwenda kusoma wanamaliza? Tunachotegemea ni nini kama watoto hawamalizi pamoja na kujenga majengo mazuri? Pamoja na kuweka hela yote hiyo tunalenga nini? Tunataka watoto wamalize ili tufute ujinga na tusirudi kule tulikotoka. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa wafuatilie taarifa ya CAG waone ni kwa kiwango gani na ni kwa *percentage* gani watoto hawa hawamalizi shule ili tuone kama kweli malengo yetu yatatimizwa kwamba, watoto watasoma watamaliza na tutafuta ujinga katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea kuhusu madeni ya Magereza. Tumekuwa tukipigania Magereza kulipwa pesa zao za madeni. Hawa wana madeni wanayodai Serikalini kama ilivyo kwa Askari Polisi, Uhamiaji na hata Jeshi, lakini hawa wamekuwa hawalipwi. Mwezi Februari, Serikali ilipita kuhakiki madeni, wamehakiki madeni lakini mpaka sasa hivi hawa Askari Magereza hawajalipwa. Hawa Askari Magereza wanalazimika wakati mwingine kutoa hela yao mfukoni kusafirisha wafungwa, yaani anasafirishwa mfungwa kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine kwa pesa ya Askari Magereza halafu hawawalipi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuendelee kuwasemea lakini Serikali ichukue hatua. Wawaone hawa Askari Magereza kama askari wengine, wanafanya kazi kubwa ya kulinda wafungwa, wanateseka nao. Mvua ikinyesha inamnyeshea Askari Magereza na mfungwa ananyeshewa, umeona? Kwa hiyo, wanafanya kazi kubwa ya kulinda hawa watu na pia kuwapa mafunzo. Serikali iwalipe madeni yao au stahiki zao ili nao wahakikishe kwamba sasa wanafurahia kazi zao wanazozifanya, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwa wazee; siwezi kuacha kusemea wazee maana yake tumezeeka, hakuna jinsi. Halafu ninyi vijana mnatuita wazee, hatujazeeka midomo, midomo yetu inaongea. Kwa hiyo, mtuache na sisi tuendelee, tunasema hatuvumi lakini tupo. Sasa, kuna Sera ya Afya ambayo inaongea kwamba wale watoto chini ya miaka mitano na wazee

wanapaswa kutibiwa bure. Sawa sera ipo na ukienda hospitali utakuta madirisha yapo, lakini je, ni kweli wazee wanapata huduma? Ni kwa nini sera hii haitungiwi sheria? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kunapaswa kuwa na sheria ya kumlinda mzee kwenye sera hizi, zisitungwe tu kisiasa siasa, lazima kuwe na sheria ambayo inasema huyu mzee atakaposhindwa kupata huduma ataenda wapi? Ni kitu gani kinachomlinda? Kuwe na sheria ambayo inasema, huyu mtoa huduma asipotoa huduma huyu mzee aende wapi au aishie tu? Kwa maana wanakwenda hospitali, madirisha yapo, lakini dawa hakuna. Kwa hiyo, analazimika kutoa pesa kwenda kununua dawa, lakini hawezi kumwajibisha mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni sera ya kulinda hawa watoto na hata wazee, basi sera ziambatane na sheria yake. Jambo hili tumekuwa tukilisema kwa muda mrefu. Pia muda mrefu tumekuwa tukisema kwamba, wazee wanastahili kupata pensheni ili tulinde hadhi yao ndani ya familia. Mheshimiwa Jenista anakumbuka wakati ule alikuwa kabisa *champion* wa jambo hili, sijui mambo yaliishiaishia wapi. Tunapaswa kuhakikisha kwamba wazee wetu wanapata pensheni kidogo ambayo itawafanya wathaminiwe ndani ya familia. Kwa hiyo, tunaomba pensheni pamoja na sheria ili kutekeleza sera ambayo Serikali imetunga ili kama watakosa huduma wajue mahali pa kukimbilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa leo nisiseme mengi, niliyokuwa nayo ni hayo na nina uhakika wakiyachukua yataweza kusaidia, ni maoni yangu *personal* lakini yanaweza kuwa ni maoni ya jumla. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere wajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba katika Bunge lako Tukufu nilete shukrani za wananchi wa Hanang na Mkoa wa Manyara. Shukrani za Wanahanang pamoja na wananchi wa Mkoa wa Manyara tunaishukuru sana Serikali. Tarehe 3 Disemba, 2023 tulipata janga kubwa lililoikumba nchi yetu, janga la kihistoria, janga ambalo halijawahi kutokea. Sisi Wanahanang, sisi watu wa Manyara tuna kila sababu ya kuishukuru Serikali na tukianza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Jambo lile lilikuwa ni kubwa, jambo lile lilikuwa la kutisha na jambo lile lilikuwa la kushangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu kama nilivyosema ya kumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye wakati ule alikuwa na ziara nje ya nchi, lakini alisitisha ziara na kurudi nchini na kuungana na Watanzania, lakini kuungana na Wanamanyara pamoja na Wanahanang katika kuhakikisha wanatatua na kutusaidia sisi watu tuliokumbwa na lile tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais anakuja kutoka nje, mimi kama Mwakilishi wa vijana ninayetokea Wilaya ya Hanang nilikuwa sehemu ya kuwapigia Mawaziri ikiwemo Mheshimiwa Jenista Mhagama. Wanahanang tunamshukuru sana, Wanamanyara tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu. Washirikiana na sisi kikamilifu, hatukuwahi kutarajia, tulikuwa hatuna mavazi, makazi, malazi, huduma za afya na tumepoteza watu wetu lakini hatukuwa na uthubutu wa kuweza kufukua matope na kuwapata wananchi ambao walipotelea ndani ya tope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kupitia Mheshimiwa Rais, tunamshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na tunaishukuru Serikali nzima. Leo Wanahanang kupitia Serikali tunalishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wabunge na kwa kuongozwa na wewe, mliweza kuja Hanang kwa wakati na kuja kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavishukuru Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Nchi hii kwa ngazi zote. Tutakuwa wachoyo wa fadhila kama hatutakishukuru Chama Cha Mapinduzi pamoja na jumuiya zake hususan Jumuiya ya Umoja wa Vijana pale ambapo jeshi lilipokuja kusaidia kufukua miili kutafuta watu wetu, Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi haukurudi nyuma, tulishika nao jembe na beleshi kutafuta watu na kurudisha mali za wananchi. Kwa hilo watu wa Hanang tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatukuwahi kutarajia kama watoto wetu watarudi shuleni, ninavyoongea, watoto wa Hanang, watoto wa Manyara wamerudi shuleni na wanaendelea na masomo kama Watanzania wengine. Tunaishukuru Serikali, hatukujua tutazikaje lakini kupitia Mheshimiwa Jenista hakuna Waziri ambaye hatukuwahi kumwona Hanang, Mawaziri hawa tulikuwa tunakaa nao ndani ya halmashauri kwenye Ofisi ya Mkurugenzi kuhakikisha tunaongea lugha moja ya kutatua changamoto za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwaangalia Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Aweso, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ni Waziri yupi ambaye hakufika Hanang kupitia wewe pia Mheshimiwa Spika? Hatukutarajia kama vituo vya afya vya kwetu vingeweza kutoa huduma ambayo tulistahili, lakini tunaishukuru Serikali, tulikuwa hatuna huduma ya *Ambulance*, leo *Ambulance* imekuja. Tunaishukuru Serikali na kupitia Wizara ya Afya tunamshukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kuja Hanang na kuendelea kutatua matatizo ya Wanahanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wananchi wa Hanang waliopotelewa na makazi yao, ni kitu cha kushangaza, lakini kwa jeuri ya Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassani, tuna zaidi ya nyumba 130 zinajengwa kule Hanang kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Ahsante Serikali ya Awamu ya Sita, ahsante Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakuwa wachoyo wa fadhila sisi Wanahanang, sisi Wanamanyara tukiache kuzishukuru taasisi

mbalimbali, vyombo vya dini, Watanzania wote, vyombo vya habari ambavyo vilitusaidia kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema nitangulize shukrani za Wanahanang kwa sababu yaliyofanyika hatukuyatarajia, kwetu sisi ni miujiza lakini kwa sababu Serikali ni ya Mama na Mama ni msikivu, hakika uongozi wa mwanamke unatosha, unalipa na chenji inabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zetu kwa kazi kubwa iliyofanywa na Mawaziri hawa na Serikali, tunaomba, kwa kuwa tatizo lile lilikuwa ni kubwa, shughuli za kibinadamu zimerejeshwa kwa wakati, lakini kutokana na udharura ule bado changamoto zipo. Sasa, tunaiomba Serikali iweze kuiangalia Wilaya ya Hanang kwa jicho la kipekee kwa kuzingatia kuboreshwa kwa bajeti. *(Makofi)*

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Stella Fiyao.

**TAARIFA**

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, suala lililotokea katika Mkoa wa Manyara, Watanzania wote kwa ujumla walishiriki vikiwemo vyama vya upinzani. Kwa hiyo, kusema tu ilishiriki CCM wanakuwa hawatutendei haki watu wengine. Nashukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwanza Mheshimiwa Mbunge anaendelea na mchango kwa hiyo, hatujui kama angewataja mahali kama aliwaona. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa sababu, anaendelea na shukurani bado. Anaendelea, ametaja changamoto, labda walichokifanya chama kingine labda walishughulika na mojawapo ya changamoto kwa hiyo, anaendelea na mchango. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Asia Halamga, kuna taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Stella Fiyao kwa kunipa taarifa hiyo, lakini nilikuwa naendelea na mchango. Nikutaarifu kwamba, wananchi wa Hanang wapo wana-CCM, wapo wa vyama vingine na ndiyo maana nilikuwa naendelea na mchango wangu. Kwa hiyo, nakushukuru kwa kunisaidia kunipa taarifa hiyo na kumalizia kulisema hilo ambalo nilitaka kulisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikiendelea kutoa shukurani na kuomba Serikali ituangalie kwa jicho la kipekee kwa kweli, nimalizie kwa upande huo wa shukurani kuwashukuru sana wanachi wa Wilaya ya Hanang na wa Mkoa wa Manyara. Katika kipindi chote ambacho tumepata tatizo wamekuwa ni wananchi watulivu, wamekuwa ni wananchi wasikivu, wamekuwa ni wananchi waliosaidiana na Serikali kwa kila hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule wilayani mpaka sasa hivi tunaye Ndugu Msangi anayetokea Ofisi ya Waziri Mkuu, akiendelea kuratibu masuala haya ya maafa pale ambapo hapajakamilika. Tunawashukuru sana na changamoto zozote zitakazojitokeza, kama ambavyo tulivyopiga simu kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ambavyo tulivyogonga hodi na wakatupokea, basi sitasita mimi Mheshimiwa Asia Halamga kuja kusema ya wananchi wa Wilaya ya Hanang na wananchi wa Manyara. Najua Serikali yetu ni sikivu, imenisikia kwenye hilo na itatuongezea bajeti ili ile miundombinu ambayo imeharibika iweze kurejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Tuiombe Serikali kupitia Mfuko huu kwa sasa iweze kutuongezea fedha ili kutatua changamoto nyingi za vijana kwa sababu, kwa sasa hivi ile asilimia 10 ambayo ilikuwa inawasaidia sana vijana imesitishwa. Pamoja na asilimia 10 kusitishwa na huku kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ukiangalia kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilitengwa shilingi bilioni moja, lakini mpaka Februari 2024, hela hiyo haikuweza

kuingizwa. Kwa hiyo tuombe sana Serikali ipeleke fedha katika Mfuko wa Vijana ili kuweza kutatua changamoto na kuwasaidia vijana wa Kitanzania katika mkopo huu nafuu na kuachana na mikopo ya kausha damu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa siku ya leo itoshe kusema nalishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuhakikisha mnatupa nafasi sisi Wabunge ya kuwasemea vijana na kuwasemea wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mchango wangu wa kwanza niuelekeze kwenye uzalishaji wa chakula na lishe. Naishukuru Serikali ya Tanzania ambayo kwa miongo mitatu imeweka *concentration* kubwa wenye uzalishaji wa chakula na matokeo yake tumeona, kwamba, Tanzania tunazalisha chakula cha kutosha na tunajitosheleza kwa chakula kwa zaidi ya 100% au 124%.

Mheshimiwa Spika, bado Tanzania tuna changamoto kubwa ya kilishe na tuna changamoto ya udumavu. Changamoto ya udumavu ni kubwa, asilimia 30 ya watoto wetu wana udumavu. Udumavu ni changamoto ambayo baadaye huwezi kurekebisha. Kwa mfano, udumavu wa ubongo, udumavu wa mwili kiasi kwamba, wanafunzi walioko darasani huwezi ukawafundisha wakakimbizana na teknolojia ya sasa na hata wanapokuwa watu wazima wanashindwa kujijenga katika uchumi huu ambao teknolojia nyingi zinazotumika ni za kisasa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni wazuri kwa kuzalisha. Ukiangalia mikoa inayoongoza kwa udumavu ikiwepo Iringa, Njombe, Rukwa, Geita mpaka Bukoba ni maeneo mazuri kabisa

ya uzalishaji, lakini hebu ona tutakuwa na Taifa ambalo kesho na kesho kutwa wana udumavu kwa kuwa sasa tunaweka uwekezaji mkubwa kwenye maendeleo ya vitu bila kujali watu, kiasi kwamba siku moja watashindwa kuvitawala hivi vitu.

Mheshimiwa Spika, kuna *gap* hapa katikati. Kwa nini katika nchi 10 mbaya duniani zenye udumavu Tanzania ipo? Katika nchi 10 Afrika zenye udumavu Tanzania ipo? Hii ni aibu kwa Watanzania. Katika miaka 60 ya uhuru tunayoongea bado tunaongea udumavu? Bado tunaongea changamoto za kilishe Tanzania? Tujue kuna *gap* hapa katikati kwa sababu, tumezungukwa na maziwa, tuna mabonde mazuri ya uzalishaji, tuna mifugo, kwa nini bado tuendelee kuwa na udumavu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya wekundu wa damu ambapo wanawake wengi wanaathirika. Wanawake walio kwenye umri wa kuzaa, miaka 15 mpaka miaka 49, wana changamto hii ya upungufu wa wekundu wa damu na vifo vingi vya uzazi vinatokana na upungufu wa wekundu wa damu. Hata watoto karibu 50% wana upungufu wa wekundu wa damu. Changamoto hii ni *serious* na kwa sababu tunazo rasilimali za kutosha na tuna vyakula vya kutosha, lazima tujue *gap* hapa katikati linasababishwa na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto ya upungufu wa vitamini A. Tunaona siku hizi watu wana uono hafifu, hata wanafunzi wa rika zote wanavaa miwani. Hebu tuangalie wapi kuna *gap* katika nchi hii ya Tanzania kiasi kwamba, changamoto ya lishe bado inakuwa kubwa?

Mheshimiwa Spika, kuna kampeni ya Kitaifa, kuna kampeni ya siku 1,000 toka mtoto akiwa tumboni mwa mama yake, lakini ukiangalia kwenye idadi kubwa ya wanawake walio kwenye umri wa kuzaa, miaka 15 mpaka 49, ambao wanafika 14,992,288 sawa na 47%, hii kampeni imewafikia kwa kiasi gani? Kwa sababu, udumavu wa mtoto na upungufu wa lishe, unaanza toka siku ya kwanza ya mtoto kwenye tumbo la mama.

Mheshimiwa Spika, kuna kampeni pia ya afua za lishe. Nataka kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali inasimamia hii afua ambayo ni mtambuka kwenye wizara zote na ni kwa kiasi gani wanafanya? Kwa sababu ni aibu kwa Tanzania, hivyo tufahamu ili tuone kama mkakati huu unafaa kuondoa kabisa tatizo la utapiamlo katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampeni ziko nyingi, kwenye hotuba ya Waziri ameeleza kwenye *page* namba 19, aya 193 mpaka 195, inaeleza mkakati wa nchi katika kuondoa upungufu wa lishe. Nafikiri Serikali isimamie Wizara zote zichukue afua ya lishe kama mtambuka na kuona namna gani kila Wizara na halmashauri zote zinatenga bajeti ili kuondoa tatizo la lishe ambalo ni changamoto kubwa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu viwanda vyetu. Uwekezaji katika viwanda, lakini matumizi ya mazao yanayotoka kwenye viwanda vyetu. Tunatumia fedha nyingi, 60% ya vipuri, magari, mitambo tunaagiza kutoka nje, lakini kumbe tuna uwezo mkubwa wa kupunguza kiwango hicho kama tukiwa na nia ya dhati ya kutenga fedha katika bajeti hii, kuboresha viwanda vyetu na kuweza kutumia bidhaa zinazotokana na viwanda. Kwa mfano, tuna *CAMARTEC* Arusha, *CARMATEC* ni jibu kwa vipuri vya wakulima na wafugaji; wanatengeneza mashine mbalimbali, matrekta madogo yanayoweza kulima na kupanda, wana mashine za kuvuna, wana mashine za kupukuchua, wana mashine mbalimbali za kusindika vyakula vya mifugo, lakini kwa nini sasa tusikirasimishe kikafanya kazi kibiashara, kuliko kuagiza hata *power tiller* kutoka nje na hazina maisha na vipuri vingi vinapatikana kutoka hapa? Sasa tuone namna gani tunawekeza kwenye Kituo hiki cha *CAMARTEC,* lakini pia, wananchi wetu, kwa uzalendo wawe mstari wa mbele kutumia vifaa vya *CAMARTEC*.

Mheshimiwa Spika, kuna *TEMDO,* wana uwezo mkubwa sana wa kuzalisha vifaa mbalimbali kwa ajili ya taasisi zetu. Kwa mfano afya, *TEMDO* wanazalisha vitanda vizuri tu vya wagonjwa hospitalini, wanazalisha hizi *fridge* ambazo zinatumika *mortuary,* lakini sisi hatuitumii *TEMDO* kuzalisha hivyo vitu. Pengine uwezo

wao ni mdogo, lakini kwa nia thabiti kabisa, kwa nini isifanyike *local arrangement, TEMDO* wawezeshwe fedha na kila kitu waweze kuzalisha hivi vifaa ambavyo vinahitajika katika taasisi mbalimbali ikiwepo afya ili tupunguze fedha za kigeni tunazotumia kuagiza hivi vitu kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TEMDO* haiwezi ku-*compete* na taasisi nyingine kwa sababu, kwa mfano *Medical Store Department* inavyoagiza vitu inatoa *tender* ya kuzalisha vitu vingi ikiwepo *syringe*, kiasi kwamba *TEMDO* haiwezi ku-*compete* na taasisi nyingine. Sasa, Serikali inaweza ikafanya *locally,* ikawapa *TEMDO* kuzalisha vifaa vinavyotakiwa pengine kama kuna *gap* ndiyo iagize kutoka nje. Kwa hiyo, nafikiri kwa uzalendo wa nchi yetu sasa tuone kwamba, vile vitu vinavyoweza kuzalishwa ndani ya nchi yetu vizalishwe, tuwape nguvu, tuwape mtaji, ili tuweze kuwatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kiwanda cha *KMTC (Kilimanjaro Machine Tools)* wanazalisha vitu vizuri sana. Wanazalisha mitambo, wanazalisha viwanda vya sukari, wanazalisha vyuma vyote, nondo na vyuma vinavyotumika katika nchi yetu. Hawa changamoto yao ni malighafi. Ukiona kiwanda kikubwa kama hicho na naishukuru Serikali imefanya ukarabati, imesimika mtambo mkubwa wa kuyeyusha chuma, lakini kinafanya kazi chini ya kiwango kinachotakiwa kwa sababu, ya kukosa malighafi. Bado wanategemea chuma chakavu kinachookotwa mitaani na kupelekwa kwenye kiwanda ndio kiweze kufua umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nchi yetu ina nia ya dhati ni kwa nini sasa hivi tusikamilishe Mradi wa Liganga, ili *KMTC* wakapata malighafi ya kutosha? Wana uwezo mkubwa wa kuzalisha vyuma ambavyo nchi yetu inavihitaji katika miradi mbalimbali, katika Mradi wa *Standard Gauge* na kujenga kwa sababu, tunatumia fedha nyingi kuagiza vyuma kutoka nje. Kwa nini Serikali isifanye hivyo ili liwe ni suluhisho la upatikanaji wa vyuma na kila kitu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, ingeweka kipaumbele kabisa katika kukamilisha Mradi wa Liganga ili viwanda vyetu hivi ambavyo changamoto kubwa ni upatikanaji wa malighafi, ambapo Liganga inaweza kuzalisha zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka, ikavipatia viwanda vyetu vya *TEMDO* na *KMTC*. Viwanda hivi vina uwezo kabisa wa kuzalisha vipuri vya kutosha kwa ajili ya matumizi ya Watanzania, kwa ajili ya taasisi mbalimbali ili tuweze kujikwamua kutoka kwenye changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nimemaliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Deus Sangu ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi ni mwanakamati, kwa hiyo, naunga mkono yale yote yaliyozungumzwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu, nchi yetu sasa hivi imetulia, wananchi wana maendeleo na vitu vinaendelea kuonekana. Kwa hiyo, tunaendelea kumshukuru, Mungu amlinde, aendelee kuwepo na wale wanaosema tano tena, mimi nadhani siyo tano tena, kwamba yeye alishashinda ila kura ndio sijui ni ngapi, sisi Wabunge ndiyo tunatafuta. Kwa hiyo, naendelea kumwombea aendelee kuwepo ili aiendeleze nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi kubwa sana, anazunguka nchi nzima, amekuwa *bulldozer,* tunamwona anaenda kila mahali. Tunamshukuru Naibu Waziri Mkuu na yeye anatembea, anasuluhisha matatizo ya wananchi na nimshukuru Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo kwenye Wizara hii, Mstaafu Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Waziri mpya Mheshimiwa Ndejembi na Naibu Waziri Mheshimiwa Katambi, wote tunawashukuru kwa kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wakurugenzi wa Taasisi kwa sababu tunafanya nazo kazi, haya mashirika ya kijamii, Mifuko ya kijamii, kuna *PSSSF*, *NSSF*, *OSHA* na *WCF* wanafanya kazi nzuri, tumeona majengo yao, tumeona wananchi wanavyokuwa wanahudumiwa na zile taasisi na jamii. Niendelee kuwashukuru ili watende kazi nzuri, Mungu atawabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na miradi ya kimkakati. Nianze na Mradi wa Bwawa la Nyerere. Wamezungumza Waheshimiwa Wabunge hapa, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano ambalo linaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia, tuangalie hali ya umeme nchini kwa kweli, hali ya umeme nchini inatisha sana, inatisha mno. Umeme unapokatika kwa sababu upo katika maeneo mengi, hili giza la usiku linawapa shida sana wananchi. Biashara zinakwama, yaani kila mtu sasa hivi anategemea umeme, kwa hiyo tuombe sana watu wanaoshughulika na umeme na wizara inayoshughulika na masuala ya umeme wajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere, imefanya vizuri, lakini waendelee kuweka bidii ili tuweze kupata umeme. Kwa taarifa ya leo nchi yetu itapata matukio makubwa mawili usiku wa leo, leo tarehe 5/4/2024 kuanzia saa tatu mpaka saa tano kutakuwa na kupatwa kwa jua na kupatwa kwa mwezi kwa mara ya kwanza katika nchi yetu ya Tanzania kwa hiyo, umeme usikatike. Tunaomba leo, kuanzia saa tatu mpaka saa tano umeme usikatike. Tena tuwaombe wanaohusika wasikie kwamba, umeme usikatike. Kwa hiyo, naomba kwenye eneo hili Waziri wake ni Naibu Waziri Mkuu aangalie umeme leo usikatike kuna kupatwa kwa jua na kupatwa kwa mwezi kuanzia saa tatu mpaka saa tano. Naomba jambo hili lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie mfumo wa ajira. Mfumo wa ajira katika nchi yetu Wabunge tumeshazungumza hapa, hauko sawa. Huu mfumo unaoitwa *Ajira Portal* au Ajira Mtandao hauko sawa kwa sababu, hatuna uhakika watoto wangapi wanachukuliwa kutoka mikoa mbalimbali. Tumezungumza hapa kwamba, huu mfumo wa ajira uangaliwe upya, hasa kwenye walimu na waganga, wale watu

wanaokwenda vituo vya afya na zahanati. Tuombe sasa hizi ajira 240, 250, 300 au mia ngapi, zigawanywe kwenye maeneo ya mikoa kama siyo majimbo ili tuwe na uhakika kwamba, Mkoa wa Mara una watu wameajiriwa, Mkoa wa Kilimanjaro una watu wameajiriwa au Mkoa wa Mbeya una watu wameajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mfumo wa ajira, *Ajira Portal* una upendeleo wa hali ya juu kwa sababu, watoto wa Kitanzania walio maskini wanasoma shule za kawaida, watoto wanaoweza kufanya vizuri na kuongea Kiingereza vizuri ni wale wanaosoma *English Medium* na wengi hawasomeshwi huko ndani. Kwa hiyo, ajira hii ikifuata hivyo wataanza wa A, wale wa B na C hawatapata ajira. Kwa hiyo, niombe hili tuliangalie vizuri, hii ajira iangaliwe, *distribution* iwepo, tugawanye kwenye mikoa ili kila mkoa uwe na uhakika wa kujua kwamba, watu wake wanapataje ajira hizo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Vijana, wamezungumza watu wengi sana hapa. Mimi ni Mjumbe wa Kamati, kuna shilingi 5,000,000,000 ilitengwa tangu 2018 lakini haijawahi kutoka. Wametenga shilingi 1,000,000,000, haijawahi kutoka na tunataka tukopeshe vijana kwenye Mfuko wa Vijana wa Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaomba hii shilingi 1,000,000,000 iliyotengwa itoke mapema ili vijana waweze kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya majengo ya shule za msingi ni mbaya. Ni mbaya zaidi kwenye Jimbo la Bunda, sielewi majimbo mengine. Kuna shule za msingi za miaka ya uhuru mpaka leo, majengo yamechoka. Serikali ifanye mpango mkakati wa kuzikarabati shule hizi.

Mheshimiwa Spika, tunaposikia kwamba, kuna hela zimeliwa mabilioni, watu wanafanya mikutano nje, wakati majengo yetu yamechoka na pengine watoto wetu wengine wanakaa chini, inauma sana. Kwa hiyo, niiombe Serikali ianze kutenga fedha ili maboma ya shule za msingi yajengwe, lakini shule mbovu ziweze kukarabatiwa na hasa kwenye Jimbo la Bunda.  Kwa mfano, kuna shule 10 kwenye jimbo langu, kuna shule ya Saramba A na B,

Steven Wasira, Nyansiloli, Nyang'arambe, Marambete, Nyamswa A, Nyamswa B, Salato, Sanzati na Saramakati, zote zimechoka sana. Shule hizi 10 ukienda kuzitazama unataka ukimbie. Huu Ubunge nao una shida zake, unaweza ukaangalia watu na shule unasema hivi na Ubunge huu sasa nafanyaje na sina uwezo. Niombe wanaohusika watusaidie sisi Jimbo la Bunda tuweze kujenga hizi shule kwani zimechoka mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna malipo ya tembo. Bahati nzuri nimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu wake, kwa kweli tumekaa wote tunaohusika na maeneo ya tembo, wametuahidi kulipa fidia katika maeneo haya. Kwangu walifika wakafanya tathmini, lakini malipo hamna. Sasa wananchi wanauliza, kila siku mnakuja kufanya tathmini, malipo yako wapi? Kwa hiyo, niiombe tena Wizara hiyo. Niwasisitize tena, waende wakawalipe wananchi wa Bunda kwenye maeneo yale ambayo walienda waweze kuwasaidia, kwani wananchi wale mazao yao yameharibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna malipo ya fidia ya vijiji vitatu, Nyatwali, Serengeti na Tamau. Nimesikia hata Mheshimiwa Rais jana alikuwa anaongelea hili jambo. Amemwambia Mkuu wa Mkoa wa Mara aende akaangalie. Hivi unawezaje kukaa na watu umewazuia kulima, umewazuia kufanya kazi, umewazuia kufanya chochote, wapo tu, alisema atawalipa mwezi wa Tisa mwaka jana lakini mpaka leo hawajalipwa, umekuwa wimbo tu? Watu wanalia huku na huku, malipo yenyewe ni kidogo, kwa nini wasilipwe? Hapo ndio shida ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamezuia watu ili wanyama waende kunywa maji Ziwa Victoria tutunze mazingira, maajabu ya ziwa na ya Serengeti, lakini watu hawalipwi. Sasa tunaomba Serikali kwa kuwa imeahidi kwenda kuwalipa iharakishe ili waende kufanya kazi zao kwenye maeneo yao kwa kadri wanavyohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu wananchi wangu wanatembea kilomita 240 kwenda kutafuta halmashauri. Nimesikia mara nyingi sana Serikali inasema kwamba, wanatengeneza miundombinu iliyokuwepo kwa halmashauri

walizounda. Mimi kwangu iliyokuwa Halmashauri ya Bunda majengo yapo, majengo yapo tu na popo ndiyo wanaoishi humo ndani. Majengo yapo Halmashauri ya Bunda ina majengo. Sisi tunaomba turudishwe kutoka Kibara kilometa 240, tuingizwe kwenye majengo yetu. Sisi tunachohitaji ni uteuzi wa Mkurugenzi tu, kwa hiyo, tupewe Mkurugenzi kwenye majengo yetu ambayo yapo. Kwa hiyo, kama ni miundombinu wawaambie wanaohusika sisi tuna majengo, watuletee Mkurugenzi ili waweze kupunguza mwendo mrefu ambao wananchi wanahangaika, kilometa 240 ni parefu sana. Kwa sababu tunataka kutoa huduma karibu na wananchi, tunaomba tusaidiwe kwenye jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Halmashauri tumejenga hospitali za halmashauri, Hospitali ya Bukama imejengwa imetumia shilingi 3,600,000,000 ina Waganga wawili na haijakamilika mpaka leo. Kwa hiyo, niombe wanaohusika na bahati nzuri wameikagua Mawaziri wameenda pale mara mbili au tatu na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi amepita pale, tukamwambia tunaomba hospitali ya Bukama ipewe Waganga ili ifanye kazi, kwa sababu hatuwezi kutumia hela nyingi sana halafu tumebaki na majengo. Kwa hiyo, hospitali hii tunaomba isadiwe ili iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna ujenzi wa sekondari; tunaendelea kujenga sekondari, kuna eneo langu la Nyaburundu, wanafunzi wanatembea kilometa 36, wananchi wameanzisha ujenzi wa sekondari, tunaomba Serikali iwa-*support* Nyaburundu wapate sekondari. Wameshajenga msingi na wanaendelea kujenga. Kuna Manchimweru wasaidiwe kujenga sekondari kwa sababu Watoto wanatembea kilometa 40. Kuna maeneo mengi ambayo wananchi wanatembea mwendo mrefu kwenda kutafuta shule za sekondari. Kwa hiyo, tunaomba wananchi kwenye maeneo haya wasaidiwe kujenga shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya kwangu leo yalikuwa hayo, nam-*support* Mheshimiwa Rais na nimwombe tu aendelee kutenda kazi na namshukuru kwa safari zake anazoenda, anatuletea heshima kwenye nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenisaidia kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa, hakika Mungu amekuwa msaada wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, lakini pia, kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Taifa hili la Tanzania, tunaiona na kwa kweli tunampongeza sana. Nimpongeze Waziri wetu Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na timu yake, wanafanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze sana na kuendelea kumwombea kwa Mungu Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Ni ukweli usiopingika Mheshimiwa Rais ameleta fedha nyingi kwenye miradi mingi kwenye majimbo yetu. Kwa kweli tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumpa afya njema ili aendelee kututumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuchangia suala la makusanyo katika nchi yetu. Tunayo miradi mingi ambayo imeletwa kwenye maeneo yetu na miradi hii inahitaji fedha nyingi. Pamoja na Serikali kuendelea kukusanya fedha nyingi, lakini bado kuna shida kwa Watanzania wengi. Watanzania wengi hatuna utaratibu wa kulipa kodi na hatuna utaratibu wa kudai risiti na kutoa risiti. Nimekuwa nikifanya utafiti na wakati mwingine ninapokwenda Dar es Salaam au hata hapa Dodoma; unapoenda kwenye maeneo mengi wafanyabiashara wengi hawatoi risiti, lakini na Watanzania walio wengi huwa hatudai risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo la makusanyo tukiiachia Serikali naamini haitaweza. Hili jambo tulibebe kama Watanzania liwe la kwetu sote ili Serikali iweze kupata mapato. Mapato haya

ambayo ndiyo yanaenda kuleta maendeleo kwenye Taifa letu. Niombe sana Waheshimiwa Wabunge hili jambo tulibebe. Sisi tunakutana na wananchi, tunafanya mikutano mingi. Hebu tukatoe elimu kwa wananchi wetu, kwa nini tunataka wananchi wadai risiti na wafanyabiashara watoe risiti? Ni kwa sababu ya faida ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuja hapa Bungeni kila Mheshimiwa Mbunge anasema nataka maji, nataka barabara, nataka umeme lakini yeye amehusika vipi katika kutafuta fedha ambayo itaenda kuendeleza miradi hii. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla lakini pia, niiombe *TRA* wafanye kazi yao, wasimamie vizuri, kwa sababu unaenda kwa wafanyabiashara, lakini ukiuliza wafanyabiashara wengi hizi mashine za kutoa risiti mwingine anakwambia imeharibika, ni zaidi ya wiki mbili ameipeleka kule *TRA* na hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoteza mapato mengi, kwa sababu wengine wapo ofisini, wamekaa wanasubiri mwisho wa mwezi kupata mshahara. Kwa hiyo, niombe sana Waheshimiwa Wabunge, Watanzania tuwe wazalendo, jambo hili la kupata mapato mengi ni kwa faida ya nchi yetu siyo kwa faida ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niongelee suala la ushirika; Serikali inazungumzia kuhusu kuendeleza ushirika, ushirika ni jambo muhimu kwa wananchi wetu. Nitoe mfano, kule kwetu Kyerwa na Mkoa wa Kagera. Mazao mengi hasa hasa zao la kahawa tulikuwa hatuuzi kwenye ushirika, lakini leo hii tunaona faida kubwa na leo hii kwa kweli nimpongeze sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe. Mawaziri wengi walishindwa kusimamia suala la kahawa kuuzwa kwenye mnada ili pawepo na ushindani. Waheshimiwa Wabunge mimi ni shahidi kwetu Kagera hasa hasa Wilaya ya Kyerwa kahawa ilikuwa inauzwa shilingi 1,100, lakini baada ya Mheshimiwa Rais kuridhia kahawa hii iuzwe kwenye mnada pawepo na ushindani, kahawa imefika shilingi 3,200.

Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunampongeza sana Mheshimiwa Bashe amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana kwenye ushirika na hili ni jambo ambalo liende moja kwa moja kwa wakulima, tunataka ushirika huu uweze kumsaidia mkulima anapoanza kulima, anapoanza kuhudumia zao kama ni kahawa, kama ni pamba, haya mazao yote yanayouzwa kwenye ushirika pawepo na fedha ya kumsaidia. Hapo mnaongelea Benki ya Kilimo, Benki hii ya Kilimo hatujaiona kwa wananchi wa hali ya chini. Tunaiona kwa wafanyabiashara wakubwa ambao wanakuja kuwalangua hawa wakulima. Tuone hii Benki inaenda kwa wananchi wa hali ya chini ili kuwasaidia. Huyu mwananchi anapoanza kuhudumia kahawa, kuandaa kahawa yake mpaka ifike wakati wa kuipeleka kwenye mnada awe na fedha ya kumhudumia. Hii itaondoa biashara ya *butura*, itaondoa biashara ya *kangomba*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana hili jambo walisimamie. Nimeona Serikali ina mpango nzuri wa kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika, sasa tuombe sana hii Benki inapoanzishwa na yenyewe iende kuwahudumia wananchi wa hali ya chini isiishie hapo juu. Naiomba sana Serikali iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunapowasaidia wakulima, niseme kwa mfano Kyerwa, sisi ni wazalishaji, hakuna wilaya inayozalisha kahawa nyingi kama Kyerwa, lakini bado hatujaona nguvu kubwa ya Serikali ya kwenda kumsaidia huyu mkulima. Hawa Maafisa Ugani wapo wapi? Maafisa Ugani na Serikali huwa tunaiona kahawa ikishakomaa, wanapeleka kwenda kuuza. Sasa tuone hawa Maafisa Ugani wanamsaidia mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka kushauri kwenye suala la kilimo ni kwamba, tunao hawa watu wanaofanya utafiti wakati mazao yanapopatwa na magonjwa, nashangaa sana, mtu ambaye ni mtaalam anakwambia bwana kahawa imepatwa na ugonjwa wa mnyauko, mje muikate muitoe. Hivi kweli mtaalam umesomea kukata kahawa na kuing'oa, ndio utaalamu uliousomea? Waje na utaalamu ambao

utamsaidia huyu mkulima pale kahawa yake au zao lingine linapopata shida aweze kupata utaalam wa kusaidia zao lake lihudumiwe na kuondoa haya magonjwa. Hili lipo hata kwenye migomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee suala la usafirishaji; niombe Serikali, ni kweli inaendelea kuboresha barabara, inaweka nguvu kubwa, hili tunalipongeza sana, lakini naomba tuweke nguvu sana kwa wananchi wa hali ya chini huku ambako ndiko kuna wakulima wengi. Serikali iweke nguvu, iboreshe miundombinu, tutakapowawekea miundombinu mizuri hawa wananchi, watasafirisha mazao yao kwa urahisi, lakini pia tutapunguza gharama za uzalishaji wa mazao haya. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iliangalie hili na iangalie maeneo ambayo yana shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, niongelee kwetu Kyerwa, Mkoa wa Kagera na mikoa mingine, tuna vipindi virefu vya mvua. Mikoa hii na wilaya hizi ambazo zina vipindi virefu vya mvua, barabara zijengwe kwa kiwango cha changarawe. Hali ni mbaya huko katika kipindi hicho na wakulima wanashindwa kusafirisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilisemee ni suala la maji; niipongeze sana Serikali, imewekeza fedha nyingi, Serikali inaongelea kufikia asilimia 95 na asilimia 85. Ili tuweze kuifikia, tumeanzisha miradi mingi. Niombe sana Serikali penye miradi hii ihakikishe inaikamilisha. Miradi mingi bado ina madeni mengi, hatutaweza kufikia lengo kama hii miradi hatutaisimamia ikakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, kuna Mradi wa Kaisho - Rutunguru na Isingiro. Mradi huu unajengwa kwa awamu mbili, lakini mkandarasi amemaliza amefikia 85% bado anadai. Amelipwa 30%, hawezi kuendelea, mradi huu umesimama na hii ni awamu ya kwanza unajengwa kwa awamu mbili. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iwekeze sana kwenye kukamilisha miradi hii ambayo tumeianzisha ili iweze kuwahudumia wananchi wetu wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilisemee, Serikali iangalie sana wameweka nguvu sana katika kujenga vyumba vya madarasa na kujenga shule nyingine mpya, tunapongeza sana. Kwa kweli hapo Serikali imefanya kazi kubwa sana, lakini tukumbuke kuwa, kuna shule ambazo ni za zamani. Shule hizi zimechakaa, unakuta pembeni wamejenga vyumba viwili vipya lakini wanafunzi wengine wanasoma kwenye darasa la zamani ambalo hali yake ni mbaya. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ianze kuwekeza sasa kwenye shule ambazo ni za zamani, shule kongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naendelea kuiombea Serikali, kwa kweli wanachapa kazi kubwa sana…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** … fedha ambazo zipo kwa wananchi, Serikali watembee kifua mbele, Watanzania wanaona. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa Mbunge fulani alipita kati ya Kiti na Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge umemwona anayezungumza alipo? Rudi nyuma halafu utarejea.

Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Deus Clement Sangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nipate kuchangia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyowasilishwa hapa Bungeni. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwaletea maendeleo Watanzania. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mchango wangu utajikita kwenye mambo mawili makuu. La kwanza, nitazungumzia suala la maafa jimboni, lakini la pili nitazungumzia mfumo wa ununuzi wa mazao ya wananchi kupitia *NFRA*.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na maafa jimboni; naomba kwanza kupitia Bunge lako nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Kwela kwa maafa makubwa ambayo yanaendelea jimboni kutokana na mvua nyingi zinazonyesha. Mpaka ninavyongea hivi tumepata maafa makubwa sana. Ukianza kwenye miundombinu ya barabara takribani juzi niliuliza swali hapa kuhusu madaraja 12 ambayo yameondoshwa na mafuriko, lakini juzi yameongezeka madaraja mengine mawili na usiku wa kuamkia leo katika Kata ya Muze, Kijiji cha Uzia, Kata ya Mtowisa katika Kijiji cha Kifinga na pia Kijiji cha Lwanji madaraja mengine yameondoka. Kwa hiyo, imefanya jumla ya madaraja yaliyoondoka kuwa ni madaraja 18. Bonde la Ziwa Rukwa lakini katika Kijiji cha Ilombo, Kata ya Mpui napo pale hakuna mawasiliano yamekatika kabisa.

Mheshimiwa Spika, madhara yake nini? Madaraja yote haya yaliyoondoshwa nilikuwa napata tathmini ya hasara iliyoingiwa ni takribani bilioni sita.  Hasara yake ni kwamba, barabara hii ndiyo inayounganisha Mkoa wa Songwe katika Jimbo lile la Momba kwa Mheshimiwa Condester na upande mwingine Jimbo la Kavuu kwa Mheshimiwa Pinda. Kwa hiyo, hakuna mawasiliano kupitia Bonde la Ziwa Rukwa kutoka Katavi, wala huwezi kwenda Songwe mawasiliano yamekatika na barabara takribani kiliomita 100 zimeondoshwa, hakuna mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yupo Mkuu wangu wa Wilaya kule ndugu yangu Nyakia wanapambana. Sasa tatizo hili ni kubwa limeharibu mawasiliano kwa kiasi kikubwa na Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya amekuja mara nyingi katika Jimbo la Kwela. Naomba nitoe ombi *special,* ikiwezekana katikati hapa wikiendi moja, kwa sababu uharibifu ule ni mkubwa, Mkoa wa Rukwa ume-*stuck*, kwa sababu lile bonde ndio bonde la uzalishaji, twende na Waziri tukajione tatizo hili ili tunavyoongea sasa tuwe tunaongea lugha moja.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Jenista kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tuwasiliane pia na Waziri wa Ujenzi tuone namna ya kwenda ku-*rescue,* hali ni mbaya kule. Kata 13 zote za Bonde la Ziwa Rukwa hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, niliona niliseme hili kwani ni jambo kubwa, ni msiba kwetu, ni vilio Jimboni Kwela, hamna mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, shule zimeezuliwa, kuna shule ya Kijiji cha Chombe, Kata ya Kaoze, Shule ya Sekondari Mpui, Shule ya Msingi Kapenta zimeezuliwa na Jumatatu shule zitafunguliwa watoto hawana pa kwenda. Kwa hiyo, hili jambo ni la dharura, niwaombe sana walichukulie kwa udharura wake, tutafute fedha za dharura, twende tukawasaidie watoto ili siku ya Jumatatu shule zikifunguliwa nao waende kuendelea na masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumekumbwa nalo wananchi wamepata kadhia kubwa, tulikuwa tumefika msimu wa mavuno, tayari mazao yameshaiva na wananchi walikuwa wanajiandaa kwa ajili ya kuvuna, tumepoteza takribani hekta 450 za mahindi ambazo kwa thamani ya fedha hasara ambayo inakadiriwa ni milioni 260. Pia, kwenye mpunga takribani hekta 205 zimekwenda ambazo ni thamani ya takribani milioni 160. Kwa hiyo, wananchi wameathirika, lakini kaya zaidi ya 400 hazina pa kuishi ambapo zina wakazi 2,102 kwa takwimu tulizozipata jana. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Jenista kwa udharura wa hili, misaada ya kibinadamu kama chakula, magodoro inahitajika, kwa sababu sasa hivi ninavyoongea, watu 2,102 hawana mahali pa kukaa kule Jimboni Kwela.

Mheshimiwa Spika, naamani kwa uharaka ule na udharura wanaofanya kwenye majanga sehemu nyingine, watachukua hatua hiyo hiyo twende tukafanye jambo na nimemwandikia haya yote kwa maandishi, nimempelekea barua ili aweze kuchukua hatua kupitia Ofisi yake. Kwa hiyo, ni hali ya majanga tu iliyopo kule Jimboni Kwela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiachana na majanga yanayoendelea, naomba nizungumzie kidogo, suala la *NFRA*. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kipindi cha miaka miwili. Kwanza kuweka ruzuku kwenye mazao. Kwa kweli uzalishaji kwenye Mkoa wa Rukwa, Jimbo la Kwela umekua sana na kipindi hiki cha msimu huu wa kilimo hatukuwa na malalamiko makubwa sana. Pamoja na mafuriko haya ninayosema na shida zinazojitokeza bado uzalishaji mwaka huu utakuwa mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hofu yetu kubwa ni kwamba, tunaweza tukapata changamoto ya masoko tena ya zao la mahindi. Sasa ndugu yangu Mheshimiwa Bashe, tulikuwa tunateta wakati fulani. Nchi jirani zinazotuzunguka zimepata majanga, wao wamekutana na ukame, sisi huku kwetu tumepata mvua nyingi ambazo zimepitiliza, sasa kuna fursa za nchi jirani. Jana nimeona tangazo *NFRA* walilitoa tarehe 25 Machi, 2024, wanawatangazia wananchi utaratibu mpya wa kununua mazao kupitia *NFRA*. Katika utaratibu huo Serikali imeweka jambo moja ambalo kidogo linaonekana ni zuri kwa *NFRA* na lina faida, kwa maana kwamba, mikataba zile *framework agreement* wanazoenda kuingia na wakulima wakubwa, zitaipa *NFRA* fursa ya kwenda ku-*access* taasisi za fedha na watapata fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hizi taasisi zinaweza zikaleta ukiritimba kwa namna nyingine. Ndio wakulima wadogo hawajawa *restricted* watauza kwa utaratibu wa zamani lakini kwa kuingia *framework agreement* kwa wakulima ambao wana ekari 100 na wanaweza kui-*supply NFRA* zaidi ya tani elfu 2,000, maana yake watageuka hawa kuwa madalali wa hawa wakulima wadogo na kuwaonea. Kwa hiyo, hawa wakulima wadogo watakuwa sasa hii sheria au mikataba haiwaathiri moja kwa moja,

lakini hawa watawahi kule kukusanya mazao, wao watakuwa madalali na hawa wakulima wadogo wadogo ambao ndio wengi wataathirika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni nini hapo? Tufanye jambo moja kama tunavyofanya kwenye mbolea ya ruzuku, tunamtambua mkulima mmoja mmoja ana ekari ngapi, ana mashamba gani, kwenye mfumo huo huo tunampa mbolea ya ruzuku. Nataka huo huo mfumo u-*apply* kwenye *NFRA* hata wakulima wadogo wadogo, kama si mmoja mmoja tuwa-*aggregate* wawe wengi, tuwaweke Pamoja, nao wapewe *framework agreement* kama tulivyowapa wakulima wakubwa, tuwasaidie nao ili tuwainue.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu tukiwaacha hivyo, tunakwenda kutengeneza madalali, mwezi wa Saba *NFRA* ikifunguliwa itakuwa ni ya wale ma-*giant,* wenye ekari 100 wanaoweza ku-*supply* tani 2,000, hawa wakulima wadogo watabaki *redundant,* hivyo, watakuwa ni wachuuzi. Kwa kuwa Serikali walishaanzisha mfumo mzuri kupitia mbolea ya ruzuku, mfumo ule ule tuutumie kwenye masoko, tuupeleke *NFRA* ili na mkulima mdogo ajione naye anahusika, kwa sababu wakulima wadogo ndiyo *majority*. Kwa hiyo, natoa ushauri huu kwa Serikali, naomba iufanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili linalolalamikiwa, unapoenda *NFRA* kupima mzigo wako, unakatwa kilo moja ya ule mfuko uliowekea, yaani ule mfuko wa salfeti unahesabika kwamba una kilo moja, kwa hiyo kama una kilo 100, ukipima wanakata kilo moja kama gharama ya mfuko. Siku moja nimekutana na Mheshimiwa Waziri nikamwambia kweli kwa hali ya kawaida salfeti linaweza likawa na kilo moja? Ikizidi sana ni 0.5 *grams*, kwa hiyo, naomba hili waka-*review,* kumkata mkulima kilo moja ukizikusanya zile ni fedha nyingi na ni kama kumuibia mkulima. Katika msimu ujao tu-*review* hili jambo likae vizuri ili wakulima waweze ku-*enjoy* na wafurahie kwenda kupeleka mazao yao *NFRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mizani imelalamikiwa sana, Mheshimiwa Waziri Bashe alitueleza kwamba wameanzisha mfumo mchakato wa manunuzi wa kununua *digital*, ile mizani ya kisasa ambayo itakuwa *centralized* nchi nzima, hata aliyekuwa Makao Makuu ya *NFRA* anaweza akajua kazi inayofanyika Mtowisa au Laela au Sumbawanga. Naomba mchakato wa mizani ya kisasa *(digitala)* uende haraka ili msimu tunaouanza kusiwe na mizani ya *analogy* ambayo imekuwa ikilalamikiwa sana na wakulima. Kwa hiyo nimeona niyaseme haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, leo sikuwa na mambo mengi, niongelee habari moja ya Bonde hilo hilo la Ziwa Rukwa, kuna gesi ya *helium,* tulikuwa na watafiti na walikuwa wanaendelea na utafiti wa gesi ya *helium*. Naomba nitoe habari njema sana, wameenda kufanya *laboratory test* imeonekana gesi inayopatikana Bonde la Ziwa Rukwa sehemu inayoitwa Kata ya Zimba ina ubora ambayo *concertation* yake ni 2.46% ambayo hakuna nchi yoyote duniani inayofikia.

Mheshimiwa Spika, ninayo rekodi ya *concertation* ya *helium* katika nchi mbalimbali duniani, nchi ya Quatar ni 0.05%, Algeria ni 0.19%, Russia ni 0.06%, USA ni 0.35%, Canada ni 0.10%, China ni 0.03%, Australia ni 0.03%, Poland ni 0.10%, Tanzania kwa upekee ndiyo *the top,* 2.4%. Hili ni jambo la kupongeza na hii fursa inabidi tuitumie kwa sababu inaenda kuongeza sana pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, utafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na hasa kwa kutamka jina langu vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitoe pongezi nyingi sana kwa Serikali nami nitasema hasa kwa upande wa elimu. Serikali imejitahidi sana kuboresha elimu katika ngazi zote. Sasa labda nijikite katika kutoa maoni; katika kuboresha huko

elimu, sasa hivi tuna suala kubwa sana la kuboresha mitaala, hii mitaala ambayo imepigiwa kelele sana katika siku za nyuma, sasa hivi kazi kubwa inafanywa kwenye hiyo mitaala. Sasa hivi watu wa mitaala wapo kwenye kazi ya kuandika vitabu na baadaye kusambaza vitabu.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lipo kwenye zile fedha za kutoa vitabu na kuvisambaza, naiomba sana Serikali, Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu na Dada yangu Mheshimiwa Jenista, fedha za kusambaza vitabu zipo TAMISEMI, sasa niombe hizo fedha zipelekwe *TIE* au zipelekwe Wizara ya Elimu, wao sasa wawakabidhi *TIE* ili waweze kusambaza hivyo vitabu. Ikiendelea hiyo fedha kubaki pale TAMISEMI itachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watu wa *TIE* wamekaa tu hawawezi kusambaza vitabu kwa sababu fedha bado hazijapelekwa, zipo TAMISEMI. TAMISEMI ina madudu mengi, si mabaya, yaani ina kazi nyingi mno. Sasa kuna kazi nyingine, afadhali wazitoe zifanyike kwenye Wizara husika. Suala la vitabu, suala la *TIE* lipo chini ya Wizara ya Elimu, sasa tuwaombe sana hizi Wizara ziwasiliane, watoe hizi fedha ziende haraka *TIE* ili waweze kukamilisha kazi ya vitabu na vitabu viweze kusambazwa, isije ikatokea sasa tukakwama kwenye suala zima la hiyo mitaala ambayo imeboreshwa.

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, suala la uboreshaji limepelekea kupata wanafunzi wengi sana wanaomaliza vyuo vikuu. Sasa tatizo lipo kwenye ajira. Mwenzangu Mheshimiwa Riziki amesema, hebu sasa Serikali ijipange tupate takwimu za wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu, *versus* wale wanaopata ajira kila mwaka ili tujue kwa kiasi gani tunakwenda. Je, kuna wanafunzi wanaoongezeka katika wale wanaopata ajira au tunakwama wapi? Wengi wanamaliza lakini ajira pia zionekane ili tukisoma tuseme aaa! Mwaka huu wanafunzi kadhaa wamepata ajira au wanafunzi kadhaa wamemaliza, lakini kadhaa wamepata ajira ili sekta zinazohusika na ajira, Mheshimiwa Waziri Deo aweze sasa kujipanga kusaidia hawa watoto wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye jambo lingine linalohusu Mwongozo wa Mwaka 2023. Huu mwongozo ulikuwa wa shule ya nyumbani kwa watoto wenye ulemavu mkubwa sana, tunaita watoto wenye *multiple disability*. Kulikuwa na mwongozo huu wa shule za nyumbani kwa kizungu wanasema *home schooling*. Nataka niulize Wizara au Serikali, hivi hili jambo ni kweli linatekelezwa? Wanafunzi wangapi ambao wapo majumbani kuanzia *primary* hadi vyuo vikuu wanafikiwa na hii *program* ya *home schooling* au tumeliweka tu?

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Kuna wanafunzi wengine angalau wapo kwenye shule hizi za mchanganyiko, wanapata elimu, lakini nahofia wale wenye *disability* kubwa sana wanatakiwa kwenda vyuo vikuu. Kama hii shule ya nyumbani imekwama haitekelezwi, hivi hawa wanafunzi kweli wataweza kufika vyuo vikuu? Sasa hapa nataka nijue, kwanza watuambie, ni wanafunzi wangapi mpaka leo wanapata hii elimu inayoitwa elimu ya nyumbani kutoka *primary* mpaka vyuo vikuu au tumeweka tu mwongozo upo pale lakini utekelezaji hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uboreshaji wa miundombinu katika vyuo vyetu na hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu. Wakienda kwenye vyuo vikuu vyote, leo nenda hata hiki Chuo Kikuu cha *UDOM* kutoka *college* moja mpaka *college* nyingine ni umbali mkubwa mno, sasa tunawasaidiaje hawa wanafunzi wenye ulemavu? Kwa nini tusiweke *shuttle* pale, wenye ulemavu wawe wanasafiri bure? Yaani anatoka *college* moja kwenda *college* nyingine, ni mbali mno. Ukienda hata kwenye zile ngazi zao wanazotembea na hizo *lab* mnazosema, zile ngazi nyingine zimepigwa rangi nyeusi, mtoto mwenye huoni hafifu anakanyaga ile ngazi anaiona kama moja, hivi tunafanya nini? Niiombe Serikali, ipite kwenye vyuo ikakague miundombinu, iangalie, ikae vizuri ili hao watoto wenye ulemavu wanapoingia vyuo vikuu, basi waweze kusoma vizuri ili wasipate tena changamoto ya hilo tatizo. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatoka wapi? Aah! jirani yake? Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mariam Mwinyi. Nyuma yako ni nani? Mheshimiwa Mariam Nyoka, leo umehama kiti?

**TAARIFA**

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasikiliza mchango wa Dkt. Thea Ntara pamoja na uchangiaji wake mzuri, naomba aongezee utolewaji wa elimu kwa watumishi waliopo vyuoni juu ya lugha za alama, nayo ni uboreshaji wa miundombinu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara unapokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nasema nakushukuru sana sana. Ni kweli tunahitaji watumishi wote wa vyuo vikuu wapewe elimu ya lugha ya alama, wanaweza kutumia hata hizi *foundation*, zipo zinazotoa elimu hiyo ya lugha ya alama ili kuwasaidia wanafunzi wale wote walio na tatizo la kutokusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye jambo lingine, haya mafunzo tunayoyasema pia yatasaidia sana sio tu kwa watumishi wa pale vyuo vikuu, hata sisi Wabunge tunahitaji hiyo elimu. Kuna *foundation* hapa inaitwa *Foundation for Disability* ipo hapa, walishatoa elimu hii kwa watu 200. Walitoa elimu *TRA*, wakatoa elimu kwenye *TCRA*, walitoa elimu kwa baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi, kwa hiyo wale wanaweza wakasaidia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza ikafanya, lakini na ile *foundation for disability* inaweza ikasaidia kutoa lugha ya alama. Hii lugha ya alama sasa hivi kwa wenzetu *is very international,* lakini sisi tunaiona tu kama ni ya watu wachache na ndiyo maana wanapotuongoza kwenye *TBC* tunaangalia pale, tunatumbua macho tu, ukiijua hii lugha ya alama inasaidia sana kuona kwamba hata ile meseji inayokwenda kwa wenzetu kumbe ni meseji ya ukweli, maana yake kama unaangalia tu unaweza ukaona tu kama unadanganywa, lakini ni vizuri wote tukaipata

lugha ya alama na sisi katika kuboresha mitaala tunaishauri Serikali, sasa hivi lugha ya alama iwe *compulsory* kwa walimu wote ili akimaliza iwe kama nchi za wenzetu kama South Afrika na Namibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, nimejiandaa baadaye tutakapokuja kwenye Wizara, hili jambo lisipofanyiwa kazi, nitashika shilingi. Nawaambia mapema Mheshimiwa Dada yangu Jenista, naomba mlifanyie kazi. Suala hili la mishahara ya wakuu wa vyuo nalisema leo ni mara ya nne. Kila nikisema mnasema sijui kama lipo kwenye meza ipi, sijui meza gani. Naomba hili suala Mheshimiwa Dada yangu kipenzi Jenista, lichukue hili sasa lifike mwisho. Hawa wakuu wa vyuo tunawaonea jamani, mtu anasimamia chuo mshahara wake ni sawa na yule *Lecturer* wa kawaida! Hili naomba lifanyiwe kazi ili tutakapokutana tena, sitaki kushika shilingi kwako kwa maana itakuwa balaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyowasilishwa kwetu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema chochote, nitumie nafasi hii sana kutoa shukrani zangu katika sehemu kuu tatu au nne. Kwanza, kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwenye nchi yetu. Kwa ziada nimpongeze sana kwa uteuzi alioufanya wa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na hasa kwa kuniletea mdogo wangu Hassan Bomboko, namkaribisha kwa sababu wakati anafika nilikuwa kwenye ziara za Kamati. Namtakia heri mdogo wangu Hashimu Abdala Komba kwa kufanya kazi nzuri Ubungo na sasa kaelekea Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Dada yangu Jenista Mhagama pamoja na

mdogo wangu Mheshimiwa Deo Ndejembi kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ofisi hii vizuri. Sisi tunaendelea kuwatakia kila la kheri na tutaendelea kuwapa ushirikiano unaotakiwa. Nawapongeza pia Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote wawili. Mwisho, pongezi zangu nyingi ziende kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaka yetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kweli kwa kazi ambayo anafanya ya kuratibu shughuli za Serikali, hatuna mashaka, hata wananchi wanaona kabisa kazi yake kubwa anayoifanya, akisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Biteko.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niseme katika maeneo machache. Suala la kwanza ni eneo la ardhi na hili nakumbusha tu, katika ukurasa wa 44 wa taarifa umezungumza juu ya urasimishaji lakini pia na utatuzi wa migogoro ya kiutawala ya ardhi. Hapa ndiyo ninapotaka kusema kidogo, niliwahi kusema hapa ndani, kwenye Jimbo la Kibamba upo mgogoro ambao wananchi wana sintomfahamu hadi leo. Eneo la Msumi ambalo linabeba eneo kubwa sana la Msumi, Tegeta A nzima, Madale na maeneo hayo makubwa, zaidi ya watu 70,000 kwa Majimbo mawili ya Kawe na Jimbo la Kibamba, hili ni lile Malolo *Farm*.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisema hapa ni shamba lenye hati 30139 lililotolewa tarehe Mosi Aprili, 1983, muda mrefu takribani miaka 40, lakini sasa leo wananchi ni wengi, zaidi ya 70,000, wamejenga nyumba bora lakini na nyumba pia za chini. Sasa natamani sana kuishauri Serikali, niliwahi kusema hapa imeanza kuanza michakato ya kuona jinsi gani wananchi hawa wanyonge wanaenda kusaidiwa kurasimishiwa makazi yao. Maana leo lile jambo letu la urasimishaji linakwama na wengi wakitaka wanaambiwa shamba la uvamizi, eneo la uvamizi au kiwanja cha uvamizi, sasa hii lugha si nzuri sana. Kwa hiyo, niwatake sana Serikali waendelee kuongeza kasi ili wananchi hawa waweze kuthaminishiwa ardhi ile na waweze kupata hati ili wajiinue kiuchumi. Hilo nilikuwa nimeona nilikumbushe tu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni mafuriko, mvua nyingi za *El-Nino* ambazo Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema, kwa kweli Dar es Salaam tunalia sana, niwape pole na maeneo

mengine ya Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani, lakini Dar es Salaam hali ni mbaya sana. Niseme tu, sehemu ndogo ya Jimbo langu kuna Mto Mpiji na Mto Mbezi, nyumba nyingi sana zinaanguka sasa hivi hasa Mto Mbezi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu taasisi za umma, Malamba Mawili shule ya Msingi Msigani, si muda mrefu yote inaharibika na tumeweka fedha nyingi za umma, lakini tunaenda Mbezi Louis pale Kibanda cha Mkaa, bonde limepanuka, nyumba zaidi ya 20 zenye hadhi zimebomoka na juzi nimetoka kuwatembelea wananchi pale, ni kilio kikubwa. Pia ukienda Shule ya Msingi Matosa pale Goba, niiombe Serikali yangu sikivu ya Awamu ya Sita, ya Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ichukue tahadhari kubwa kwenye hili. Serikali iende ikawaone wananchi hawa ambao wapo katika sintofahamu kubwa na ikifika sehemu inayofaa nje ya bajeti tunayoenda nayo ya 2024/2025, fedha maalum itengwe kwa ajili ya kushughulikia jambo hili katika maeneo yote kwenye nchi yetu, ili baada ya tathmini wananchi wetu waone kabisa kuwa kesho yao bado ipo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maeneo hayo nizungumzie kidogo kuhusu eneo la huduma za jamii ambalo lipo kwenye ukurasa wa 57 wa hotuba. Eneo hili ni maeneo mbalimbali, eneo la kwanza ni eneo la miundombinu. Niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita, kwa kweli lazima niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewatendea haki wananchi wa Jimbo la Kibamba, hawana sababu ya kutomlipa mwaka 2025 kwa kura zote. Nataka niwapitishe kidogo tu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho nimeingia pale, hakuna barabara yoyote ya zege wala ya lami. Leo nataka niwaambie na wewe ni shahidi, Barabara ya Msumi kuelekea Madale imeshapewa *DMDP,* kilomita 11. Makabe nzima unaenda Msumi yote hadi Madale siyo mchezo, haijawahi kutokea hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tegeta A - Goba inaenda mpaka Madale, kilomita 7.6, ndugu zangu sikilizeni haya, Msingwa – Kisaki - Kifuru tunaendelea nazo hadi sasa, hizo barabara za zege na wananchi wanaziona. Pia Gogoni – Kiluvya - Kawawa *Road,* kilomita mbili tayari ina lami na wananchi wanaziona na wanazitumia. Ziada sasa hivi tunavyoendelea, Matosa Njia Nne - Temboni kuelekea Barabara ya Njia Nane, kilomita tatu mkandarasi yupo *site*. Hizo ni barabara za lami, haijawahi kutokea. Ni wakati wa Mheshimiwa Mama Samia, tuna wakati wa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wao na Madiwani waliopo. Hii haijawahi kutokea kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia Kimara, Bonyokwa kwa Wabunge watatu, niwashukuru sana. Hapa naanza mimi Mheshimiwa Mtemvu, mwanzo pale Kimara Darajani, anafuata Mheshimiwa Kitila Mkumbo, anamaliza Dada yangu Mheshimiwa Bonnah, kilomita sita zimetolewa zote. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunakushukuru sana na wananchi wa Majimbo haya mawili Ubungo na Kibamba wanakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwenye hili, tunayo barabara sasa na kama Mbunge nitoe kipaumbele cha Jimbo la Kibamba. Barabara ya Victoria au tunaita Mbezi Shule kwa Yusufu kwenda Mpiji Magohe kilometa 9.5. Serikali nawaomba sana, wameniahidi mwaka huu ndiyo wataiingiza kwenye bajeti baada ya usanifu wa kina na upembuzi yakinifu kukamilika. Wananchi wa Jimbo lile wanataka kusikia sasa na kesho kutwa wakati nitakapokuwa nachangia Wizara ya Ujenzi, wanaitamka hii kwa ukamilifu wake. Kilometa 9.5 ndiyo kipaumbele cha kwanza cha Jimbo la Kibamba. Naishukuru sana Serikali ya Awamu hii ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika huduma za jamii kuna eneo la maji, siwezi kuacha kusema, miaka yangu mitatu humu ndani, nimeingia humu nalia, nazungumzia maji asilimia 25 hadi 30 tu ndani ya Jimbo la Kibamba. Leo nataka niseme ukweli, tumeshafikisha 87% hadi 90%. Ni kwa nini? Ili tukamilishe maji Jimbo la Kibamba ilikuwa yafanyike mambo matatu. Tanki la kwanza Tegeta A lenye ujazo wa lita 5,000,000, nimeliomba humu na

limeshajengwa na maji yapo. Tanki la pili, Mshikamano Mbezi lita 6,000,000, fedha za UVIKO bilioni 4.8 tayari limejengwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la tatu la jana, ni kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Aweso, amekuja tumesaini mkataba wa milioni 42 kutoka Benki ya Dunia linajengwa Bangulo kule Ilala kwa ajili ya *Southern part of Dar es Salaam,* hapa ndiyo umekamilisha, nidai nini? Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa namshukuru Mheshimiwa Rais. Lililobaki kwenye hili naomba sana utandawazi au wanasema *distribution*, wapeleke mabomba tumalize, vyanzo vya maji vipo. Kaka yangu Mheshimiwa Aweso amefanya kazi kubwa, wananchi wa Kibamba wanamshukuru sana na tupelekee salamu kwa Mheshimiwa Rais, kwa kweli wametusaidia sana kwa kuwatua akinamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye eneo la maji. Leo vifaa vya maji tunavyo na hatuna shida kwenye hili, tunakamilisha na wakandarasi wanamaliza. Tuwaombe maeneo mawili. Eneo la kwanza ni Bwawa la Kidunda ambalo linaendelea, zaidi ya shilingi bilioni 320 zinaelekezwa pale. Kwa sasa taarifa inasema 17%, naomba tuongeze juhudi. Mwakani mwezi Juni tunatarajia kumaliza, hiki ndicho chanzo kitakachotusaidia tuwe na *sustainability* ya kupata maji kwa nyakati zote katika maeneo yetu ya pembezoni ya kusini, *peri urban*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni Mto Rufiji Bwawa la Mwalimu Nyerere. Wamesema jana, swali la Mheshimiwa Mwambe, amelijibu vizuri juu ya kuendelea na tathmini. Niombe hiyo tathmini wanayoimaliza tuendelee nayo, pia ilete maji maeneo ya mijini ili Ruvu peke yake juu na chini zitusaidie watu wa mwanzoni hapa ili tuweze kufanikisha hii 95%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua taarifa bado au muda wangu bado ni mzuri. Kwa kumalizia kutoa shukrani, niende eneo la mwisho katika suala la elimu, kazi imefanyika sana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake ameshanijengea shule sita za sekondari na ile maalum ya shilingi 4,000,000,000, ameshaniletea *VETA* ya Wilaya, nitake nini tena? Zaidi ni kusema

naunga mkono hoja, bajeti hizi zipite vizuri na tumwombee kila la heri Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mawaziri wanaomsaidia, Mungu awape umri mrefu.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana siku ya leo. Nitataja baadhi ya majina ya Wabunge ambao tutaanza nao tutakaporejea tena ambao ni Mheshimiwa Athipas Zeno Mgungusi, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Nicholaus George Ngasa na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda unavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache, kuna tangazo lililokuwa limetoka kwa ajili ya kukutana kwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, ukumbi wa Msekwa saa saba, sasa itakuwa saa tisa kamili badala ya saa saba.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wameingia Bungeni baada ya kuwa wageni wameshatangazwa:-

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni 208 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni Wanamaombi kutoka madhehebu mbalimbambali ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa wakiongozwa na Askofu Dkt. Peter Rashid Aboubakar ambaye ni mwanzilishi na Mkurugenzi Taifa wa Taasisi ya Kumwombea Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake. Pia ameongozana na Askofu Dkt. Daniel Kwilemba Kwiyeya kutoka Zanzibar. Wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 62 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni marafiki zake aliosoma nao kidato cha tano na sita katika Shule ya Sekondari Lufilyo, Busekelo kule Tukuyu, Mbeya na wanafunzi aliosoma nao Sayansi ya Siasa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2012. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni wetu waliokuja baada ya kuwatangaza wale wa mwanzo.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Mheshimiwa Kasim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametuandalia Iftar maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge. Iftar hii itafanyika katika viwanja vya Bunge leo Ijumaa saa 12.30 jioni. Mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge sisi na watumishi tutaelekea kwenye viwanja vyetu vya Iftar kwa hisani ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *Inshallah Allah* amjaze, ahsante sana. Hilo tangazo ni muhimu, hapa amemalizia Katibu wa Bunge kwamba hii ni bila kukosa. Imeandikwa hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mbio za Bunge *Marathon,* zitakazofanyika tarehe 13 Aprili, 2024. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, maandalizi yanaendelea vizuri, lakini anawakumbusha tuwashirikishe wananchi kwenye Majimbo yetu kwa maana ya kupeleka matangazo kuhusu mbio hizi hasa kwa kuzingatia umuhimu wake kwamba inakusudiwa kujenga Shule ya Sekondari ya Wavulana kwa ajili ya kidato cha tano na cha sita.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tuwahimize wananchi wetu kushiriki, lakini pia anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, wale ambao watakuwa wakijisajili kama makundi kwa maana ya watu zaidi ya kumi, watapata punguzo la ile ada ya kujiandikisha kwa 10%. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa maandalizi anawakumbusha hilo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 alasiri leo.

*(Saa 7.06 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Ahmed Pathan na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Nimesimama leo kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu moja tu kubwa. Malinyi tuna changamoto nyingi, lakini hasa za mafuriko na changamoto ya barabara. Jambo letu hili linahusiana na takribani Wizara tatu hadi nne, kwa maana ya TAMISEMI *(TARURA)*, Wizara ya Ujenzi *(TANROADS)* na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira (Idara au Kurugenzi ya Mazingira – *NEMC*).

Mheshimiwa Spika, sisi Malinyi mpaka hivi ninavyozungumza kuna changamoto kubwa, athari za mafuriko zimekuwa kubwa sana lakini kasi ya kupeleka habari hizi mitandaoni ni ndogo sana. Ni kwamba hatufanyi sehemu kubwa kuonesha ukubwa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba shida zetu ni kubwa kuliko kile kidogo ambacho mnakiona mitandaoni. Pengine watu wanaweza wakachukulia kama kuna jambo dogo au pengine hakuna shida sana. Tunafahamu mafuriko mwaka huu, kwa maana ya *El-Nino* imezunguka nchi nzima. Kila mahali kumeathirika, lakini kiwango cha athari kinatofautiana. Malinyi tumeathirika sana.

Mheshimiwa Spika, tangu vurugu hizi za mvua zimeanza, mpaka leo niseme tu kwamba watu wa Malinyi tumepoteza wananchi zaidi ya 14, wamefariki kwa ajili ya maji ya mafuriko. Nyumba zaidi ya 100 zimebomoka na nyumba zaidi ya 147 zimeingiliwa na maji. Kwa hiyo, wananchi zaidi ya 400 hadi 500 hawana mahali pa kukaa. Wengine wanajibanza kwa ndugu, wengine wanaona namna ya kukaa na bado hatujasaidika wala kuwasaidia. Kwa hiyo, binafsi kama Mbunge na wenzangu Serikali ya Wilaya tunakosa ufumbuzi wa haraka juu ya jambo hili, hivyo tukasema basi nije nizungumze kuweza kuhitaji msaada wa Serikali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu hili jambo hasa la maafa linahusu Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, hivi ninavyozungumza, sasa hivi Malinyi hapaingiliki. Magari kutoka Dar es Salaam, Morogoro, Ifakara na kwingineko hayawezi kuingia Malinyi. Ni zaidi ya wiki tatu sasa magari yanakwama, tunahangaika. Wenzetu wa *TANROADS* wanakuja wanafanya kidogo magari yanapita siku moja mbili, kesho yanakatika tena, kesho kutwa barabara zinakatika tena. Kwa hiyo, mpaka hivi ninavyozungumza Malinyi hapafikiki.

Mheshimiwa Spika, pia sehemu ya Malinyi Mjini katika Tarafa za Mtimbira na Malinyi yenyewe sehemu kubwa barabara za mitaani za *TARURA* zimekatika. Maji yapo usawa wa kiunoni mpaka kifuani. Kwa hiyo, barabara zimekatika, vijiji na vijiji hakuna mawasiliano. Kata ya Itete ambayo ni mwanzo kabisa wa wilaya kwenda pembeni Madababadaba hakupitiki. Kutoka Itete, hii njia ya kwenda Ipera Asilia hakupitiki, kutoka Ngwelanga kwenda Mkanga, hakupitiki. Kila mahali kuna changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, Malinyi tumeganda.

Mheshimiwa Spika, kama mliona kipindi fulani wiki iliyopita kuna picha ilikuwa inaenea mitandaoni ikionesha Hospitali ya Wilaya ilikuwa na maji yamejaa, halikadhalika hata ofisi za Serikali kwenye jengo la halmashauri maji yemezunguka. Kwa hiyo, mpaka hivi ninavyozungumza, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Malinyi na timu yake wanapaswa kwenda kazini kwa kutumia mtumbwi ndipo wakaingie ofisini. Kwa hiyo, wananchi hawapati

huduma. Baadhi ya shule tumezifunga, Shule ya Msingi Kiwale na nyingine zimefungwa kwa sababu shule nazo zimejaa maji. Kimsingi Malinyi imesimama, hakuna ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, gharama za maisha zimekuwa kubwa sana kutokana na ugumu wa kusafirisha bidhaa kutoka Ifakara na Dar es Salaam. Gharama zimekuwa kubwa, maisha yanakuwa magumu, lakini haionekani kwa sababu pengine hatuweki sana mitandaoni, lakini athari ni kubwa kuliko ambavyo inaonekana.

Mheshimiwa Spika, naomba tu, pamoja na Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa, atoe kipaumbele kwa Malinyi ili tuangaliwe kwa jicho la kipekee. Nadhani mnafahamu huu ni mwaka wa tatu sasa au wa nne, kila nikisimama hapa Bungeni nazungumzia changamoto ya barabara za Malinyi, hata kabla ya *El-Nino* ya mwaka huu haijaja. Kila mwaka nasimama kuzungumzia shida ya Barabara ya Malinyi kwamba magari hayapiti. Kwa hiyo, wakati wengine kuna unafuu, wako vizuri, sisi tumekuwa tukiendelea kulia.

Mheshimiwa Spika, *imagine* mwaka huu tatizo hili ni kwa nchi nzima, Malinyi ina hali gani? Kwa hiyo, sina namna nyingine ya kuonesha au kuifanya Serikali labda waone kwa ukaribu kwamba tuna shida kwa ukubwa huo, lakini naomba tu ichukuliwe kwa maneno machache kwamba hali ya Malinyi ni mbaya, magari hayaingii na kila kitu kimesimama. Kwa hiyo, tunaomba sana msaada wa haraka wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, nashukuru wote tulipata taarifa jana kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwamba kwa upande wa *TANROADS* tumepata hela kidogo, shilingi bilioni moja. Nashukuru. Hata hivyo, ni kwa ajili ya marekebisho madogo madogo. Hata hiyo haiwezi kutibu ukubwa wa tatizo la barabara zetu hizi za *TANROADS* ambazo ni takribani kilometa 200 ambako sehemu nyingi kuna mashimo na hali ni mbaya zaidi. Kwa hiyo, uhitaji ni pesa nyingi kuliko hizi ambazo nimezitaja. Siwezi kujua *exactly figure* ni kiasi gani, lakini barabara za *TARURA* ndiyo tumepewa shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kushirikiana na wenzangu, tumeandaa andiko kwa ajili ya dharura, lakini tumepata shilingi milioni 200 tu kama wiki mbili zilizopita, ilhali uhitaji ni zaidi ya shilingi bilioni tatu. Nafahamu kwamba Serikali kipato chake ni kidogo na pengine Serikali inahangaika, inajitahidi ku-*balance* kila mahali kidogo kidogo lakini katika uwiano ni lazima baadhi ya majimbo yaangaliwe kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwe wakweli kwamba unapogawanya kila jimbo lipate kiasi fulani, sidhani kama ni sawa sawa, tunatofautiana kiwango. Leo hii Dodoma Mjini hapa ambapo wote tunaishi, tuko hapa tunaona mafuriko haya hayawezi kufanana na ya Liwale, Malinyi na sehemu nyingine. Kwa hiyo, sisemi kwamba ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde asisaidiwe, sizungumzii hivyo, lakini uhalisia ndiyo uko hivyo. Kinondoni na Ubungo haiwezi kufanana na huko kwenye mikoa mingine, lakini Bonde la Kilombelo, Mlimba wale majirani zangu, Ifakara, Malinyi na Ulanga, yote hali ni mbaya zaidi na hatuwezi kufanana na maeneo mengine ya mjini yenye lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niikumbushe Serikali na nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtupe kipaumbele majimbo ya vijijini hasa ambayo hayana lami. Kukiwa na mafuriko kwenye wilaya ambazo zina lami, maana yake athari kubwa pale ni kwamba matairi ya gari yataloa tu kwenye lami, lakini ambapo hakuna lami maana yake gari itashikiliwa, haliwezi kutembea na haliwezi kwenda mbele. Kwa hiyo, vitu kama hivi lazima kuwe na *consideration*. Ukiacha mafuriko kuwa makubwa sana pengine na kusababisha magari kuweza kusombwa hata kwenye lami, lakini kwenye ile hali ya kawaida sisi wa vijijini tuna hali ngumu zaidi, na huoni kama jambo hili linakuwa *considered* na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba pengine unisaidie kusema au pengine unishauri kitu cha ziada cha kufanya, lakini naamini kila anayehusika na jambo hili, kama vile *TARURA* na *TANROADS* wanafahamu. Taarifa nimefikisha kila mahali kwa namna yoyote ambayo nimeweza, lakini bado hatujasaidiwa. Bahati mbaya zaidi bado hatujatembelewa, kwa hiyo, watu wa

Malinyi wanasubiri. Kunapotokea mafuriko kama haya, tunaona taarifa ya habari maeneo mengine viongozi wako kule na kule, kwa hiyo, sisi ikoje? Inaonekana tuna unafuu, au umuhimu wetu pengine ni mdogo, au kuwa pembezoni sana! Tupo wilaya ya mwisho katika Mkoa wa Morogoro ambako ni karibu na Ruvuma. Kila mtu anajiuliza maswali, hakuna namna.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku hata mimi kama Mbunge kwenye nafsi yangu najisikia na kujiona ninaonekana kama mzembe, hata wananchi wanaweza kudhani kwamba Mbunge wao hawasaidii, lakini uwezo wangu unani-*limit* kwenye kutoa taarifa Serikalini, ndilo jambo ambalo ninapaswa niseme na kukumbushia, lakini *the rest* ni jambo la Serikali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ananisikia, nakuomba mzee wangu kipekee uwasaidie watu wa Malinyi. Sina namna nyingine ya kufanya ili mweze kutusikia, lakini mwelewe maneno machache kwamba Malinyi tuna changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna namna mbili kuhusu shida zetu. Suala la kwanza ni barabara kutopitika. Ni kwamba sehemu kubwa nyakati za kiangazi wakandarasi wanavyofanya marekebisho wanaweka vifusi vya tope ambavyo ndivyo vinavyosababisha tunasa, lakini ukiweka vifusi vizito vya mawe na changarawe kutakuwa na unafuu mkubwa. Kwa hiyo, kuanzia Ifakara, Lupilo mpaka kufika Malinyi, *issue* kubwa ni kutokana na barabara kuwekwa matope wakati wa matengenezo, na leo ndiyo inatugharimu.

Mheshimiwa Spika, upande wa Malinyi Mjini na kata za jirani ambazo nimesema athari kubwa inatokana na Mto Furuwa. Tuna mto mkubwa pale Malinyi Mjini hauna kina, umejaa mchanga, hauna kingo kwa sababu kingo zake zimeharibika. Kwa hiyo, muda mwingine hata mvua isiponyesha Malinyi, ikinyesha jirani kwenye maeneo ya Ulanga na Mahenge, Malinyi maji yanajaa mitaani ilhali hata mvua haijanyesha. Kwa hiyo, Mto Furuwa ndiyo unaotusumbua na ndiyo unaopaswa utafutiwe suluhisho la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita, mwaka 2021 tulikuwa tunapata fedha za dharura. Nimekuwa naomba kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mara nyingi nimekuwa nikisaidiwa kwa kupewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara za *TARURA* na *TANROADS*. Mwaka 2022 tulikuwa tunapata shilingi bilioni moja hadi moja na nusu kwa ajili ya kutibu changamoto za barabara za *TANROADS* zinazotokana na Mto Furuwa, na mwaka huu tena tumepata fedha kidogo ili kutibu changamoto za barabara kutokana na Mto Furuwa. Sasa ukiunganisha hizo hela za dharura za miaka minne, zingetosha kudhibiti Mto Furuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita nilikwenda kule, akiwamo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira aliuona Mto Furuwa na watu wa *NEMC* wamekwenda wameuona, na watu wa Bonde wako kule, wanasema tu kuwa wataufanyia kazi, huku wakiwa na maandiko, michakato na wanachakata mpaka milele. Hatuwezi kusaidiwa mpaka hivi ninavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aongee na Mawaziri wake au aone kinachowezekana ili tusaidiwe watu wa Malinyi ili Mto Furuwa udhibitiwe. Najua *TANROADS* hawawezi kuweka bajeti ya Mto Furuwa kwa sababu atapata *auditing query* kwamba hili siyo jambo lao, hali kadhalika *TARURA* wataambiwa hili siyo jambo lao, kwa nini wameweka hela? Sasa kuna maana gani ilhali unajua kabisa shida ni sehemu fulani halafu unachelewa kujiandaa kuja kutibu dharura ya chanzo ambacho kinafahamika na Serikali ni moja? Kwa hiyo, wakati mwingine sielewi, sijui nifanyeje? Kuna wakati unapata hasira, naona kama tunapuuzwa. Kimsingi tunahitaji sana kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mto Furuwa wanaweza kuchukua Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Makamu wa Rais, Mazingira na wengine, unganisheni nguvu ili tuka-*deal* na Mto Furuwa. Hili litakuwa suluhisho la kudumu kwa watu wa Malinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ninavyokwambia hakuna kijiji ambacho kinafikika, kila mtu ameganda sehemu yake. Sasa tunapaswa kufanya nini? Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na unanisikia, sina maneno mapya ya kuzungumza kushawishi, naomba yatoshe haya kueleweka kwamba tunahitaji kusaidiwa sana. Hatulazimiki ku-*post* sana kwenye mitandao ili mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Ahmed Pathan. Atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai kwa kuweza kuwepo Bungeni hapa na kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nimpe pongezi zake nyingi sana Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake ambazo anazifanya. Tumeona kazi kubwa alizozifanya ndani ya miaka mitatu aliyokuwepo mama huyu. Ameboresha maeneo ya elimu, vituo vya afya, zahanati, hospitali, vifaa mbalimbali, mambo ya maji na mambo mengine mengi. Kwa kweli tunatakiwa tumpe pongezi zake za dhati Mheshimiwa mama yetu Samia Suluhu Hassan wa kazi kubwa alizofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninampa pongezi Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri Mkuu na ofisi yako kwa kazi nzuri mnayoifanya na kwa kutuandalia bajeti nzuri ambayo ina sura ambayo inaonekana inakwenda kumkomboa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaongelea sehemu chache kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, kwenye ile bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna mahali wameandika kuhusu Mkakati bora wa kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama; tunakubaliana na usemi huu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajua Serikali yetu inataka sisi tuwe salama, lakini nina ombi moja, na ninajua hili ni janga la kitaifa, lakini kwenye janga hilo la kitaifa kuna sehemu limezidi mno.

Mheshimiwa Spika, kuna hawa wanyama wanaitwa tembo. Tembo wamekuwa ni janga la kitaifa. Hali itakayotokea Mkoa wa Lindi kwenye maeneo ya Mchinga, Liwale, Nachingwea na Kilwa ni njaa kubwa sana. Mnyama huyu tembo kwanza anaua sana watu kule kwetu, watu wengi namepoteza maisha sana. Pia mnyama huyu ana akili sana, kwa sababu anajua kabisa sasa hivi mazao fulani yako tayari, anakuja. Makundi makubwa ya tembo wanakuja kula mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali iliyoko huko wilayani ni mbaya sana. Hakuna mahindi, mbaazi, korosho, karanga, hakuna kitu chochote. Wanakuja kundi kubwa; wanaweza wakaja 100 au 50. Wakivuruga shambani masaa mawili, hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala ukiliongelea hapa inaonekana kama ni suala la kawaida sana, lakini hili suala ukienda *site* hali ni mbaya sana. Mimi nilikuwa huko mwezi uliopita, nilikwenda eneo moja Nachingwea linaitwa Nditi kuwapa pole wale wahanga waliofikwa na majanga hayo ya tembo. Ilipofika saa kumi tukaambiwa sasa hivi ndiyo mida yao kwa hiyo inabidi muondoke haraka haraka. Tuliondoka mbio. Tumefika njiani eneo ambalo ni baya, gari liliharibika. Tukaambiwa hapa jinsi ya kutengeneza hii gari lazima mshuke chini, na hakukuwa na nyumba. Wakati huo huo tunaambiwa hapa ndiyo njia yao. Hebu fikirieni kwanza hiyo hali. Nilianza kuumwa na kuchanganyikiwa, hali ni mbaya. Kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu akatujalia tukatengeneza gari, tukaanza safari ya kuondoka huku tunapishana nao njiani. Hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hali hii huku tunaweka mkakati wa kuhakikisha tunaboresha maisha ya Watanzania. Tutaboreshaje? Watu hawaendi kwenye shughuli zao, watu wanashindwa kwenda mashambani, na hata wakienda wakilima

mazao yote yanaliwa na tembo. Maendeleo yatapatikana kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maoni yangu. Japo kila siku masuala yangu ni hayo hayo, nitandelea kuongea. Sitaki kwenda kinyume na Serikali, wala kinyume na maliasili lakini naomba nitoe ushauri tena kwa mara ya nne kama siyo ya tano, kwamba hawa wanyama inaonekana wako wengi mno kutuzidi sisi watu. Naomba sana hawa wanyama wavunwe ili wapungue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nilishaliongelea sana. Tunaomba nchi iweke mkakati wa kuweka *solar electric fence* kwenye maeneo haya yanayozungukwa na mbuga za wanyama. Tunajua gharama za *solar electric fence* lakini kwa kuwa hili ni suala la muda mrefu na mipango ya nchi, sidhani kama inaweza kushindikana. Sasa hivi tumeweza kuweka umeme wa *REA* kila kijiji, sehemu nyingi tumeweka umeme wa *REA*, tunashindwa nini kuwa na wazo hili la kuweka *solar electric fence? Solar electric fence* itawekwa kwenye maeneo yale tu ambayo kuna mwingiliano ambapo tunajua ndiyo njia ya wale wanyama. Huko *site* hali ni mbaya sana. Tunaomba sana mtusaidie katika hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitaongelea suala la kuporomoka kwa bei ya korosho. Hali ni mbaya hata kwa sehemu zile ambazo bado hawa wanyama hawajaingia. Kuna korosho kidogo lakini hakuna maslahi kwani kwa sasa hivi tozo zimekuwa ni nyingi sana. Mkulima anapata shida, analima kwa shida, na kwa bidii kubwa, lakini matokeo yake hela anayokuja kuipata baada ya makato mengi, inasikitisha sana. Mkulima hawezi kuendelea. Wananchi wetu wengi sasa hivi wameacha kulima korosho, mashamba yana mapori mengi. Hebu tuangalie hizi tozo tulizoziweka, tujaribu kuzipitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kingine, tukiangalia masoko ya nje, mbona korosho bado ina bei kubwa? Ukiangalia kuna kati ya dola sita mpaka 11 kwa kilo moja, lakini inakuwaje mkulima wa Tanzania anashindwa hata kupata dola moja akishauza kilo moja ya korosho? Hii siyo haki. Hatuwatendei haki wakulima wetu na

kwa mtindo huu hatuwezi tukabadilisha maisha ya Mtanzania. Kila siku Mtanzania atazidi kwenda chini, kudidimia na kuwa na hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye uchakavu wa miundombinu ya barabara. Inajulikana kwamba kutokana na mvua zilizonyesha barabara nyingi ni mbovu, lakini kuna zile barabara za *EPC+F* ambazo tumesaini mkataba mwaka 2023 tarehe 16 mwezi wa Kumi. Sasa hivi kuna mkanganyiko huko majimboni, kila mtu ana jibu lake kwenye hiyo wizara.

Mheshimiwa Spika, niseme ukweli, ukimwuliza namba moja, anakwambia hivi, ukimuuliza mtu namba mbili anakwambia vingine. Huko mitaani hali ni mbaya, tunaomba tupate jibu moja na tunaomba tusaidiwe. Zile barabara ambazo zimesainiwa kwa *EPC+F* tupewe jibu kama inawezekana au haiwezekani, na kama zinaanza tupate jibu kwenye Bunge hili la Bajeti. Huko kuna utata, wananchi wetu wamechanganyikiwa, wamekaa wahajielewi. Tunaomba sana kwenye hili tusaidiwe na Wizara ya Ujenzi itupatie jibu kuhusu barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kilio cha wavuvi. Kwenye bajeti hii inaonesha kwamba wavuvi wanatakiwa kuwekewa mazingira safi ya vitendea kazi, maisha mazuri na kadhalika, lakini ni tofauti na hali ilivyo. Sisi Wabunge ambao tupo kwenye maeneo ya wavuvi, kwenye bahari, maziwa na mito tunaona, na wengi wataniunga mkono hapa, Sheria za Uvuvi nyingi zimekuwa mbaya, haziko rafiki na wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania tutakuwa tunafuga samaki lakini sio wavuvi wala sio wala Samaki. Samaki zitakuwa zinaliwa na nchi za wenzetu kwa sababu Sheria na Kanuni zilizowekwa nyingine ni kandamizi, siyo rafiki, ni ngumu sana. Naomba sheria na taratibu zilizowekwa kwenye Wizara ya Uvuvi kwa ajili ya uvuvi zibadilishwe na zirekebishwe. Naomba sana, mtoe mwanga kwa wavuvi wengine, waje hapa watoe maoni yao, tuyachukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie bajeti hii ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/2025. Kwanza nianze na shukrani. Mama Samia Suluhu Hassan kalitendea haki sana Jimbo la Tabora Kaskazini, tunamshukuru sana na tunampongeza sana. Naomba nitaje baadhi ya mambo au miradi aliyotupa Mama Samia. Katika miaka mitatu hii ya kipindi chake, tumejenga majengo ya Halmashauri ambayo hayakuwepo, pamoja na ukumbi wa mikutano. Vile vile tumejenga Hospitali ya Wilaya, tumejenga Vituo vya Afya vitatu, tumejenga shule mbili za sekondari, tumejenga shule mpya moja ya shule ya msingi na kukarabati madarasa, tuna maji ya Ziwa Victoria katika vijiji 58, tuna umeme katika vijiji vyote vya Tabora Kaskazini, tumejengewa barabara, tumejenga Kituo cha *VETA* na bado tunasoma elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya siyo madogo kwa jimbo moja ambalo limepata jumla ya shilingi bilioni 55.6 katika kipindi cha miaka mitatu. Tunamshukuru sana Mama Samia na tunakupongeza sana. Tumeona mama huyu ni mwenye utu, upendo na ulinzi kwa Jimbo letu la Tabora Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuyataja mambo ambayo nataka nichangie katika bajeti ya Waziri Mkuu. Upo Mfuko wa Vijana ambao Serikali iliweka katika fungu la 65 ili kusaidia vijana kama mfuko wa maendeleo. Kila mwaka mfuko huu unaweka shilingi bilioni moja, lakini hadi kufikia tarehe 22 Machi, mwaka huu 2024 hata senti tano haijatoka kwenda kwa vijana, na hili siyo jambo zuri. Vilevile uko mfuko kwa ajili ya kuendeleza Machinga, nao umewekewa bilioni moja, lakini mpaka kufikia tarehe 22 hakuna hata senti ambayo imekwenda kwa Machinga

kuwasaidia, matokeo yake hakuna chochote kwa Machinga na wanazidi kuhangaika kutafuta uwezeshwaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *SDL* (tozo ya maendeleo ya ujuzi). Serikali iliweka makubaliano na waajiri kwamba theluthi moja ya hela yote inayokusanywa kutoka kwa waajiri ambayo wanawakata wafanyakazi kupeleka kwenye elimu ya kati, kwa mfano, mpaka 2021/2022 walikusanya shilingi bilioni 251 kama theluthi moja, lakini wamepeleka asilimia ndogo sana, yaani shilingi bilioni saba tu. Hii inafanya Serikali ishindwe kufikia malengo yake ya kufundisha vijana 47,000 kwa mwaka na kushusha idadi hiyo mpaka vijana 12,000 tu. Serikali ilijipangia kufundisha vijana 681, lakini lengo hili halifikiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Machinga, miaka miwili Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya Machinga, lakini hela hizo haziendi. Mwaka 2022/2023 waliweka shilingi bilioni 22 na mwaka 2023/2024 waliweka shilingi bilioni 18 lakini hela hizo hazikwenda mpaka leo. Vijana ndiyo nguvu ya Taifa na wasipoandaliwa na kuwezeshwa hawawezi kwenda popote. Tunaitaka Serikali itimize wajibu wake wa kusema itawasaidia vijana hao, itawawezesha, ili juhudi zao za kujitegemea ziweze kuwa na mpango mzuri.

Mheshimiwa Spika, liko suala la ahadi za viongozi. Viongozi wakitembelea kwenye maeneo yetu sisi Wabunge, wanatoa ahadi. Ahadi hizi viongozi wa kitaifa wakiondoka inakuwa mzigo kwa Wabunge. Nina mfano kwenye jimbo langu ambako kumekuwa na ahadi kubwa sana ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Usagari na ahadi hii iliwekwa na viongozi watatu. Kwanza, Mheshimiwa Rais, Marehemu Mkapa, baadaye Mheshimiwa Marehemu Dkt. Magufuli na sasa hivi Mheshimiwa Dkt. Samia ameweka ahadi ya kujenga kituo hicho, lakini sasa ni miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri wa Fedha ajaribu sana kulifanyia kazi jambo hili kwa kweli haipendezi. Sisi tunadharauliwa kule, hata sielewi, kwa sababu, kujenga kituo kwa ahadi ya viongozi wa juu namna hii, ni nini kinatokea? Mbunge akipita kule wanamwuliza, vipi Mheshimiwa Mbunge, kile kituo

chetu? Nakosa majibu kwa sababu nami sipati majibu huku. Suala hili siyo geni humu Bungeni, liko kwenye vikao vya siri, nimesema jamani Mheshimiwa Waziri wa Fedha hawezi kupata! Maana tumejenga wenyewe kwa gharama ya karibu shilingi milioni 100, hatuwezi kupata hela za kumalizia kituo hiki? Nikaseme nini kwa wananchi kule ninapokwenda? Wakiniuliza kituo chetu, niseme nini mimi kama Mbunge wao walinituma? Nawaomba sana mwaka huu tujaribu kuweka fedha za kumalizia Kituo hicho cha Benjamin Mkapa kilichopo katika Kata ya Usagari, Kijiji cha Migungumao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za afya jimboni kwangu, nina kata 19 umbali wa kilometa 300 kutoka mwanzo wa jimbo mpaka mwisho wa jimbo. Kuna kata tatu zina zahanati tu, tunajenga Kituo cha Afya kwa nguvu zetu wenyewe, yaani kwa fedha za mfukoni za Mbunge, hela za jimbo na nguvu za wananchi, tumeshindwa kumalizia ili kituo kile kiweze kuhudumia kata tatu. Kata ya Shitage yenyewe, Kata ya Igulungu na Kata ya Bukumbi. Naomba sana katika bajeti hii kituo hicho kijengwe. Vilevile Kata ya Ufuluma wananchi ni wengi sana, lakini hakuna Kituo cha Afya, wanatibiwa mbali kabisa. Jimbo zima likiwa hata na vituo vitano itanisaidia sana kusemea siasa yetu. Wananchi wanataka afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha tumbaku. Zao la tumbaku sasa kwa Wabunge wote mjue kwamba ndilo linaloingizia fedha za kigeni kuliko zao lolote hapa Tanzania. Tulikuwa na korosho karibu shilingi bilioni 200, lakini sehemu kubwa sasa tumbaku ndiyo inaingiza hela nyingi za kigeni, lakini hatupati ruzuku ya mbolea kwa ajili ya kilimo cha tumbaku. Tunaomba Serikali ilipe kipaumbele zao hili ili liendelee kuwa chanzo cha kupata hela za kigeni. Zao la tumbaku ni muhimu sana katika Jimbo la Tabora Kaskazini au Mkoa wa Tabora, kwa sababu asilimia 60 ya tumbaku yote inalimwa huko.

Mheshimiwa Spika, pia ule mgao wa mitungi ya gesi ni muhimu sana ikapendelewa Tabora Kaskazini, Uyui kwa sababu ndipo tumbaku inalimwa na inakaushwa kwa kutumia kuni. Tunataka tuondoe kuni katika kupikia. Tukipunguza kuni ikabakia

ya kuchomea tumbaku tu na kupikia tutumie gesi, tutapunguza tatizo mara chungu nzima. Sasa hivi wananchi wanakata miti kukaushia tumbaku. Kwa mabani ya kisasa, imepungua kidogo, lakini wanakata miti kwa ajili ya mkaa wa kupikia. Eneo hili lenye matumizi mawili ya kukaushia tumbaku na kupikia, hebu tuondoe kupikia tuwape gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, atakapogawa majiko, aipendelee Tabora Kaskazini ambako tunalima tumbaku ili tuondoe tatizo la kupikia, tuwape gesi, tubakie na kazi ya kukata tumbaku kwa sababu inaingiza fedha za kigeni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi huku kwenye mambo mengine ya kitaifa. Liko suala la Sheria za Kazi na Ajira; Sheria za Kazi na Ajira zinazotumika sasa zimepitwa na wakati. Nalisema mara ya pili hili. Naomba pia sheria hizi zifanyiwe uboreshajia, uhuishwaji wa usasa, tunaongelea mambo ya teknolojia sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, dakika moja malizia.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tunatumia suala la akili bandia lakini sheria hizi zilishindwa kutusaidia wakati ule wa *Corona*. Wananchi, wafanyakazi na waajiri walienda kugombana kwa sababu sheria haikutusaidia. Tunaomba sheria hii ihuishwe, iboreshwe na iwe ya kisasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus…

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, atafuatiwa na Mheshimiwa John Pallangyo na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu jioni hii. Nitatoa baadhi ya mapendekezo na maoni yangu ambayo naamini Serikali itayaweka katika utekelezaji wake na yatakuwa na mchango.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi madhubuti anayoifanya kwa ajili ya Taifa letu la Tanzania. Mheshimiwa Rais amekuwa imara sana na kwa takribani miaka mitatu tumeona mabadiliko makubwa sana kwenye majimbo yetu, Halmashauri zetu na Wilaya zetu, kiasi kwamba hata ukifuatilia mijadala ya Waheshimiwa Wabunge, utakubaliana nami taarifa kuhusu changamoto zimepungua kwa kiasi kikubwa sana kama ukifanya tathmini ya haraka haraka. Maana yake kazi kubwa imefanyika, na hii ni kazi ya kujitoa kwa ajili ya Taifa. Tunamwombea Mheshimiwa Rais wetu, Mwenyezi Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika usimamizi wa Shughuli za Serikali, pamoja na Waziri wake Jenista Mhagama kwa ajili ya uratibu, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ummy pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Patrobass Katambi na Mheshimiwa Ndalichako ambaye alitoka hivi karibuni. Walikuwa pamoja wanashirikiana katika ofisi hii, wanafanya kazi nzuri sana ya uendeshaji wa shughuli za Serikali na Uratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, duniani kote ukifuatilia au ukifanya utafiti, mafanikio ya taasisi yoyote yanatokana na mambo makubwa matatu. Jambo la kwanza ni rasilimali watu *(personnel/human resource),* jambo la pili ni rasilimali fedha na tatu, ni mifumo ya uendeshaji (maamuzi, sheria, kanuni na miongozo). Kuna maeneo ambayo napenda kushauri na kama Taifa tunaweza tukayaangalia ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, tumefanya mambo mengi sana, lakini kuna baadhi ya maeneo bado tunahitajia kufanya maamuzi. Jambo la kwanza, naweza nikaanza kusema kwa mfano kwenye

ujenzi wa barabara za vijijini na mijini, nijielekeze upande wa *TARURA*. Kama tunakumbuka, tulipokuja Bunge la Januari, tulikuwa na *concern* kubwa sana kuhusu barabara za dharura nyingi zilikatika kutokana na mvua zinazoendelea nchini, lakini Mheshimiwa Rais, alitoa maelekezo zitoke fedha za dharura kwenda kutatua changamoto hii, lakini fedha zimetoka mpaka leo Wakandarasi bado hawajaingia *site*. Ukiuliza changamoto ni nini, unaambiwa tatizo ni mchakato wa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, sasa naishauri Serikali, kwa kuwa mnatoa fedha kwa mfumo wa dharura, hatuhitaji mchakato wa manunuzi wa miezi mitatu au minne kupata Mkandarasi. Unapotoa fedha za dharura, mtengeneze mfumo wa dharura wa kutatua tatizo. Kwa mfano, jimboni kwangu Igunga mvua zimenyesha mwezi wa Kumi na Moja, barabara imekatika halafu zinatoka fedha za dharura mwezi Januari, mpaka leo mwezi wa Nne hakuna Mkandarasi. Ukiuliza unaambiwa mchakato wa manunuzi unaendelea. Hiyo fedha ya dharura Mheshimiwa Rais ameidhinisha ya nini? Tuangalie mfumo mpya kama tulivyofanya kwenye fedha za *Rapid* za *Covid*, tulipata fedha na tukazitumia haraka haraka kwa mfumo wa dharura, madarasa yalijengwa ndani ya miezi miwili, miezi mitatu tulimaliza tatizo la madarasa nchini *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, hili mliangalie, mtasaidia sana uendeshaji katika Taifa letu kwa sababu hizi barabara ndiyo mihimili ya Uchumi kwa usafirishaji wa mazao, usafirishaji wa rasilimali mbalimbali kutoka eneo moja kwenda lingine. Sasa unapotoa pesa ya dharura mwezi wa kwanza, barabara inakuja kujengwa mwezi wa Sita, na mvua zimeisha imeshaingia kiangazi, maana yake udharura pale haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali waliangalie hili. Kwa mfano pale Igunga, nina barabara moja ambayo inaenda kwenye eneo moja kubwa sana la uzalishaji linaitwa Igunga, Mwanzugi, Lugugu, Itumba. Kule tuna *skim* kubwa za kilimo cha umwagiliaji tumepewa fedha ya dharura, Mheshimiwa Rais ametupatia fedha, lakini mpaka leo hatujapata

Mkandarasi. Ukiuliza, unaambiwa mchakato wa manunuzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ijaribu kusaidiana na TAMISEMI, lakini pia na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iangalie hili jambo twende na mfumo mpya ambao utakuwa unasaidia fedha zinapotoka katika mfumo wa dharura, basi zitoe suluhisho kwa mfumo wa dharura.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kwenye barabara kuna fedha tulipewa jimboni kwetu mwaka 2023, zinaitwa *bottleneck*, ambazo tuliambiwa zitatoka *World Bank*, toka mwezi wa Kumi, mpaka leo haijafika na yenyewe mchakato wa manunuzi unaendelea. Mwisho wa siku hata wananchi hawaoni tija ya hizi fedha. Tunapopewa fedha na zikishakuwa *open* au *disclosed* maana yake michakato ifanyike. Kama changamoto ni Sheria ya Manunuzi, basi Wizara ya Fedha walete hiyo sheria tuipitishe, tubadilishe maeneo ambayo tunaona yanatukwamisha. Mwisho wa siku tutakuwa tunafanya kitu kimoja kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, kwenye suala la barabara naomba waende kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine napenda kushauri hapa kwenye suala la barabara, tunaomba kabisa TAMISEMI kupitia *TARURA*, waongeze usimamizi katika haya masuala ya barabara. Hizi barabara wanapofanya ukaguzi hakikisha wanazikagua vizuri na zinapopokelewa, basi zipokelewe zikiwa zimekamilika kwa viwango vinavyotakiwa. TAMISEMI ni Wizara kubwa na kila jimbo lina Barabara, sasa *TARURA* kusipokuwa na usimamizi mzuri, maana yake tutatengenezewa barabara ambayo ikinyesha mvua ya kwanza, ikaja ya pili nchi nzima hakuna barabara za vijijini, tunaanza kuwekeza upya kama ambavyo alikuwa anasema Mbunge wa Malinyi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulieleza jioni hii ni ujenzi wa masoko na stendi za mabasi. Kumekuwa na *trend* ambapo tukiongea kuhusu ujenzi wa masoko na stendi za mabasi mara kwa mara, majibu ambayo tumekuwa tukipata kutoka Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni kwamba

halmashauri ziandike maandiko, zipeleke, halafu wenyewe wataangalia na kufanyia tathmini na kuamua.

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi ulitoa maelekezo kwa Waziri wa Uwekezaji, kwamba angalau nchi nzima waje na *model* mpya inayoelezeka na kutekelezeka, siyo kila sehemu lazima tujenge soko au stendi ya shilingi bilioni mbili au tatu. Kwa mfano, kwenye madarasa tulikuja na *model* ya darasa moja, yale ambayo ni maboma, tumeenda kuyamaliza kwa shilingi milioni 20. Tuweke mfumo wa kutengeneza stendi angalau hata za shilingi milioni 300 au 400 ambazo karibia kila halmashauri itakuwa na stendi inayoeleweka na itakuwa pembezoni mwa barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Igunga tuna changamoto kubwa. Tuna stendi yetu ya mabasi iko takribani kilometa tatu kutoka *highway,* hata mabasi sasa hivi yanakataa kwenda, biashara za wananchi zinakufa, lakini ukiangalia kwa mfano pale Kibaha, wamejenga stendi tu ya *highway* au Chalinze pale hata basi kuingia halioni usumbufu. Sasa, TAMISEMI mtusaidie hili, mweke *model* nzuri ya kujenga stendi za gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwani stendi ni nini? Si suala la kukwangua eneo na kuweka miundombinu kama vyoo pale na huduma ya maji, maisha yanaendelea! Anayetaka kujenga kibanda cha biashara anapewa mkataba na halmashauri, anajenga. Tukiwa na mawazo ya kujenga stendi ya shilingi bilioni nne, hatutaweza kwenda. Kila mtu atakuwa anaomba stendi, kila mtu anaomba soko humu ndani, halafu mwisho wa siku tunaambiwa tupeleke maandiko na utekelezaji utakuwa hakuna. Kwa hiyo, naomba hilo tulifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano Igunga pale, tuna soko letu kubwa ambalo lina uchumi mkubwa sana, tunaliita Kariakoo ya Igunga. Kila jumatano mali zinafunguliwa, wafanyabiashara kutoka Singida, Shinyanga na Simiyu wanakuja. Tunahitaji ujenzi wa hili soko. Sasa kama TAMISEMI wakitoa mwongozo, mnaweza mkatusaidia tukapata soko la bei nafuu ambalo linaweza likajengwa na tukaweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la tatu ambalo napenda kulichangia jioni hii ni ujenzi wa vyoo kwenye shule za msingi na shule za sekondari. Namshukuru Mheshimiwa Rais, juzi kule Igunga tumepata shilingi 1,100,000,000 kwenye halmashauri yetu na kwenye jimbo langu takribani shilingi 800,000,000 zimebaki kwa ajili ya ujenzi wa vyoo kwenye shule za sekondari na madarasa.

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri kitu kimoja ambacho pia umeshawahi kukitolea maelekezo. Itakuwa ni fedheha kwa Taifa letu tukiendelea kuongelea changamoto za vyoo humu kwenye Bunge. Ushauri wangu ni kwamba, kila Mkurugenzi wa Halmashauri anapoteuliwa, apewe mwongozo wa kwenda kutatua changamoto za ujenzi wa vyoo kwenye halmashauri yake. Hii imekaaje? Kwa mfano, leo mimi nilipopata hizi fedha kwenye kata moja, inaenda milioni 14, inajenga seti ya vyoo nane ambapo unaweza ukamwambia Mkurugenzi kila mwaka ahakikishe anajenga vyoo 10 kwa shule za msingi na vyoo 10 shule za sekondari. Kwa takribani shilingi milioni 280, hakuna Mkurugenzi ambaye atashindwa kupata fedha hizo kujenga vyoo.

Mheshimiwa Spika, hata vyoo navyo tuanze kusubiri fedha kutoka TAMISEMI, Serikali Kuu! Hili nawashauri kama Serikali mliangalie, hawa watu mnaowateua mwape *KP eyes,* vitu vya kwenda kufanya vya kutoa matokeo. Watumie fedha za halmashauri, vinginevyo kila kitu tukiwa tunasaidiwa kutoka Serikali Kuu maana yake ni mnawa-*incapacitate*, watakuwa hawana hata akili za kufikiria kukusanya fedha za mapato. Wapeni msaada kwamba nenda kila mwaka jenga vyoo 20; vyoo 10 kwa sekondari na 10 kwa shule za msingi na ndiyo unawapima kwa matokeo, ndiyo tutakavyokwenda. Kwa hiyo mambo mengine tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mlitupa maelekezo tujenge vituo vya afya kwa mapato ya ndani, sisi pale Igunga tumejenga Kituo cha Nang'a kwa shilingi milioni 400. Leo tutashindwa kujenga vyoo kama mkazo na mwongozo utakaotoka huku Serikalini! Naamini kwamba suala ni kuthubutu na tutaamua na tutaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ambalo ningependa kuchangia ni uhamisho wa watumishi wa umma. Sasa hivi kuna mfumo unaosimamia uhamisho wa watumishi wa umma. Hiki nacho kimekuwa ni kichaka kingine cha urasimu. Sasa hivi mtu kila akiomba anaambiwa ipo kwenye mfumo subiri. Hapa niwashauri Serikali, kama tunavyotoa mikopo kwenye elimu ya juu, kuna kipindi tunasema *window period,* yaani kile kipindi cha kutoa mikopo, wekeni utaratibu Serikalini labda mwezi wa Tisa mpaka mwezi wa Kumi ni kipindi tunachoshughulikia uhamisho. Anayetaka uhamisho kama anauingiza kwenye mfumo na aseme.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wapo tayari kuhama kwa kujigharamia, siyo mpaka walipwe zile hela za Serikali, lakini watu wanabaki wanafanya maombi kwenye mfumo hawajibiwi chochote. Matokeo yake kila mtu anakutumia nakala zake alizotuma, Mheshimiwa Mbunge, naomba barua zangu hizo hapo, nisukumie kwa Katibu Mkuu wa Utumishi ili niweze kupata uhamisho. Tubadilike, tuendeshe Serikali kisasa ili tuweze kurahisisha mambo. *Stress* nyingine mnazowapa watumishi wa umma ndiyo maana hata wanakuwa wazembe kufikiria kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa kuna changamoto nyingine. Kuna mwajiri ambaye ni Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, kuna Msimamizi wa Kazi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hapa unakuta mtu ameomba kwa Mkurugenzi wake Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mkurugenzi wake, uhamisho umeruhusiwa, unaenda Utumishi kwa Katibu Mkuu unazuiwa. *Stress* nyingine mnatengeneza kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikalini wakubaliane, waweke *modality* nzuri ya kushughulikia huu uhamisho wa watumishi wa umma ili tuwaondolee *stress*. Mtu anayetaka kujihamisha kwa hiyari, yupo tayari, hahitaji kulipwa, mwache aende. Halafu kama unasema kwamba ni *switching,* weka utaratibu mzuri. Ukitangaza mtu ata-*switch* na huyu anapatikana, lakini sasa hivi maombi yanakaa *pending* na imeshakuwa ni kigezo, kila ukiwasiliana

unaambiwa lipo kwenye mfumo, subiri yafanyiwe kazi na mfumo haufunguliwi wala hata hayafanyii kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano, ningependa kuchangia jioni hii ni sekta ya mifugo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa malizia dakika moja. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimalizie na Sekta ya Mifugo. Igunga ni moja ya wilaya yenye mifugo mingi sana na tuna mnada mkubwa wa pili kwa Tanzania ukiacha ule wa Pugu. Tunaomba Wizara ya Mifugo, tunahitaji kujenga majosho na mabirika ya kunyweshea maji mifugo ya wafugaji wetu. Tunaomba watupe kipaumbele kwa kuwa wanachukua fedha za ule mnada wetu, basi *in return* watusaidie kututengea fedha za kutengeneza mabirika na majosho kwa ajili ya kuweza ku-*facilitate* mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwa kifupi kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imesomwa wiki hii. Kwanza nianze kuungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametupa siku ya leo tumekutana kwenye Bunge hili, Mkutano wa Kumi na Tano ambao naona kama utakuwa ni mkutano wa mwisho kwetu na tunajadili bajeti. Pia itakuwa ni bajeti ya mwisho kuijadili na kuipitisha na kushuhudia utelekezaji wake. Bajeti inayokuja hatutaona utelekezaji wake, nadhani mmenielewa. Bajeti hii tunajadili, tunaipitisha na tutashuhudia utekelezaji wake. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, watu wanapata wasiwasi kwamba kama umeamua wewe kutokurudi humu Bungeni, wengine wana mpango wa kurudi. Ndiyo changamoto hiyo unayoiona.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, msiogope Waheshimiwa Wabunge. Jitahidini, sawa sawa kabisa mkuu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli, kwa miaka mitatu ambayo amekuwa ofisini amefanya kazi kubwa sana kwa Watanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba yake imesheheni taarifa muhimu ya tulikotoka, tulipo na tunakokwenda. Pia nampongeza kwa kazi kubwa ambayo anafanya, ni pamoja na wasaidizi wake Waheshimiwa Mawaziri ambao ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waheshimiwa Manaibu Waziri, wote wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za pongezi, sasa nizungumze kidogo kuhusu mambo ambayo yananikera kule jimboni. Nitazungumzia habari ya maji. Tunaishukuru sana Serikali, imetupatia shilingi bilioni 14 jimboni ambazo zimetekeleza miradi ya maji. Japo kwa mwaka uliopita fedha zilikuja kwa kusuasua sana, lakini pamoja na fedha hizo, jimbo langu upande wa Mashariki bado watu wana matatizo makubwa ya maji, bado watu wanafuata maji kwa kutumia punda. Tatizo ni kwamba, maji yanayotoka Mto Meru ni mengi, lakini yana *fluoride* nyingi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tumekuwa na bahati kwamba kuna Mkorea mmoja amesema atakuja kutusaidia kuondoa ile *fluoride.* Alishaanza kujenga kituo Kata ya Kilori kwa ajili ya kufunza vijana. Pia katuletea mashine za kuondoa *fluoride* kwenye maji. Aliomba tumpatie eneo la kujenga tanki kubwa la lita milioni 24 *up stream* kwa ajili ya kukusanya maji ambayo yana *fluoride* yachujwe halafu yasambaziwe kwa wananchi wa Kata zile za Ngarenanyuki, Ngabobo, Maruvango, King'ori, Malula hadi Majengo. Ombi langu ni kwamba, apewe ushirikiano na Serikali. Kwa hiyo, nitaomba kwa kipindi hiki wakati tunajadili bajeti, nikae na Mheshimiwa Waziri wa Maji tuweze kujadili hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali imefanya kazi kubwa kwenye barabara, imejenga barabara za lami. Niseme kwamba, barabara za lami huwa siyo kwamba zinachochea tu maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi, lakini pia zinapendezesha sana mazingira kule zinakopita. Nimebahatika kupita *privately,* lakini pia nikiwa kwenye kamati, Serikali imefanya kazi kubwa sana, lakini bado tuko nyuma ya malengo. Kwenye ilani tuliahidi kilomita 8,000, bado tuko nyuma na kule jimboni kwangu hali ndiyo mbaya kabisa. Hali ni mbaya na bahati mbaya jimbo langu kwa sehemu kubwa ni mlima. Kwa hiyo, wananchi wengi wapo kwenye mteremko *(slopes)*, barabara za udongo hazifai.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Serikali imejitahidi, kuna barabara ya lami wameanza kujenga ambayo inaanzia Sangisi - Ndoombo kupitia Akeri, na mwaka 2022/2023 tuliweza kujenga mita 900. Mwaka huu wa fedha, tumepata fedha za kujenga mita 700, ile barabara ina kilometa kama nane. Kwa *speed* hiyo mpaka imalizike, kule ambako itakuwa imeshafanyika kazi vizuri, tutakuwa tumeanza kuona *potholes*. Kwa hiyo, naomba nguvu iongezeke zaidi katika kutoa fedha kwani mwaka huu zilichelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni ahadi. Kuna mwenzangu alisema kwamba ahadi za Viongozi Wakuu hazitekelezwi. Kule Meru pia kuna ahadi ya Barabara ya King'ori iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. Magufuli. Mwaka 2020 nilikuwa naimba kila leo, lakini hadi leo hakuna kilichofanyika. Niseme kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo Kiongozi wa Shughuli za Serikali, hili lichukuliwe ili hii barabara ianze kujengwa, hata tukipata kilomita 10 kabla ya mwaka kesho itarudisha imani kwa wananchi. Kule wanatuona sisi ni watu wa ovyo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niseme kwamba, kwa mazingira ya kijiografia Jimbo la Arumeru Mashariki kwa kweli tunahitaji *share* kubwa kwenye sekta ya Barabara. Mazingira yale siyo rafiki, kwa hiyo, tunahitaji fedha zaidi. Angalau kwa bajeti ambayo tunapata sasa hivi ingefanywa mara mbili. *TARURA* wanajitahidi, lakini shida

ni *resources.* Kwa hiyo, hili naomba liangaliwe, tuongezewe *resources*.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali, imefanya kazi kubwa sana. Tumepata madarasa mengi kwenye sekta ya elimu, madarasa mengi yamejengwa, lakini ukarabati wa shule kongwe unasuasua. Naomba *speed* iongezeke katika kukarabati shule hizi. Kuna shule inaitwa Ndovwa Sekondari, nilikwenda kuitembelea nikakuta ina walimu watano, wanafunzi 500, lakini miundombinu ilikuwa imeharibika mno. Pia nadhani walimu waliondoka kwa sababu mazingira yamekuwa magumu. Kwa hiyo, tunaomba *speed* ya ukarabati wa shule kongwe iongezeke. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele, au bado!

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, siyo shule moja ambayo imeharibika miundombinu yake, kule Meru kuna shule kama nne za mfano ambazo kwa kweli zinahitaji zifanyiwe kazi haraka sana. Labda nizitaje, Ndombo Sekondari, Urisho *Primary School* na Mareo. Hizi shule zimekaa vibaya hata, Kigogo aliziona akaanza kututukana kwenye mitandao akamsema *DC*, Mbunge, hata hawajui wanafanya nini! Sasa tusaidieni tusije tukaonekana ni watu wa ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, nakushukuru kwa muda ulionipa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa

Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake kumshukuru na kumpongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanyia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ina kurasa takribani 110. Hotuba hii ni hotuba nzuri na imebeba matumaini makubwa kwa Watanzania. Mheshimiwa Rais wetu anafanya kazi nzuri sana, ukisoma kwenye ukurasa wa 11 wa Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni dhahiri kwamba, miradi yote mikubwa ya kimkakati ya Taifa letu inakwenda vizuri sana. Hotuba hii imeeleza bayana kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mradi wa *SGR*, madaraja makubwa, viwanja vya ndege, barabara, bomba la mafuta na kadhalika. Miradi yote hii inakwenda vizuri na mingine imekamilika. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ukienda kwenye ukurasa wa 19 wa hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni dhahiri kwamba Serikali yetu pia imefanikiwa kudhibiti mfumko wa bei kutoka *digit* 4.8 mpaka 3.2. Haya ni mafanikio makubwa sana, lakini pia ukusanyaji wa mapato ukurasa ule wa 17, ni dhahiri kwamba, pia Mheshimiwa Rais na Serikali yake ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuendelea kukuza ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 4.7 mpaka asilimia 3.5. Haya ni mafanikio makubwa, na Taifa letu linazidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ukusanyaji wa kodi ambapo kulikuwa na kasumba huko nyuma ya kuvuja kwa mapato ya Serikali, lakini ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukusanyaji wa mapato ya Serikali umepanda kwa zaidi ya asilimia 10 ukilinganisha na mwaka 2022/2023. Tunapompongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri, haya ni sehemu tu ya mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maeneo machache. Kwanza nianze na eneo la kilimo. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu eneo la kilimo limesemwa kwenye ukurasa wa 26

mpaka wa 32. Kwa kuanza, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Wizara yake kwa ujumla kwa namna ambavyo kilimo kimeendelea kusonga mbele. Taarifa zinaonesha kwamba, Taifa letu kwa sasa halina uhaba wa chakula, tuna utoshelevu mkubwa wa chakula nchini. Haya ni mafanikio makubwa kwa Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, uniruhusu nitoe shukurani maalumu kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia kupita Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wananchi wa Jimbo la Lupembe wana imani kubwa na Serikali hii na wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo Lupembe kilimo kinakwenda vizuri. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2021 alikuja Mkoani Njombe kwenye Kongamano la Wakulima wa Chai, na kati ya maelekezo aliyoyatoa ilikuwa ni pamoja na kutafutwa kwa mwekezaji mpya wa kusaidia zao la chai Lupembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe taarifa ndani ya Bunge lako kwamba, mwekezaji wa yuko Lupembe, anawasaidia sana wananchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana na hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia jambo moja ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alionesha wasiwasi akiwa Mkoani Njombe, halijafanyiwa kazi, na hili ndiyo limekuwa ndiyo donda sugu la wakulima wa zao la chai nchini. Akiwa Njombe hiyo tarehe 10/03/2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu alionesha wasiwasi wake juu ya mwekezaji *DL* wa kiwanda cha chai *Ikanga Tea Factory* na alieleza kwenye hotuba yake kwamba, huyu mwekezaji kwenye nchi yao ya jirani anawalipa vizuri wakulima wao, lakini hapa nchini kwetu viwanda vyote vitatu alivyonunua vina hali mbaya. Hii ilikuwa ni kauli nzito ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na alieleza wasi wasi wake kwamba isije ikawa ni *sabotage*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeongea mara kadhaa ndani ya Bunge lako hili, mwekezaji huyu, *DL Company*, amechukua viwanda vyote vitatu vikubwa mkoani Njombe na tangu achukue viwanda hivi vilikuwa vikifanya kazi vizuri. Mashamba yalikuwa vizuri, leo havifanyi kazi. Kiwanda cha *Ikanga Tea Factory,* hivi

tunavyozungumza hakichukui chai kwa wakulima wa Lupembe, maana yake aliyotabiri Mheshimiwa Waziri Mkuu yamekwenda kutimia. Kwenye madeni ya chai ya wakulima wa Tanzania, *DL* peke yake anadaiwa zaidi ya asilimia 80 ya madai yote ya wakulima Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, kupitia Waziri wa Kilimo na Waziri Mkuu yuko hapa, ile kauli ya tarehe 10/03/2021 Njombe, Serikali ifuatilie. Ilikuwaje mwekezaji mmoja amechukua viwanda vyote muhimu na vimekufa havifanyi kazi wakati kwao viwanda vyake vinafanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, jana Mheshimiwa Mwakagenda pia alisema ndani ya Bunge lako Tukufu juu ya hali mbaya ya zao la chai kule Mkoani Mbeya, Rungwe na maeneo mengine. Zipo taarifa kwamba mwekezaji aliyeko kwenye haya maeneo ya Rungwe na kule Tanga naye anakusudia kufunga viwanda. Mwekezaji huyu anamiliki asilimia 30 ya mashamba yote ya chai nchini, maana yake akifunga viwanda zaidi ya asilimia 30, wakulima wa chai wataathirika nchini. Naiomba tena Serikali ikachunguze, mkataba wa kuuziwa viwanda hivi ulikuwa unasemaje kuhusu kuwasaidia wakulima wa Tanzania? *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa nia njema...

**SPIKA:** Mheshimiwa Swalle kuna taarifa kutoa kwa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**TAARIFA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anayezungumza anasema haki kabisa. Leo nimeongea na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, lakini pia kuna taarifa kwamba tarehe 30/03 ambapo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alitoa agizo la kwamba Mo (Mohamed Dewji) asifunge kununua chai Wilaya ya Rungwe, amesimamisha kazi tayari, na

barua watu wamepewa, wanazo mikononi, lakini kiwanda cha Tukuyu, Katumba, pia kimefungwa na wameanza kuuza mali za kiwanda. Kwa hiyo, hii hali kweli ni mbaya, tunaomba tulifanyie kazi tuone tunawasaidiaje wakulima wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Swalle, unaipokea faarifa hiyo?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Mwakagenda kwa heshima kubwa na ndiyo maana nasema Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu alifanya kazi nzuri na akatoa maelekezo. Ombi langu kwa Serikali, viwanda hivi vya chai ukafanyike uchunguzi, ni nini kinaendelea kwenye viwanda hivi?

Mheshimiwa Spika, hili ni Taifa, tunao wakulima wanapata shida kubwa kwenye kuchuma chai, lakini inaonekana kuna ajenda binafsi kwenye zao la chai nchini. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, mimi kama Mheshimiwa Mbunge pia najiuliza, Sheria ya Chai ya Mwaka 2010 imeeleza wazi kwamba mwekezaji akichukua chai ya wakulima awalipe siku 15 baada ya mwezi kwisha, ndani ya siku15, sheria iko wazi. Sheria imesema, asipolipa anatakiwa ashitakiwe, apigwe *fine* au kufungwa. Mwekezaji huyu *DL* ana miezi zaidi ya tisa halipi wakulima, hajawahi kuitwa Mahakamani, hajahojiwa popote.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Lupembe na wananchi wote, wakulima wa chai nchini, zao la chai nchini lisife, Serikali iingilie kati kunusuru hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo la pili kuhusu kilimo. Wananchi wetu pia wameitikia kuhusu jambo kubwa la kutumia pembejeo kwenye kilimo chao. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, ile mbolea ya ruzuku ya kilo 50 siyo wananchi wote wana uwezo wa kununua. Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, kwa kuwa wananchi wetu wengi hawana uwezo, ile mbolea tukaiweke kuwe pia na mfuko wa kilo tano, kilo 10 na

kadhalika ili wananchi wetu wenye uchumi wa chini nao waweze kumudu kununua hizo mbolea ambazo Mheshimiwa Rais ametoa ruzuku kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nihame niende kwenye eneo la ujenzi, ama usafirishaji ambayo ipo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 48 - 50. Kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista na Mawaziri wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wanaendelea kuyakabili maafa nchini kwetu. Nchi nzima kwa sasa inakabiliwa na maafa, lakini Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mawaziri wake wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kila mahali wanakwenda haraka na kuchukua hatua. Hapa tunapozungumza, Lupembe sasa hivi barabara yangu ya Kibena kwenda kule Lupembe kuna eneo la Ikombe limeharibika na wananchi wana hali mbaya, magari hayatembei. Naiomba Serikali itenge fedha zaidi za dharura kutatua changamoto ya barabara ya Kidegembye, Sehemu ya Mtonga – Lubela ili wananchi wetu waendelee kupita na maisha yao yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, nashukuru sana. Naunga mkono hoja hii, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyofanya kazi katika kuiongoza nchi hii na kuiletea maendeleo makubwa. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anavyoiongoza nchi yetu ya pili ya Zanzibar. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na tunawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kipekee kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote kwa namna ambavyo wamekuwa wakiratibu na kuisimamia Serikali, na kwa jinsi walivyokuja na hotuba nzuri na bajeti nzuri ambayo sisi wote leo tunaijadili ikiwemo Mfuko wa Bunge. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yanapimwa kwa kuangalia vigezo kadhaa na moja ya maeneo nitakayoyazungumzia, yapo kama manne, lakini nitazungumzia labda matatu. Eneo la kwanza ambalo tunaipima nchi kwa maendeleo ni eneo la viwanda. Eneo la viwanda ni kiashiria kikubwa sana katika maendeleo ya nchi na uchumi wa nchi. Sasa nchi yetu lazima iwe na mkakati wa kutosha kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda mama na viwanda vya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiachilia mbali viwanda mama, viwanda vya kuongeza thamani bado hatujavipa kipaumbele cha kutosha na ndiyo maana kama nchi tumekuwa tukipata matatizo makubwa na tutaendelea kupata matatizo. Wataalam wanasema, kama umeamua kuwa mzalishaji wa malighafi, maana yake umechagua kuwa maskini wa milele. Sasa nchi yetu hatuwezi kuendelea kuwa ni wazalishaji wa malighafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunazalisha pamba na tunaiuza kama malighafi, tunazalisha kahawa tunaiuza kama malighafi, tunazalisha korosho tunauza kama malighafi, tunazalisha chai tunauza kama malighafi, hii haitupeleki mahali pazuri. Kama nchi ni lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa na viwanda vya kuongeza thamani na kutengeneza bidhaa za mwisho, yaani *finished products*. Hapo ndiyo nchi itaona thamani na ndipo tutakuwa na uchumi mkubwa, uchumi himilivu na uchumi wenye manufaa na nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kila kitu tunaagiza nje. Hiki kitu siyo kizuri sana. Kwa kuwa, kwenye eneo la viwanda tunayo sera ya viwanda, ninaamini na ninadhani kuna haja ya Serikali kukaa

chini na kuangalia kwenye viwanda mama tunafanyaje? Viwanda vya kuongeza thamani tunafanyaje? Viwanda vya kuunganisha *(constructive industries)* tufanyeje? Hapo ndipo tutaweza kujenga uchumi imara na himilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo tunaliangalia kwenye maendeleo ya nchi ni biashara. Kwenye biashara tunazo biashara za ndani, biashara za nje na huduma zinazoendana na biashara. Sasa kwenye maeneo haya huduma zinazoendana na biashara tunaangalia mambo ya benki, mambo ya bima, mambo ya usafirishaji, masoko na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu iko *strategically located* na sisi sote tumekuwa tukiimba, maana yake nini? Maana yake fursa tulizonazo tunaweza tukazitumia na tukafanya biashara nzuri na nchi yetu ikaweza kupata mapato makubwa. Sasa, ukiangalia katika biashara za ndani hatujafanya vizuri, bado haturatibu vizuri. Biashara za nje bado hatufanyi vizuri, maana yake tumejikita zaidi katika kuuza malighafi kitu ambacho siyo kiashiria kizuri sana kwenye maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye hili eneo la huduma za biashara kwenye upande wa usafirishaji, kule kwetu sisi ni wazalishaji wakubwa na ni wakulima. Tunalima mazao ya kahawa kwa wingi, tunalima mazao ya chakula kwa wingi, lakini tuna tatizo la miundombinu ya kusafirisha. Kwa mfano, barabara ya kutoka Vwawa - London - Iganduka - Msia hadi Isalalo, ile barabara tumekuwa tukiimba kwa muda mrefu lakini bado ina changamoto. Tunayo barabara ya kutoka Ihanda kwenda Ipunga mpaka maeneo mengine bado barabara ile ni shida.

Mheshimiwa Spika, pia tunayo Barabara ya Vwawa – Nyimbili kwenda mpaka Ileje, zile barabara zote zinaenda kwenye maeneo ya uzalishaji. Kwa hiyo, naiomba Serikali iziangalie sana hizi barabara ili kuhakikisha mazao na bidhaa zinazozalishwa katika maeneo yale zinaweza kuchangia uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, hilo eneo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo nilitaka kusema ambalo tunaiangalia nchi ni namna huduma za jamii zinavyotolewa. Kwenye eneo la huduma za jamii, tunayo maeneo kama eneo la maji, eneo la elimu na masuala ya utawala bora. Ni wazi kabisa nchi yetu inafanya vizuri kwenye upande wa huduma za jamii, lakini kama nchi, ni lazima sasa tuangalie tunavyozigawa rasilimali. Kwenye viwanda tunapeleka kiasi gani? Kwenye biashara tunapeleka kiasi gani? Kwenye upande wa huduma za jamii tunapeleka kiasi gani ili tuweze kujenga rasilimali watu na tuijenge nchi iliyo nzuri?

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa katika nchi yetu ni suala la umaskini kwa Watanzania. Suala la ajira kwa Watanzania hivi sasa ni kubwa na haya matatizo hatuwezi kuondokana nayo mpaka tuwekeze vya kutosha kwenye viwanda, mpaka tuwekeze vya kutosha katika biashara, mpaka tuwekeze vya kutosha kwenye elimu, mpaka tuwekeze vya kutosha kwenye huduma za jamii. Tukiwekeza vya kutosha ndipo tutaweza kukabiliana na suala hili la ukosefu wa ajira, suala la umaskini na ndipo tutaweza kutoa mchango mkubwa katika kujenga uchumi ulio imara. Haya maeneo naamini ni muhimu sana katika kuiendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine katika hilo ambalo nataka kudokezea tu ni kuhusu watumishi. Watumishi ni moja ya walipa kodi. Katika maeneo ya biashara na viwanda wote watakuwa ni walipa kodi lakini watumishi wanalipa kodi. Ili watumishi waweze kulipa kodi na kodi iweze kupatikana kwa wingi ni lazima tuwaangalie katika maslahi yao, wapate mishahara mikubwa. Wakilipwa vizuri ndiyo kodi inakuwa kubwa na ndiyo wanaenda sasa kutumia hizo fedha kuwekeza, wanaenda kula maisha katika maeneo mbalimbali, hela zinatawanyika sasa, mambo yanakwenda kuwa mazuri. Wakiwa hawana fedha za kutosha hawawezi kutumia na uchumi hauwezi kuchangamka. Ili uchumi uchangamke, unahitaji watu ku-*spend* hela. Sasa ili u-*spend* hela, uwe nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, angalieni masilahi ya watumishi wa umma, angalieni masilahi ya watumishi

wa sekta binafsi, walipwe mishahara mizuri ndiyo watalipa kodi vizuri na ndipo uchumi wa nchi yetu utaweza kuchangamka vizuri. Hilo ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kuchangia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kuchangia linahusu mfumo na mwongozo wa utayarishaji wa mipango yetu pamoja na bajeti. Robert Smith mwaka 1996 alikuja na mwongozo wa kutayarisha bajeti ya Serikali Kuu. Katika kutayarisha huo mfumo, yeye alisema Serikali Kuu inahitaji kuwa na vyanzo hivi vya mapato, akaweka masuala ya kodi na kadhalika. Akaondoa bajeti za mashirika ya umma na taasisi zake zote, akasema hizo zote zisiingie kwenye bajeti kuu.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni nini? Matokeo yake nchi nyingi zika-*adopt* hiyo *modal*, zika-*adopt* hiyo *formula* sasa bajeti kuu inayokuja unakuta mashirika mengi ya Serikali na taasisi zake hazipo kwenye bajeti kuu. Mapato yote ambayo mashirika yanakusanya, iwe ni *TTCL,* iwe ni Bandari, iwe ni *TRC,* iwe ni shirika gani, mashirika yote bajeti zao haziji hapa Bungeni kwa sababu ya hiyo *modal* aliyoileta Robert Smith. Sasa nadhani umefika wakati Serikali ikae chini itathmini, je, ile *modal* ya mwaka 1996 bado ina umuhimu wa kuendelea kubaki kama ilivyo au kuna haja ya kuiangalia upya ile *modal* ili kusudi bajeti za mashirika ya umma ziweze kuwa ni sehemu ya bajeti kuu?

Mheshimiwa Spika, nimeangalia hata hii bajeti ambayo imeletwa hapo, kuna bajeti ya Serikali Kuu shilingi trilioni 33, Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.3, mashirika ya umma au gawio kutoka kwenye mashirika ya umma, hakuna, haijawekwa pale. Ukija misaada na mikopo shilingi trilioni 5.1, mikopo ya nje shilingi trilioni 9.6, inakuja bajeti ya shilingi trilioni 49, bajeti za mashirika ya umma

hazimo hapa, lakini mashirika hayo ya umma ndiyo yanatekeleza majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri wakati umefika katika zile *reforms* za Mheshimiwa Rais za mabadiliko aliyoyaleta, nashauri aliangalie na hili ili aweze kuleta mabadiliko kusudi bajeti za mashirika ya umma ziweze kuwa ni sehemu ya bajeti kuu na ziweze kutumika ipasavyo. Pia, Bunge lipate mamlaka kamili ya kuweza kupitisha, kuzisimamia na tuweze sasa kuishauri Serikali namna ya kuwa na matumizi bora ya hizo rasilimali za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hili jambo ni la muhimu na ninaamini Serikali italichambua, italitafakari na kuona namna bora itkavyoweza kuja na *model* mpya inayoendana na kasi na muda muafaka uliopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika bajeti hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayolifanyia Taifa hili kwa maendeleo ya Watanzania ambayo kwa kweli tunayaona. Mama tunakupongeza na tunakuombea afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote akiongozwa na dada yangu Mheshimiwa Jenista pale, kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya. Hongereni na tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia mambo makuu mawili. Maendeleo yote tunayoyafanya katika nchi hii au tunayopanga kuyafanya yatakuwa na tija kubwa kama kutakuwa na ustawi wa jamii kwa maana ya wananchi wetu kuwa katika hali ambayo ni bora na nzuri kiakili, kiafya na kiuchumi. Nasema hayo kwa sababu, sasa hivi katika jamii tuliyopo kuna ukatili mwingi na mkubwa kwa watoto na ndani ya familia. Utasikia mume kamuua mke, mke kamuua mume, utasikia mtoto kafanyiwa ukatili, utasikia huyu kamfanyia yule ukatili na kadhalika. Sasa hili ni jambo ambalo ni muhimu na lazima Serikali ione namna ya kuliingilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunajua kuna mikakati, kuna miongozo na vitu kama hivyo, hiyo pekee yake haitoshi kwa sababu, hii mikakati na miongozo ipo lakini bado tunaona kasi ya ukatili, masuala ya afya ya akili na mambo mengine ni tishio kwa Watanzania. Kwa hiyo, hayo yote yatakuwa na *impact* kama pia tukiliangalia jambo hili kwa ukaribu zaidi na kuliwekea mikakati kuhakikisha hawa maafisa maendeleo ya jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii tulionao katika maeneo yetu wanawezeshwa, wanaweza kuwasidia watu.

Mheshimiwa Spika, pia nafikiri tufikirie namna bora hata ya kuweka vituo. Tunajua kwenye jamii, watu wana msongo mwingi wa mawazo, watu wengine wanatafuta mahali tu aende apumue apate unafuu, aende aongee na nani, lakini tukiwa na *centers* ambazo zina wataalam, wabobezi mtu anaenda pale, kama ni mama, mke au mume, kila mtu ana nafasi ya kwenda kusema, kwa sababu pamoja na yote, kusema pia ni kupona. Asiposema maana yake ataendelea kuwa nalo na atapata shida.

Mheshimiwa Spika, pia hao watoto wanaofanyiwa ukatili ambao kila leo tunasikia, hivi watoto hawa wanapewa ushauri nasaha katika *level* gani na kwa kiwango gani? Je, baadaye wanafuatiliwa? Fikiria, labda mtoto wa darasa la pili au la tatu amefanyiwa ukatili mkubwa sana, hivi mtoto yule atarudi shule ile ile na atakutana na watoto wale wale ambao tayari wana taarifa kwamba mwenzao alifanyiwa ukatili ule? Alifanyiwa labda

kitendo kibaya, je, Serikali inamtazamaje mtoto huyu kuhakikisha kwamba anapewa ushauri nasaha na kubadilishiwa mazingira, hata kama ni ya kusoma, labda asisome pale asome shule nyingine? Hata kama atasoma pale pale, awe na ujasiri kwamba pamoja na kwamba nilipitia madhila fulani fulani lakini ninapoenda kukutana na wenzangu nami niendelee kujiona ni sehemu ya wale wanafunzi na ni sehemu ya ile jamii pamoja na hayo niliyopitia.

Mheshimiwa Spika, hiyo itafanikiwa kama mtoto huyu atatengenezewa mazingira ya ushauri nasaha kutoka kwa wataalam na Serikali ikaweka mkono wake, kama kuweka vituo vya kuhakikisha mtoto huyu tunamkomboa na kumsaidia, kwa sababu kwa kweli kuna tishio kubwa sana la ukatili, na ukisikia kama wewe ni mzazi, kwa kweli inatia uchungu kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, nafikiri hilo ni jambo muhimu sana, Serikali ilitazame kwa ukaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la afya; magonjwa yasiyoambukiza, na masuala ya utumiaji wa vitu ambavyo tunajua vina athari kubwa kwa baadaye katika miili yetu. Tunaona wanaeleza kabisa kwamba utumiaji wa vinywaji kama *energy drinks* kwa kiwango kikubwa ni hatari, ni mtu ambaye anaendelea kujitengenezea ugonjwa kwa miaka ijayo. Tunaona vijana wetu wanafanya vitu kama hivyo lakini tunafanyaje kudhibiti suala hili? Inawezekana ni biashara ya watu ndiyo, lakini ni kwa kiwango gani tunatoa elimu ili mtu ajue mimi ninapokunywa *energy drink* ninakunywa kwa kiwango gani ambacho kinatakiwa na *recommended* na wataalam? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lingine ni matumizi ya shisha. Shisha nayo imekuwa ni tishio. Kuna matumizi makubwa ya shisha. Sijui shisha ni Kiswahili sahihi au siyo sahihi! Ukienda kwenye kumbi za starehe, ukienda baa unakuta watoto wadogo wanatumia hizo shisha, lakini je, nini madhara yake? Hivi hatutengenezi wagonjwa watarajiwa wa baadaye? Naamini tunatengeneza wagonjwa watarajiwa wengi sana wa baadaye, lakini tunafanya nini? Nimesikia katika Afrika Mashariki, nafikiri ni Tanzania tu ndiyo shisha

inatumika. Sina uhakika kama nchi nyingine wanatumia, wamepiga marufuku, sisi tunafanya nini katika hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tufikirie, tunaandaa baadaye yetu, sasa kufikiria mzigo mkubwa, kuweka fedha nyingi kwenye sekta ya afya kwa sababu tunaenda kutibu watu wengi ambao wana magonjwa yasiyoambukiza ambayo ndiyo tishio kubwa na ndiyo ambayo yanasababisha vifo vingi sana vya wananchi hapa Tanzania kwa mujibu wa takwimu. Kwa hiyo, ni vyema sana hilo likachukuliwa na likatazamwa kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Tunafahamu kuna mifuko ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na hii mifuko mara nyingi huko nyuma tumeshauri namna ya kuiunganisha, nafikiri iko takribani 18. Tuunganishe hii mifuko. Pia tuna ile mikopo ambayo inatolewa katika halmashauri zetu, tuangalie ni namna gani tunawasaidia wananchi. Tunajua kuna benki ambazo zinatoa mikopo, kuna taasisi ambazo zimesajiliwa zinatoa mikopo, lakini kuna hao ambao sina hakika kama wamesajiliwa, lakini wanatoa mikopo ambayo baadaye ina athari kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, kuna hii mikopo ambayo inaitwa Kausha Damu, ina majina mengi, mengi sana. Hii mikopo imekuwa ni hatari na ni tishio. Hii mikopo kwanza ina riba kubwa, hii mikopo kama ni familia, inasambaratisha, hii mikopo kama mtu akichukua na hajakaa sawa sawa, hata yeye mwenyewe atajiua, tumeona matukio mbalimbali. Kama haitoshi, hata hapa juzi vyombo vya habari vimeripoti, baba mmoja huko Tarime amemuua mtoto ili apate fedha kwenye vile vikundi ili afanye marejesho kwenye hii mikopo, inasadikika hivyo. Sasa hii ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, kama tuna hii mifuko na kama tuna ile mikopo ambayo tunatoa katika halmashauri zetu, kwa nini tusifikirie kuja na mfuko mmoja au miwili kulingana na jiografia ya nchi yetu, Serikali ikaratibu kwa karibu, ikaweka fedha, ikatoa elimu kwa wananchi ili kuwafikia hao wajasiriamali wengi, hao akina mama, akina baba ambao kwa namna moja au nyingine wanatafuta hata angalau shilingi 50,000 waanzishe biashara ya

kuchoma mihogo kwenye maeneo yao au kutengeneza chapati kwenye wajipatie shilingi mia au mia mbili kwa siku. Kwa nini tusiwe na utaratibu huu? Tuwasaidie, kwa sababu kuna wananchi walio wengi kufika benki na kukidhi vigezo ambavyo benki inataka ili aweze kupata mkopo ni changamoto kubwa sana, na ni kitu ambacho hakiwezekani. Kwa hiyo, ni vizuri sana hili likatazamwe kupitia huu mfuko wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kuona namna iliyo bora kuifikia hii jamii ambayo inahitaji uwezeshaji kiuchumi, lakini kwa namna ambayo ni bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais, lakini kuna baadhi ya taasisi ambazo watu wameaminiwa, wamepewa fursa, lakini kuna ubadhirifu mkubwa na hii inaoneshwa kupitia Ripoti ya *CAG* na hata ukipitia taarifa ambazo zinakuja kwenye mitandao ambazo najua nyingine hazijakanushwa, inawezekana kuna ukweli. Kuna shida kubwa sana kwa baadhi ya watumishi wetu wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, mfano, pale Ngorongoro tunaona kuna *clip* inatembea, sijajua pale huwa kuna shida gani? Kuna shida kubwa sana na ninafikiri kila anayeletwa pale kuna tatizo. Tufike mahali sasa kuwepo na mfumo, kwa sababu hatuwezi kumpata malaika wa kumweka pale, kwa sababu inaonekana kila anayefika pale ni upigaji. Tuweke mfumo ambao yeyote atakayeenda pale, awe ni mtakatifu au awe ni shetani, mfumo utambana asiweze kuiba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Sekta ya Utalii, ambayo imeimarika baada ya *Covid*, wageni ni wengi na sekta imekua kwa kiasi kikubwa. Sekta hii ni muhimu kwa uchumi wa Taifa, lakini haya yanayotokana na matokeo ya utalii huu, yanaliwa na wachache. Watanzania wengi wakisikia haya, ni chuki, na wengi hawapendi kuyasikia haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mashirika yetu kwa mfano Ngorongoro na *TANAPA,* ripoti ya *CAG* imesema mara nyingi, tumeona kuna *clip* zinatembea kwenye mitandao kwamba watu wachache wanapiga hela nyingi mpaka unasikitika, unasema,

hivi ni kweli au ni hadithi! Nadhani Serikali ije na mfumo. Haya ni baadhi ya mashirika machache ambayo nimeyataja, lakini yapo mashirika mengi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Serikali ije na mfumo ambao utahakikisha tunabana na kudhibiti wizi wa fedha ambazo zinawekwa pale ili mwisho wa siku kila Mtanzania afaidike na rasilimali za nchi hii. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Jackson Kiswaga ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa utangulizi, nimetambua jambo moja kwamba binadamu kwa tabia yake anapenda kusifiwa, lakini anapenda pale unapoonesha shukurani. Nilikwenda mbali zaidi wakati fulani, nikakutana na Mchungaji mmoja akanikumbusha hata kwa maana ya sala yetu inayosema "Baba yetu Uliye Mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako ufike, utakalo lifanyike duniani kama mbinguni." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Baba na kumtukuza, ndiyo unamchomekea, utupatie leo mkate wetu au riziki yetu ya kila siku. Kwa hiyo, hata Mwenyezi Mungu mwenyewe anapenda kushukuriwa kwa kiasi hicho. Hata hivyo, ninyi mama zangu, mtoto anapokuwa mdogo, kadri anavyoanza kuonesha hatua utakuta mama anakapongeza kale katoto, kumbe ndiyo kanaendelea kuongeza hatua. Hiyo ni maumbile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hayo nami naomba nianze na shukurani. Namshukuru Mama Samia kwani pale kwetu Katavi kulikuwa na shida kubwa ya suala la uchujaji damu na nikilisema namaanisha. Wapigakura wangu wamehamia Mbeya, Dar es Salaam na Mwanza kwa ajili ya suala la uchuchaji damu kwa ajili ya tatizo la figo. Kwa nini wamehamia Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam? Kwa sababu kwa wiki wanachuja damu mara tatu, sasa hawawezi kukaa Mpanda. Wamekuja Mbeya

wameishia kukodi vyumba. Tatizo ni la kuchuja damu, lakini wameingia tatizo lingine mpaka la kukodi chumba.

Mheshimiwa Spika, Mama Samia Suluhu Hassan baada ya kuliona hilo, ameniletea fedha Mpanda, shilingi milioni 196 kwa kuanzia, kwa ajili ya kujenga chumba cha kusaidia wagonjwa wa uchuchaji wa damu. Nimelisema hilo, lakini nikasema ninaposhukuru ni ustaarabu wa kuomba tena. Ule mradi kwa ujumla wake ni shilingi milioni 400, lakini kwa kilio hiki alichoanza nacho Mama cha kuwajali wale wagonjwa, nilikuwa naomba twende mbali zaidi. Nashukuru sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo kama halitoshi, *scheme* ya umwagiliaji, maji ya Mwamkulu ambayo tumeletewa shilingi bilioni 31 na *point,* najua *scheme* ile kasi yake ni ndogo, lakini naomba wataalamu waliopo huko waongeze kasi. Tuna mradi wa *TACTIC* ulikuwa na shida kidogo, lakini sasa hivi wataalamu wamekuja kufanya utafiti pale, tuna kilometa 8.2 za lami kwa ajili ya ule Mji wa Mpanda. Naomba wataalam waandike kwa herufi kubwa, ni kilometa nane za Mji wa Mpanda. Hayo yote yananifanya nishukuru ukiachilia mbali miji 28, kwa maana ya tatizo la maji katika Mji wetu wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo naomba ni fidia kwa wananchi wa bwawa la Milala na kwa wananchi waliopisha ujenzi wa barabara kutoka Sitalike kuja mpaka Mpanda Mjini. Tunaomba sana fidia ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, najua tumezungumzia suala la biashara ya *carbon*. Biashara hii ni chanzo kikubwa cha mapato. Jana alizungumza mtu mwingine hapa, nami naomba nirudie. Biashara ya *carbon* ukiacha suala la mtu kati, tukienda moja kwa moja kwenye soko ni biashara kubwa sana. Tuachilie mbali suala la misitu na uoteshaji misitu, kuna eneo lingine la madampo haya ya kisasa. Tunapotengeneza madampo, tufikirie pia kuhusiana na suala la biashara ya *carbon*. Hata suala la maji tu, ukiweka *filter,* ni wataalam tu wajue kabla ya hapo uchafuzi ulikuwa ni kiasi gani? Ukipiga mahesabu yake hapo utakuta kuna suala zima la biashara ya *carbon* hapo katikati. Kwa hiyo, wataalam

walichukue hilo, nasi kwenye Kamati yetu tulishauri kuwa elimu hii ya *carbon* iwafikie Wabunge wote kwa ujumla wetu. Eneo hilo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye miradi ya vielelezo ya barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari. Najua ujenzi wa reli ya kati ambayo inajengwa Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma – Tabora mpaka Mwanza na Kigoma, tunaambiwa kwa kiwango cha kimataifa, ni jambo jema sana. Katika ujumla wake wakati tukiandika kile kipande cha kutoka Kaliua kwenda Mpanda na Mpanda kwenda Karema, nilikuwa naomba sana kisomeke.

Mheshimiwa Spika, leo ni kwa nini nashabikia sana suala hili la reli hii ambayo ni ya mwendokasi? Kwetu Mpanda ukipanda treni ya kawaida kutoka Mpanda mpaka ufike Dar es Salaam ni karibia siku tatu. Sasa kwa dunia ya leo na suala la wakati, wakati ni fedha, kwa hiyo, unapokutana na chombo kinachomfanya mwananchi awe na muda mrefu kwenye usafiri, anapitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa maana ya ndege tu. Kwa mfano, nikitoka Dar es Salaam kuja Mpanda natumia masaa mawili, hebu chukulia mwenzangu ana siku tatu bado anasafiri, utaionaje tija? Kwa hiyo, ndiyo maana tunapokwenda kuibadili hii miundo, pia hapa naishukuru Serikali, kwani tunaambiwa tutakarabitiwa kutoka Kaliua kuja Mpanda, kwa maana ya reli hiyo ya kizamani. Ninapozungumzia habari ya reli ya sasa hivi, ni kuiangalia dunia na mabadiliko ya wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite sasa kwenye eneo la uchimbaji madini. Naishukuru Serikali kwa ujumla wake kwa uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Naomba jambo moja katika eneo hili la uchimbaji kama nchi. Nilikuwa nafuatilia taarifa hapa, tunaambiwa kwamba nchi ya Ghana ni ya kwanza Afrika kwa uzalishaji wa dhahabu ambayo ina 117.6 *metric tons*, na Tanzania tunasomeka kama ni wa nne kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja kwamba ukija kwa maana ya dunia, tunayo nchi kama China ina 370 *metric tons,* Australia 310 *metric tons,* Russia 310 *metric tons,* Canada 200 *metric tons,* na *United State of America 170 metric tons*. Nataka kusema nini? Madini haya nasi kama Watanzania tusipofanya vizuri na tusipoangalia eneo hilo kama sehemu ya kuisaidia nchi, kwanza tukumbuke leo sisi sio wachimbaji pekee wa dhahabu duniani, zipo nchi nyingine zinachimba, lakini tunafanyaje kwa maana ya kuwawezesha wachimbaji wetu?

Mheshimiwa Spika, kama nchi, tulitenga maeneo na tukasema baadhi ya maeneo yatakuwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Nitatoa mfano, kule kwetu Mpanda kuna eneo moja linaitwa Dilifu na maeneo ya Kapanda kwa ajili ya wachimbaji wadogo, lakini sasa hivi kuna wachimbaji wengine wakubwa wameanza kurudi kwa mlango wa nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme madhara na Waziri Mkuu apaone hapa. Leo maeneo tuliyotenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo tukiyaacha yote yakachukuliwa na wachimbaji wakubwa, madhara yake ni nini? Wachimbaji wadogo kwa kupitia shughuli zao za uchimbaji, wamejiajiri wenyewe, wanaisaidia Serikali kwa maana ya shida kubwa ya suala la ajira. Kwa hiyo, hawa wote ikionekana maeneo ambayo Serikali ilikuwa imeyatenga kwa makusudi kwa ajili yao, wachimbaji wakubwa wameanza kuhodhi huko, tafsiri yake ni kwamba watakosa maeneo ya kwenda kufanya kazi, na wakikosa maeneo ya kwenda kufanya kazi, watarudi mjini na kufanya mjini kusitawalike. Kwa hiyo, nilichokuwa naiomba sana Serikali kwa unyenyekevu mkubwa, tuendelee kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, twende mbali zaidi, kwa mfano hapa tunaambiwa Tanzania kwa ujumla wake tuna wakia milioni 45 ya akiba ya dhahabu. Sasa leo ninashangaa sana tunaposomeka Tanzania ni kati ya nchi maskini duniani. Ukiangalia hotuba ya Waziri Mkuu imesheheni. Tumezungumzia misitu, maji, madini na kilimo. Kuna nchi haina msitu, kwanza ni jangwa. Wanachojivunia labda ni *gas* na kitu kingine cha namna hiyo. Sasa kwa nchi yetu

hii ya Tanzania kila kitu kipo. Kwa nini tunaangukia huko kwenye nchi maskini? Ni wapi tumekosea?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Mwanahamis Kassim Saidi ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nitaanza na shukurani kwa ajili ya mambo mengi makubwa ambayo Serikali yetu inafanya katika maeneo yetu yanayoonekana kwa macho. Hata hivyo, kwa ajili ya masilahi ya muda, nataka niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 85 na 86 wa hotuba ya Waziri Mkuu, kipengele cha 172 na 173 kinachoongelea maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana ndiyo nguvu ya Taifa lolote, vijana ndiyo *future* ya Taifa lolote. Ukitaka kujua kwamba Taifa hili baada ya miaka 10 au 20 ijayo litakuwa na nguvu gani kiuchumi, kijamii, kiulinzi ama kisiasa, unaangalia vijana wake jinsi walivyo. Ndiyo maana uwekezaji kwa vijana siyo jambo la kuchagua, ni jambo la lazima. Kuwekeza kwa vijana siyo *option,* ni *compulsory*. Tunawajibika kuwekeza kwa vijana kwa ajili ya *future* ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaeleza namna ambavyo Serikali imefanya kwa mwaka 2023/2024 kwa kuwakopesha au kuwawezesha kiuchumi vijana wetu. Ametamka kwamba, wameweza kuwawezesha vijana kwa kuwakopesha shilingi 1,270,000,000. Waheshimiwa Wabunge wengine hapa wamesema, zipo *program* mbalimbali kwa maagizo ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 26 inatutaka tuwekeze kwa vijana. Ibara ya 26(c), (d), (e) na (f) zote zinaongelea kuiagiza Serikali yake na Chama cha Mapinduzi kitakavyoisimamia Serikali katika kuwekeza kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, chama kimeongelea namna ambavyo kinaitaka Serikali yake iwawezeshe vijana kiuchumi, itoe mafunzo ya stadi za ujasiriamali, stadi za maisha, iweze kurasimisha biashara za vijana, iwe na *program* maalumu ya kuona namna gani watawawezesha vijana wa elimu ya juu na kati kujiajiri na kuajirika pamoja na kutoa mitaji na vifaa kwa vijana wanaomaliza mafunzo ya ufundi. Haya ni maelekezo ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kutoa mfano wa Taifa ambalo wenzetu wamefanya vizuri na wakafanya maendeleo makubwa. Taifa la China, tarehe 1 Julai, 2012 walifanya Mkutano Mkuu wa Chama chao cha *CPC,* Katibu Mkuu akiwepo *Comrade* Xi Jinping ambaye sasa hivi ni Rais wa China. Wakati ule, walikuja na mambo ya msingi kwa Taifa lao wakitaka Taifa lao lizaliwe upya kimaendeleo. Wakasema katika mambo ya msingi tutakayofanya, kwanza ni lazima tutambue *workforce* ya Taifa hili, ambapo wao kwa makusudi kabisa waliamua kutambua umuhimu wa vijana, waliamua kujali na kuthamini vijana, waliamua kuwaamini vijana na wakawekeza kwa vijana, wakawa na *program* za maana.

Mheshimiwa Spika, ilipofika mwaka 2021, wakati wanasherekea miaka yao 100, Rais, Xi Jinping akiwa Katibu Mkuu wa chama chao, akasema, "ni muhimu kwa vijana wetu kuona kwamba wanakuwa na *mission* ya kuchangia mabadiliko na maendeleo ya Taifa letu ili waweze kufikia malengo yao, na pia waweze kufikia na matarajio yetu sisi tunayotaka kwa vijana wetu, chama chetu na Taifa letu."

Mheshimiwa Spika, wakati huo anasema maneno haya, alisema, vijana wetu katika miaka tisa tulipotoka wameweza kujenga, kuwa *proud* kwa maana ya kujisifia kuwa wachina, lakini wameweza kuwa *proud* kuona kwamba wanawajibika kwa Taifa lao na wamekuwa na wivu wa kuwa vinara wa kuleta maendeleo, na pia wamekuwa wazalendo wa kuweza kulitetea Taifa lao kwa sababu ya maamuzi waliyoyafanya ya kuwekeza kwa vijana wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni Ofisi ya Waziri Mkuu, na kwa sensa ya mwaka 2023, vijana tulionao kwenye Taifa letu ni 20,612,566 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35, hatujaangalia 36 hadi 45. Leo unatenga shilingi 1,270,000,000 ambazo ukiwakopesha shilingi milioni/milioni kwa vijana 1,270, zimekwisha. Chama Cha Mapinduzi kimetuagiza kuwaweka vijana hawa, kuwawezesha waweze kujiajiri na wengine makundi ya wajasiriamali waweze kuwaajiri na wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii wametengewa fedha shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kupeleka kwenye maendeleo ya vijana. Mwaka 2022/2023 hawajapelekewa, mwaka 2023/2024 shilingi bilioni 18.5 hawajapelekewa, zile kule za *SDL* Fungu 65 za Wizara ya Ajira na Vijana hawajapelekewa. Zaidi ya shilingi bilioni nane ambazo zilianza tangu enzi za Marehemu Rais Mwinyi kuwawezesha vijana, tangu mwaka 1993 mpaka leo tumepeleka shilingi bilioni nane tu, ukigawa kwa miaka 31 ni kama shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, hivi Tanzania tuna *future* gani na vijana wetu? Nguvu ya Taifa letu iko wapi? Maono ya Taifa hili yako wapi? Waheshimiwa Wabunge, tunaongea sana hapa kuhusu vijana, ifike mahali tutoke na kauli moja, tuseme tunataka bajeti ya mwaka huu ije hapa na uwezeshaji wa vijana. Katika shilingi trilioni 33, basi hata tutoe *ten percent*, tutoe hata shilingi bilioni 264 zipelekwe kwenye Majimbo zikawekezwe kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali kuchagua leo kama tunaendelea kuwaacha vijana wetu wakawa ni stadi kwenye ku-*bet* na kucheza michezo ya bahati nasibu, au kama tunaamua kuwaacha vijana wetu kwa sababu tumeamua kufungu, sasa hivi *night clubs* ziko hadi mitaani kwenye makazi ya watu, au kama tumeamua kuiacha hii nguvu kazi ya vijana imalizikie kwenye pombe, maana kuna vipombe vidogo vidogo wananunua wanatembea navyo na bei yake ni nafuu tu wakinywa wana-*flat,* hawafanyi chochote. Tuamue kuchagua leo.

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote anayetaka kuliangamiza Taifa, tumeweka sana utaratibu mzuri wa kumiliki ardhi kwenye

nchi hii, ardhi inamilikiwa na umma, lakini watu wanatuangalia, mwenye akili timamu anaangalia hawa uwekezaji wao kwa vijana ukoje? Halafu anatupigia hesabu tu, baada ya miaka 10 Taifa hili halitakuwepo na tutakuja kumiliki hii nchi. Tunatenda dhambi kwa sababu yapo mataifa yanatafuta watoto wazaliwe, wanatoa na likizo ili watu wawe na watoto, sisi tunao watoto. Vijana wetu ni wa kwetu, hivyo ni *compulsory* kuwasaidia vijana wa Taifa hili, ni haki yao, siyo *option*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifike mahali tubadili namna, tukubaliane kama Wabunge, tukisimama hapa tuusemee mfuko wa vijana kila Jimbo. Watanzania sasa hivi tumekuwa wengi kila jimbo, kuna sababu gani tuwe na reli au tununue ndege wapande vijana wa mataifa mengine? Tujenge reli wasafiri vijana wa mataifa mengine! Tuweke mifumo mizuri ya kilimo waje wafaidi watu wengine! Inatupa shida hata kwenye kampeni kuelezea ununuaji wa ndege kwa sababu vijana wetu wanaona haina tija kwao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, tunapotoka hapa kwa *issue* inayohusu vijana, Serikali ije ituambie, upo utaratibu ameupendekeza Mheshimiwa Shabiby, bora tufanye hata huo, lakini tuhakikishe mfuko wa vijana unakuwepo kwenye kila jimbo, kwani ukitegemea hela ya halmashauri, haisaidii chochote, ni kidogo. Vijana ni wengi, mfuko wa vijana utekelezwe, vijana wetu wawezeshwe.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii nami niweze

kuchangia katika hoja hii muhimu ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyoko Mezani. Nianze kwa kuiunga mkono hoja hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikisimama katika itifaki ambayo Mheshimiwa Kapufi aliieleza hapo awali na namna vitabu vya dini vinavyosema, basi nami nipate nafasi ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo kwa kweli amefanya mambo makubwa kwenye Jimbo langu la Kalenga pamoja na wote wanaomsaidia Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi nzuri inayoifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jimbo la Kalenga, katika ripoti ya Waziri Mkuu tumezungumzia mambo mengi na pia tumezungumzia maeneo ya kilimo hasa upande wa kilimo umwagiliaji. Jimbo la Kalenga lina miundombinu ya umwagiliaji kama skimu 19 hivi, na limekuwa likifanya vizuri katika kuzalisha chakula ambacho Watanzania wengi wamekuwa wakinufaika. Mikoa mikubwa kama Dodoma na Dar es Salaam wamekuwa wakipata mazao kama vile njegere, viazi na mazao mengine kutoka katika jimbo langu. Kwenye miundombinu hii ya umwagiliaji tuna changamoto ya miundombinu chakavu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ione namna gani tunaeza kuwekeza katika kuimarisha miundombinu katika Jimbo la Kalenga ili sasa tuendelee kuilisha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Kata ya Nzihi ambayo mimi ninazaliwa, katika kata hii kulikuwa kuna mpango wa kujenga bwawa tangu mwaka 2007, na kila wakati nimekuwa nikizungumza na Waziri husika, nimekuwa nikizungumza na Makatibu Wakuu wanasema, "tutakuja, tunamalizia upembuzi yakinifu, hela zinakuja," lakini sasa ni mwaka wa nne naona kazi hii haifanyiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na hii ya Kata ya Nzihi Magubike kule, vile vile tuna maeneo kama Magulilwa, Mgama Wangama, Masaka Wizara ya Maji, tumejenga bwawa pale. Kwa hiyo, tunapenda wenzetu wa kilimo waende wakatengeneze miundombinu ya umwagiliaji ili tuweze kuendelea kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu Jimbo la Kalenga ambalo pia ni moja ya majimbo kongwe, hivyo miundombinu hasa ya shule za msingi, zipo shule zimejengwa miaka ya 1970, 1980, nyingine kuanzia 1960 huko nyuma. Hii miundombinu imechakaa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nzuri kabisa ambazo zinafanywa na Serikali katika kuleta fedha nyingi katika miundombinu ya kujenga shule mpya, lakini naomba Serikali sasa ione namna gani tunakwenda kukarabati zile shule kongwe. Vile vile naomba tuimarishe usafi na usalama. Kwa mfano, vyoo kwenye shule zetu za misingi, kwanza hatuna vya kutosha na pia mazingira yake siyo mazuri sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ipeleke nguvu huko na pia iimarishe miundombinu ya walimu hasa kuwajengea nyumba za kuishi na maeneo mengine kama hayo, na pia tuwe na msawazo mzuri kwenye walimu.

Mheshimiwa Spika, zipo shule nyingi, lakini nitolee mfano wa Shule ya Ilala Simba, ambako nilifanya mkutano hivi karibuni. Shule hii ina wanafunzi 460, lakini kuna walimu watano. Kwa hiyo, ukiangalia hapa, uwiano kati ya walimu na wanafunzi unakuwa ni mdogo sana. Tunatambua juhudi za Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo alivyoingia ameanza kuajiri kwa kasi, lakini bado tuko nyuma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limekuwa ni changamoto ni hasa kwa walimu wa kike. Tumepiga kelele sana juu ya walimu wa kike, tumeona sasa tumeanza kupokea lakini unakuta pengine shule ina walimu tisa wa kiume, mwalimu wa kike mmoja. Tungeangalia hapo. Wakati mwingine sasa mmoja akipata changamoto, maana yake tutakuwa hatuna mwingine kama angalau *minimum* tuwe na walimu wa kike wawili kwa sababu ya changamoto ambazo zinawakuta hawa watoto wetu wa kike.

Mheshimiwa Spika, Suala lingine kwenye upande wa *TARURA,* kazi kubwa imefanyika kwenye upande wa *TARURA,* nami Kalenga nimekuwa mnufaika mkubwa. Vile vile kutokana na mvua kuwa nyingi, miundombinu mingi sana imeharibika. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba kwenye fedha zake hizo za

dharura, tuone namna gani tunakwenda kuimarisha miundombinu ya barabara hasa kwenye vivuko. Kwa mfano, ipo barabara moja ya kutoka sehemu moja maarufu sana inaitwa Kiponzero kwenda Wasa, eneo hilo sasa mabasi hayapiti, yanazunguka eneo lingine kwa sababu miundombinu yake imeharibika sana.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kalenga ni jimbo ambalo limebahatika sana kupata wawekezaji wengi wa kigeni kama vile *Overland, Silverlands* na *Philips,* pia wako Mkwawa. Kampuni kubwa zinakuja kuwekeza kwenye kilimo na ufugaji. Kwa hiyo, ni eneo muhimu sana la kimkakati kiuchumi katika kusaidia Taifa na pia kukuza uchumi wa jamii ya Wanakalenga. Kwa hiyo, eneo hili tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye *TARURA* tuna changamoto moja, kuna barabara nyingi ambazo hazijasajiliwa. Sasa wakati mwingine ukiwaambia *TARURA,* wanasema eneo hili bwana hatuwezi kujenga kwa sababu halijaingia kwenye mtandao wa *TARURA.* Ni muhimu sana sasa *TARURA* ikahakikisha kwamba tunasajili maeneo yote yenye watu ili kufikisha huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu suala la maji. Hapa niende kitaifa kidogo. Hapa Tanzania mpaka sasa tuna vijiji 2,581 ambavyo bado havijapata maji. Tunashukuru sana juhudi za Serikali katika kuhakikisha miradi mingi inatekelezwa katika nchi hii, ndani ya miaka hii miwili tuna karibu miradi 1,700 na kitu inatekelezwa lakini bado tuna vijiji kama 1,580 vimebakia.

Mheshimiwa Spika, nafahamu tunaelekea kwenye uchaguzi, kwa hiyo, tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya uchaguzi. Hata hivyo, kwenye hivi vijiji ambavyo vimebakia, kama kwenye mfuko wetu wa maji ambao tunakisia mwaka huu tunaweza tukapata kiasi cha shilingi bilioni 170, kama tutapunguza kwenye *REA,* ingesaidia katika vijiji hivi. Kwa sababu gani? Tumeshamaliza vijiji vyote Tanzania, tunakwenda kwenye vitongoji. *REA* wanapata shilingi 70. Tunaweza kufanya maamuzi ya busara tu kwamba tuchukue

shilingi 20 kutoka kwenye *REA,* tuipeleke kwenye Mfuko wa Maji. Hapo tutapata zaidi ya shilingi bilioni 220 ambazo zitatusaidia kupeleka kwenye miradi ya kimkakati ya maji. Kwa kuwa sasa tunafikiria kuwa na gridi ya Taifa, kuwa na mpango kabambe wa maji kitaifa, ni lazima tuwe na chanzo ambacho ni muhimu na cha uhakika ambacho tunaweza kukipelekea fedha. Hilo ni eneo muhimu ambalo nilipenda tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye upande wa gesi, kama nchi tumeamua kutumia gesi iliyoshindiliwa kwenye magari, na watu wengi ambao wanatumia gesi wanafurahi kwamba gharama imepungua, na vile vile itasaidia kutunza nchi kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo ipo sasa ni kwamba vituo vya kujazia hizi gesi iliyoshindiliwa kwenye magari ni vichache sana. Kwa mfano, pale Dar es Salaam wanasema viko viwili tu; *airport,* sijui na kingine kiko Posta. Nilipofuatilia, nikauliza, kwa nini sehemu nyingine hawana? Wakasema kwamba upatikanaji wa vibali unakuwa ni mgumu kidogo. Inawezekana kuna shinikizo pengine la wafanyabiashara wa mafuta pengine wanaona biashara zao zitaharibika. Kama wanafikiri kwamba kuna fursa kwenye gesi na hao wenzetu ambao wanafanya biashara za mafuta, basi nao wachukue uwakala ili nao wapate faida inayotokana na gesi.

Mheshimiwa Spika, nilimsikia Mheshimiwa Rais wakati anawaapisha viongozi hawa aliowateua hivi karibuni pale Dar es Salaam jana, akazungumzia suala la maji, akasema kwamba sasa tuwe na *pre-paid meters.*

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia kwenye mamlaka zetu, nami kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maji nafahamu, mamlaka zetu bado hazina uwezo mkubwa wa kununua mita hizo kwa wingi *(in bulk)*. Nikafikiri sana kwamba katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuna hii mifuko ya fedha, nilishazungumza kwa kifupi kwenye Bunge lililopita kwamba, kuna *PSSSF* ambao wamekuwa wakiwekeza sana kwenye miradi mikubwa ya majengo. Unakuta ghorofa 20, ghorofa 17, lakini nikawa nawaza sana kwamba je, ukiwekeza

kwenye maghorofa 17 au 20 na nchi ya Tanzania haina uhaba wa ardhi, je, kwa utamaduni wa Watanzania, ni kweli mtu atakwenda kupanga Ofisi yake ghorofa ya 20? Au wakati mwingine tunataka tu tuonekane kwamba hii Bodi imefanya kazi nzuri, imejenga majengo mazuri! Je, majengo yana tija? Je, tunapata *return*?

Mheshimiwa Spika, nifikiria ni kwa nini wenzetu wa mifuko hii wasipeleke fedha wakawekeza kwenye hizi *pre-paid meters* halafu zikalipwa ndani ya muda mfupi? Inawezekana tutapata makusanyo makubwa. Kwa hiyo, hilo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, muda wetu umekwenda, halafu nina Wabunge wawili hapa; Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda. Mheshimiwa Mwanakhamis Said.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafsi hii nami niweze kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Jenista. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana dada yangu Mheshimiwa Jenista, kwa kweli anastahili sifa sana, ni Waziri mmoja malkia wa nguvu. Nawaomba Waheshimiwa Mawaziri, hususan wanawake wafuate nyayo za Mheshimiwa Jenista. Ni mama mmoja jasiri, hana kiburi, hana jeuri, kwa kweli ni mchapakazi, anaisadia nchi yetu kwa nguvu sana na kwa kweli anaonekana. Ninampongeza na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee na roho hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mimi nikisimama hapa ni kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan Mwanzo mwisho. Ni mwanamke aliyetutoa kimasomaso wanawake, ni mwanamke anayewasimamia wanawake kwa sababu hata wanawake ambao anawapa nafasi wanaweza kufanya kazi kwa nguvu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi tunanyanyuka kumsifu Mama Samia, na hakuna Mbunge anayesimama hapa asimsifu Mheshimiwa Dkt. Samia na kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia anafanya kazi kubwa sana. Mama Samia ni miaka yake mitatu anafanya kazi na watu wote wanamwona, nchi nzima wanamwona. Mama Samia ameingia kwenye utawala wake, alikula kiapo kwamba atawasimamia na atawasaidia Watanzania. Mama Samia hakutawala akasema anatawala miili ya watu, bali anatawala nyoyo za watu. Hii ndiyo sababu leo tunaposimama Waheshimiwa Wabunge sote kila mmoja anasema Mama Samia amefanya mambo mazuri. Huyo ni mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binadamu siku zote huwezi kumfurahisha na akafurahi. Mitume walifanya mambo mazuri, lakini walipigwa mawe na wengine wakasulubiwa. Kwa hiyo, huwezi ukamridhisha binadamu. Hata hivyo, Mama Samia anafanya mambo makubwa sana. Alipoingia kwenye utawala wa nchi hii ya Tanzania kwa kula kiapo, alikuta nchi ipo kwenye tafrani kubwa sana. Watanzania hatupatani, tunagombana, lakini alichukua jukumu la kuwapatanisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo kubwa sana kwa binadamu hata kwa Mwenyezi Mungu. Binadamu atasema nini anafanya, lakini Mwenyezi Mungu anajua kitu kikubwa anachokifanya Dkt. Samia. Amewasimamia Watanzania walioko Ulaya, wamerudi nchini; walioko ndani aliwatoa, *lakini Watanzania hawa leo aliowarejesha kutoka Ulaya, wanashiba Ulaya, wanakuja kuhara Tanzania, na wanapokuja kuhara hapa, hushuka airport kwenye ndege kubwa, na wanalindwa na askari wetu, wanakuja wanatuharia, kesho wanaondoka wanakwenda zao Ulaya. Kwa*

*kweli watu hawa wanasikitisha na hiki wanachokizungumza wanapokuja kwenye nchi yetu. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamis, hebu weka lugha yako vizuri hapo.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nafuta usemi wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia alipokuja kuwaunganisha Watanzania, aliitwa kwenye vyama vya siasa wanapofanya mikutano, yeye ndiye aliyekuwa anakwenda kuhutubia na walikuwa wanamshangilia, wanampigia makofi. Leo watu hawa hawa wamehamia kwenye mitandao wanamtukana kwa maneno ambayo hayana maana. Tunapozungumza akina mama wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge tunaosema Mheshimiwa Dkt. Samia miaka mitano tena, tunamaanisha. Tunasema Mama Samia miaka mitano tena, anaweza kuwatengenezea Watanzania wa nchi hii mambo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi, kuna mambo mengi ameyafanya, miradi mingi sana, kwenye afya, elimu, kilimo, barabara na miundombinu kadha wa kadha. Kuna miradi aliianza Mheshimiwa Marehemu Dkt. Magufuli, lakini leo Mheshimiwa Dkt. Samia ameimaliza miradi mingi sana. Kwa hiyo, tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia tunampa mitano tena na mingine mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiachia hapo, nianze kuzungumzia barabara ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam. Kwa kweli kuna maeneo barabara kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam imeharibika sana. Kuna matuta hayana alama, kwa hiyo, ni matuta hatarishi. Naiomba Serikali, barabara hii waisimamie kwa nguvu zao zote kwa muda mchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze kuhusu Bandari ya Dar es Salaam. Kwa kweli Bandari ya Dar es Salaam hapajakaa sawa.

Naiomba Serikali, pale bandarini jamani ni wananchi wengi wanaopita pale, ni wapigakura wengi wanaopita pale. Kipindi kama hiki cha sikukuu watakuja watu wengi kununua nyama Dar es Salaam kwa sababu Zanzibar nyama ni kidogo, hivyo inakuwa ni ghali, kwa hiyo, huku Dar es Salaam inakuwa ni afadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu ananunua nyama yake kilo kumi na kuku wake watano, akifika pale anaambiwa atafute kibali. Kibali hicho haijulikani atakipata wapi? Akifika anasumbuliwa na kuhangaishwa. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge masuala haya tunafanyiwa. Wanaopita pale ni Watanzania, wapigakura wetu. Kuna mambo lazima yashughulikiwe. Tunapozungumza hapa hatusemi kama kwa kutaka sifa, tunataka yale mambo yashughulikiwe. Kwa kweli ni tatizo, hatupendi kugombana na Serikali. Kwa sababu kama sisi Waheshimiwa Wabunge tunapita tunanyanyasika hivyo, je, huyo mwananchi ambaye sio Mbunge atakuwa anasumbuka vipi? Tunaomba suala hili lichukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niiambie Serikali, jamani huku kwenye maduka ya wafanyabiashara zilitolewa mashine ambazo zilinunuliwa na Serikali kwa gharama kubwa, lakini mashine zile leo zimetiwa kwenye ma-*box*. Wafanyabiashara hawazitumii, nasi tunaokwenda madukani tunaona kama Serikali wamenyamaza kimya, wameridhika, wananchi hawapewi risiti. Unakwenda unanunua kitu cha shilingi milioni mbili, unapewa risiti ya shilingi laki moja na nusu. Kwa kweli inasikitisha sana. Tutapata wapi pesa za dawa? Tutapata wapi pesa za kutengenezea miundombinu ya barabara iwapo shilingi mia inayotuingizia inaenda? Itakuwa Mama Samia anahangaika huku na kule, lakini pale kwenye pesa ya uhakika haipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali na wale wanaosimamia, kuna sehemu zao wazisimamie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilisema hapa kuna majina mawili zaidi, lakini kwa muda wetu uliobaki na wengine inabidi wawahi kwenye suala kabla ya *Iftar* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, watachangia Jumatatu.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji siku ya leo, na tutaendelea kwa kadri ya siku zetu tulizojipangia kwa ajili ya kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake.

Nina tangazo hapa kabla sijaahirisha shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, kwa maana ya Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, leo mara baada ya kuahirisha shughuli hizi kutakuwa na kikao hapo nyuma *Speaker's Lounge*. Kwa hiyo, nikiahirisha tu hizi shughuli, tukutane hapo kwa ajili ya kikao muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge, kuna Wabunge wakati wa kusalimiana, kuinama kulia na kushoto, sijui wao huwa wanawaza nini? Ni kama mtu akupe mkono halafu usimsalimu, kwa sababu ile ni salamu. Sasa mimi nakusalimu, halafu wewe unanipita. Ni salamu ile. Kwa hiyo, tuagane vizuri kama ambavyo tunasalimiana vizuri asubuhi.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.04 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 8 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*